**7 NOVEMBA, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Saba – Tarehe 7 Novemba, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 36 la Tarehe 08 Septemba, 2023;
2. Toleo Na. 37 la Tarehe 15 Septemba, 2023;
3. Toleo Na. 38 la Tarehe 22 Septemba, 2023;
4. Toleo Na. 39 la Tarehe 29 Septemba, 2023;
5. Toleo Na. 40 la Tarehe 06 Oktoba, 2023;
6. Toleo Na. 41 la Tarehe 13 Oktoba, 2023;
7. Toleo Na. 42 la Tarehe 20 Oktoba, 2023;

8. Toleo Na. 43 la Tarehe 27 Oktoba, 2023; na
9. Toleo Na. 44 la Tarehe 03 Novemba, 2023.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu.

Katibu.

**NGD. LAWRENCE MAKINGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Anton Albert Mwantona Mbunge wa Rungwe sasa aulize swali lake.

Na. 87

### Halmashauri ya Mji Mdogo Tukuyu kupewa mamlaka kamili

**MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, ni lini Halmashauri ya Mji Mdogo wa Tukuyu itapewa mamlaka kamili baada ya kukamilisha taratibu na kukidhi vigezo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Jimbo la Rungwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala upo kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Sura ya 287 na 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014. Hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe inashauriwa kufuata utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa sasa Serikali imetoa kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha

miundombinu msingi kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadae kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anton Albert Mwantona swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nifanye marekebisho kidogo, siyo Halmashauri ya Mji wa Tukuyu ni Mji wa Tukuyu, kwa mujibu wa taratibu na sheria nataka nijue majukumu hasa miji midogo ni nini? Wale watumishi wa miji midogo wanatakiwa wafanye majukumu gani hasa katika ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niiombe Serikali kama ingeweza ikaandaa mwongozo ambao utasaidia hii miji midogo kuweza kujitegemea na kukua ili hatimaye baadae wawe na uwezo kuwahudumia wananchi katika maeneo yao ya kiutawala hasa katika ukusanyaji wa mapato na matumizi na kuyasimamia matumizi hayo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Jimbo la Rungwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka za miji midogo zilianzishwa kwa mujibu wa sheria na zina majukumu yake na zina Baraza la Madiwani wa Mamlaka ya Mji Mdogo. Pia zina mtendaji wa mamlaka lakini pia zina mwenyekiti wa mamlaka ya mji mdogo. Kazi zao pamoja na majukumu mengine ni pamoja na kuhakikisha kwamba zinakusanya mapato katika eneo lao la utawala katika mitaa yao. Pia kuwasilisha mapato hayo katika *account* ya halmashauri mama ambapo mkurugenzi wa halmashauri ndiye *accounting officer* wa halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusimamia miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa katika mitaa ambayo inaunda mamlaka ya mji mdogo, Mamlaka ya Mji Mdogo ni hatua ya kwanza ya kuelekea kupata kibali au kupandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji. Kwa hiyo, hii ni hatua ya mwanzo wakati wanajenga uwezo wao kujiendesha kuelekea kwenye Halmashauri ya Mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swala la pili; kuhusu mwongozo wa miji hii kujitegemea, kwa sababu hii ni hatua ya kukua kuelekea kwenye Halmashauri ya Mji maana yake ukishafika hatua ya Halmashauri ya Mji wanakuwa na mkurugenzi ambaye ndiye *accounting officer* na inakuwa ni Baraza la Madiwani la halmashauri ya mji mambalo lina majukumu yote kwa mujibu wa sheria za Serikali za Mitaa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Joseph Kakunda swali la nyongeza

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana natambua kwamba kijiji ni mamlaka ya utawala, kata ni mamlaka ya utawala na halmashauri ya mji au ya wilaya au jiji ni mamlaka ya utawala. Nafahamu msimamo wa Serikali kuhusu uendeshwaji wa mamlaka za kiutawala. Sasa swali langu, jimbo siyo mamlaka ya utawala, Jimbo langu la Sikonge ili nifike kwenye tarafa ile ya mradi natembea *kilometre* 200, ili nifike kwenye Kata ya mbali kabisa mpakani mwa Singida…

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: …**natembea *kilometre* 400. Sasa swali langu ni kwamba kwa nini Serikali hairuhusu uanzishwaji wa majimbo mapya ili uwakilishi wa wananchi uwe mzuri zaidi hapa Bungeni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nijibu swali la nyongeza la

Mheshimiwa Joseph Kakunda Mbunge wa Jimbo la Sikonge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na ni sahihi kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema kuhusiana na mamlaka za utawala katika ngazi za vijiji, kata, halmashauri na maeneo mengine. Pili, jimbo ni eneo ambalo linauwakilishi wa wananchi na yeye ndiyo Mbunge wa jimbo hilo. Namshauri kwa sababu taratibu za kuomba majimbo mapya zinafahamika nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge afuate taratibu zile na kufikisha mahala ambapo kuna mamlaka hiyo hiyo ili waweze kuona uwezekano wa kuchukua hatua hizo kwa mujibu wa mahitaji ya jimbo lake, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dennis Londo swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya Mji Mdogo wa Mikumi ina zaidi ya umri wa miaka 20 na mchakato wa kuomba halmashauri ulishapita katika ngazi ya wilaya, mokoa na TAMISEMI na kwa kuwa Jimbo la Mikumi au Tarafa ya Mikumi siyo halmashauri wala siyo makao makuu ya wilaya imepitwa na fursa zote za miradi ya kimkakati. Je, nini mpango wa Serikali katika kukumbuka miji hii ambayo haina hadhi ya wilaya au halmashauri katika miradi mikubwa ya kimkakati kama *TACTICs* na miradi mingine?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dennis Londo Mbunge wa Jimbo la Mikumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa mamlaka za miji midogo ikiwemo Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mikumi ulianzishwa kwa dhamira njema ya Serikali kuhakikisha kwamba inasogeza huduma za jamii karibu zaidi na wananchi. Hiyo ndiyo sababu ya

msingi Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mikumi ilianzishwa lakini pia na mamlaka za miji midogo maeneo mengine kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mikumi kwa kuwepo kazini kwa zidi ya miaka 20 lakini pia kwa kuwasilisha maombi ya kuomba kuwa Halmashauri ya Mji wa Mikumi kwa kufuata taratibu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunatambua kwamba Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mikumi ishawasilisha maombi yao na taratibu zinazoendelea sasa ni kujiridhisha na vigezo hivyo. Pale wakati utakapofika kwa ajili ya kuanzisha Halmashauri ya Mji wa Mikumi basi hatua hizo zitachukuliwa kwa manufaa ya wananchi wa Mikumi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 88

**Mpango wa kuweka Kitengo cha Watoto Njiti Wilaya ya Mbozi**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Kitengo cha Watoto Njiti katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kipaumbele katika Sekta ya Afya ni kupunguza vifo vya wajawazito, watoto chini ya miaka mitano na watoto wachanga kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi, katika kipindi cha mwaka 2015/2016 hadi kufikia 2022/2023 vifo vya wajawazito vimepungua kutoka vifo 556 katika

kila vizazi hai 100,000 hadi 104 katika kila vizazi hai 100,000. Vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 67 katika kila vizazi hai 1000 hadi 43 katika kila vizazi hai 1000 mtawalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetenga shilingi milioni 900 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali Kongwe ya Mbozi. Pamoja na ukarabati na ujenzi wa miundombinu utakaofanyika katika hospitali ya Halmashauri ya Mbozi, kipaumbele kimewekwa kwenye jengo la huduma za mama na mtoto ikiwemo huduma za watoto njiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juliana swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuwa Hospitali yetu ya Wilaya ya Mbozi ni chakavu sana kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyosema na hizi fedha ambazo zimetengwa kwa kweli ni kidogo. Sasa nataka nifahamu kwamba Serikali ina mpango gani au mkakati gani wa kudumu kuhakikisha kwamba majengo yote ya Hospitali ya Wilaya ya Mbozi yanakarabatiwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza kwamba Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ni hospitali kongwe ni hospitali chakavu. Ndiyo maana kwa utashi na mapenzi mema ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ameainisha hospitali hiyo miongoni mwa hospitali 19 nchini kote za kipaumbele kwa ajili ya kutenga fedha kuhakikisha majengo yanakarabatiwa na kuwa na hadhi ya hospitali ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Mheshimiwa Rais tayari ameshatenga shilingi milioni 900 katika bajeti ya mwaka huu na itapelekwa kwa ajili ya ukarabati. Tutaendelea kutenga fedha kwa awamu kuhakikisha majengo yote ya Hospitali ya

Halmashauri ya Mbozi inakarabatiwa na kutoa huduma nzuri kwa wananchi wa Mbozi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea, Mheshimiwa Fransis Isack Mtinga Mbunge wa Iramba Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 89

**Uboreshaji wa Vituo vya Afya vya Kinyangiri na Mkalama**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaboresha Vituo vya Afya vya Kinyangiri na Mkalama katika Halmashauri ya Mkalama kwa kujenga majengo ya upasuaji na wodi ili kuwa na hadhi ya Vituo vya Afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Kinyangiri na Mkalama vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ni miongoni mwa vituo vya Afya 199 chakavu ambavyo Ofisi ya Rais TAMISEMI imeviainisha kwa ajili ya kuvitafutia fedha na kuvifanyia ukarabati na upanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati na kuongeza majengo kwenye vituo vya afya chakavu kote nchini vikiwemo vituo vya afya vya Kinyangiri na Mkalama. Vituo hivi vitapewa kipaumbele kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya upasuaji na wodi mara fedha zitakapopatikana, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Isack swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali yanayotia moyo nina maswali mawili ya nyongeza. Kituo cha Afya Mkalama ni kituo chakavu sana kinazidiwa hata hadhi na baadhi ya zahanati. Je, Serikali haioni haja sasa ya kutamka kabisa rasmi kwamba ni lini watakwenda kufanya ukarabati kwenye kituo hiki ambacho kinahudumia tarafa kubwa sana yenye watu wengi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Kituo cha Afya Kinyangiri Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi alipita pale na kutoa ahadi na akaweka na *dead line* kwamba mwezi wa 12 mwaka huu kitakuwa kimeshafanyiwa upanuzi na ukarabati. Mwenyekiti wa CCM ambaye ni Rais wa Jamhuri Muungano wa Tanzania akakazia ahadi hiyo juzi alivyokuja Singida. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kutamka rasmi kwamba wanakwenda kufanya ukarabati kwenye kituo hiki kwa kuzingatia kauli za wakubwa wa nchi hii?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Isack Mtinga Mbunge wa Jimbo la Irambva Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Kituo cha Afya hilki cha Mkalama ambacho ni chakavu sana Serikali imekwisha kiainisha kama nilivyotangulia kusema. Hivi sasa tuko kwenye utaratibu wa kutafuta fedha na fedha ikipatikana mapema iwezekanavyo itapelekwa Halmashauri ya Mkalama kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya cha Mkalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mkalama kwamba Serikali inatambua uchakavu wa Kituo cha Afya. Inatafuta fedha na mapema iwezekanavyo fedha ikipatikana tutahakikisha kinakarabatiwa na kuwa hadhi ya kituo cha afya kama vilivyo vituo vya afya vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Kinyangiri ni kweli ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi. Sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kipaumbele na natoa kauli rasmi kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwamba tunakwenda kutekeleza ahadi ya Rais. Tunakwenda kutekeleza ahadi ya Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi mapema iwezekanavyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Pallangyo swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Changamoto zilizoko Iramba Mashariki zinafanana sana na Changamoto zilizoko Arumeru Mashariki katika Sekta ya Afya. Je, ni lini Serikali itakuja kuboresha Kituo cha Afya Makida ambacho majengo yake yamekuwa magofu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue hoja ya Kituo cha Afya cha Makida ambacho ni chakavu na kinahitaji ukarabati ili tuweze kutuma wataalam wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI lakini pia Mkoa wa Arusha kufanya tathmini na kutuletea makadirio ya gharama zinazohitajika ili tutafute fedha kwa kupitia mapato ya ndani lakini mahususi kupitia Serikali Kuu ili tuweze kukarabati kituo hiki cha afya kiweze kutoa huduma vizuri, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amsabi swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuwa Kituo cha Afya Iramba, Wilayani

Serengeti ni cha muda mrefu na kimechakaa sana ni lini sasa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa kituo hiki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amsabi Mrimi, Mbunge wa Jimbo la Serengeti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumuelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mara na Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Serengeti kufanya tathmini kwa maana ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya ukarabati wa kituo hiki cha afya na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kufanya tathmini lakini pia kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa kituo hicho, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Jimbo la Singida Mashariki lina kata 13 lakini tulijaliwa kupata kata moja tu ndiyo imejengewa kituo cha afya.

Je, ni lini sasa Serikali itajenga vituoa vya afya vya kata ya Misughaa na Issuna ili kuweka uwiano mzuri katika mkakati wa afya? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Miraji Mtaturu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mpango wa Serikali wa kujenga vituo vya afya vya kimkakati ni endelevu. Hivi sasa Serikali imeendelea kutafuta fedha kupitia mapato ya ndani ya Serikali Kuu, kupitia mapato ya ndani ya halmashauri lakini pia wadau

mbalimbali kuhakikisha yale maeneo ambayo yameainishwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kimkakati yanajengwa vituo hivyo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Mtaturu kwamba tutatoa kipaumbele katika kata hizi zmbazo ameziainisha iloi pia ziweze kupata vituo vya afya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kajege swali fupi la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itajenga maabara na wodi ya kina mama na Watoto katika Kituo cha Afya cha Kasuguti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa ujenzi wa vituo vya afya ambavyo vina majengo pungufu kwa kadiri ya *standard* ya vituo vya afya ni mpango ambao unaendelea kutekelezwa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuweka mipango kwa ajili ya kutafuta fedha lakini kwa ajili ya kwenda kufanya ujenzi wa majengo hayokatika kituo hiki cha afya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji Mheshimiwa Oran Manase Njeza sasa aulize swali lake.

Na. 90

**Mkakati wa kujenga viwanda maalum na maghala ya ubaridi**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, kuna Mkakati gani wa Kujenga Viwanda Maalum na Maghala ya ubaridi kwenye eneo la *Tanganyika Packers* Mbalizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Kigahe.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la *Tanganyika Packers Mbalizi* Shamba Na. 761 la kulishia mifugo la Nsalala lenye ukubwa ekari 4,900, Serikali imeshafanya maamuzi ya kulikabidhi eneo hilo kwa Mamlaka ya Maeneo Maalum kwa Mauzo Nje *(EPZA)* kwa ajili ya uwekezaji. Baada ya makabidhiano, eneo hilo litatumika kwa ajili ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa viwanda mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua maoni ya Mheshimiwa Mbunge ya ujenzi wa viwanda maalum na maghala ya ubaridi katika eneo hilo na itayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa majibu mazuri sana na pia kwa mikakati mizuri kuhakikisha eneo hili linatumika kiuchumi kwa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile hili eneo liko mkabala na *TAZARA* na uwanja wa kimkakati wa Songwe na barabara ya TANZAM, je, Serikali ina mpango gani wa kutenga eneo kwa ajili ya bandari kavu na kujenga bandari kavu katika eneo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya umuhimu wa eneo hilo, je, ni lini Serikali itaanza upimaji na kutenga maeneo ya eneo hili muhimu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli Mkoa wa Mbeya ni moja ya mikoa ya kimkakati ambayo Serikali inauangalia kuhakikisha unawekezwa vizuri, kwa maana ya miundombinu wezeshi. Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ni kweli eneo hili ni la kimkakati kwa sababu linapitiwa na barabara kuu inayoenda Zambia. Pia, kuna uwanja wa ndege na reli ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maeneo ambayo Serikali inaweka mkazo ni kuweka miundombinu wezeshi yote. Hili suala la bandari kavu ambalo litasaidiana na miundombinu hii mingine nalo ni moja ya maeneo ambayo tunayaangalia ili kuboresha eneo hili ili liwe sehemu ya kusaidia kukuza biashara, kuuza nje lakini pia kuingiza bidhaa ambazo zinatoka maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunasema eneo hili ni kwa ajili ya uwekezaji mauzo nje kwa sababu tunategemea baada ya miundombinu kukamilika na bandari kavu pia itasaidia kuuza nje, kwa maana ya kuuza bidhaa zinazozalishwa katika eneo lile kwenda nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upimaji, katika bajeti hii inayokuja tunayoenda nayo ni moja ya maeneo maalum ambayo tutaangalia namna ya kuyapima ili yaweze kutumika kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na miundombinu mingine ikiwemo bandari kavu katika eneo hili la Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kassinge swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa swali la nyongeza. Kumekuwa na mpango wa muda mrefu wa Serikali kujenga kiwanda cha mbolea kinachotokana na gesi asilia ya Songosongo pale Mjini Kilwa Masoko. Kauli ya mwisho ya Serikali ni kwamba iko kwenye mazungumzo na mwekezaji. Nataka kufahamu na wana-Kilwa pia wanataka kufahamu;

Je, mpango wa kujenga kiwanda cha mbolea Kilwa-Masoko bado uko pale pale au umesitishwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni sahihi kabisa moja ya mipango ya Serikali ni kuhakikisha tunajenga viwanda vingi vya kutosheleza mahitaji ya mbolea nchini. Ninyi ni mashahidi, tumeshaanza kujenga hicho cha *Intracom* hapa Dodoma lakini pia tunacho kile cha Minjingu ambacho kinaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki cha Kilwa-Masoko ni mahsusi kwa sababu hawa watatumia gesi asilia ambayo nayo ni muhimu sana kwa ajili ya kuzalisha mbolea ambazo zinahitajika hapa nchini. Kwa hiyo, mpango wa Serikali ni kuhakikisha tunaendelea kutafuta wawekezaji na kukamilisha mipango hiyo. Ujenzi wa kiwanda hiki cha mbolea katika eneo hili la Kilwa-Masoko utatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo. Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima Mbunge wa Kawe sasa aulize swali lake.

Na. 91

**Mpango wa kudhibiti Mito ya Nakasangwe na Tegeta**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza: -

Je, ni nini Mpango wa Serikali kudhibiti Mto Nakasangwe na Mto Tegeta n a kadhalika inayopanuka kwa kasi na kutishia maisha ya watu na mali katika Jimbo la Kawe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Khamis Khamis majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira naomba kujibu swali la Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Jimbo la Kawe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto za kupanuka kwa Mto Nakasangwe na Mto Tegeta kama ifuatavyo:

i. Kuandaa Mwongozo wa usafishaji mchanga, tope na taka ngumu kwenye mito na mabonde kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

ii. Kutoa elimu kupitia vipindi vya redio, televisheni, maonesho na mikutano kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa vyanzo vya maji katika ngazi zote ili kuongeza kasi ya uhifadhi vya vyanzo vya maji na kingo za mito.

iii. Kuhamasisha Umma kuhusu upandaji wa miti rafiki kwa vyanzo vya maji ambavyo itasaidia katika kuzuia mmomonyoko wa kingo za mito na kuimarisha mtiririko wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kusisitiza utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 kuhusu uhifadhi ya eneo la mita 60 katika kingo za mito, fukwe za bahari na maziwa yanayozuia matumizi yeyote ya kibinadamu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa kutambua kupanuka kwa kingo za mto Tegeta na Nakasangwe, Serikali itaangalia uwezekano wa kufanya tathmini katika maeneo hayo kwa lengo la kupata suluhisho la kudumu kama ilivyofanyika katika maeneo mengine ambapo Serikali ilibuni na kutekeleza miradi ya ujenzi wa kuta, kama vile ujenzi wa ukuta wa Pangani na fukwe katika Barabara ya Barak Obama katika jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naona umeridhika na majibu. Mheshimiwa Dkt. Gwajima swali la nyongeza.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya mvua nyingi zinazoendelea katika Jiji la Dar es Salaam mito mingi imejaa na kumwaga maji kwenye nyumba za wananchi; na watoto wengi wameshindwa kwenda shule kwa sababu ya mito hiyo na imehatarisha maisha ya watu na nyumba za watu.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kusaidia kudhibiti mito hii isiharibu maisha ya watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Mto Nakasangwe, Mto Tegeta, Mto Mbezi, Mto Ndumbwi na Mto Mpiji miaka miwili iliyopita ilikuwa na upana wa mita 50 tu leo ina upana wa mita 100.

Je, Waziri utakubali kwenda pamoja na mimi ukaione mito hii wewe mwenyewe na utafute ufumbuzi wa kudumu wa kudhibiti mito hii kwa ajili ya kuokoa mazingira? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge Askofu Gwajima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kumpa pole sana Mheshimiwa Gwajima kwa kuingiliwa kwa maji katika maeneo yale, mito mingi imefurika. Lakini pia nachukua fursa hii kumpongeza sana mpaka jana usiku nilikuwa naangalia kwenye vyombo vya habari yupo Kawe anawasaidia Wananchi, anashirikiana nao katika janga hili la kuingiliwa kwa maji. Nataka kuchukua fursa hii pia kuwapa pole Watanzania wote ambao wameathirika na mvua kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mipango ya dharura ambayo tunakwenda kuifanya kama Serikali kuhakikisha kwamba tunatatua hii changamoto ya kufurika kwa mito na maziwa na maeneo mengine ambayo yanajaa maji yanaathiri wananchi; kwanza ni kwenda kutafuta fedha kuhakikisha kwamba tunajenga kuta ambazo zitazuia maji yasiingie kwenye makazi ya wananchi. Pili tutahakikisha tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wajue athari za mvua na athari za kukaa kwenye mabonde, na pia wajue namna ya kuweza kuondoka mapema kabla mvua hizi hazijaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti vilevile, tunakwenda kuishirikisha jamii kwenye masuala ya usafi wa mito, mitaro na maeneo mengine ambayo yanakwamisha maji yasiende mwisho wa siku yanasabisha maafa. Kubwa ni utekelezaji wa Sheria ile ya mita 60 kama ilivyozungumzwa katika Kanuni ile ya 191 ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa jambo hili na kazi kubwa anayoifanya Dkt. Gwajima nipo tayari kwenda Jimboni Kawe kushirikiana na Wananchi kuhakikisha kwamba tunawasaidia katika kuondokana na hii changamoto ya uingiaji wa maji katika makazi yao, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Sitta swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono kabisa Dkt. Gwajima mchungaji, ameelezea vizuri. Mimi nina *video* moja hapa ambayo ukimaliza kujibu maswali tuonane. Hali ni mbaya Tegeta na kuna chanzo chake, ni kwa sababu walipokuwa wanajenga barabara ile ya kwenda Bagamoyo waliziba mifereji. Hali ni mbaya ukirudi hapa Mheshimiwa niruhusu nikuonyeshe *video* ya hali mbaya iliyoko. Nakupongeza Mheshimiwa kwa kazi uliyofanya hali ni…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Sitta uliza swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bee?

**MWENYEKITI:** Swali?

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa kwanza na-*express. (Kicheko)*

Je, ni lini Serikali kupitia *TANROADS* watazibua mifereji waliyoziba walipokuwa wanajenga barabara ya kwenda Bagamoyo? Hali ni mbaya naomba nimuonyeshe na *video***.** *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wakati mwingine Serikali inapokuwa inafanya utengenezaji au ukarabati wa miundombinu hasa ya barabara zipo changamoto ndogondogo huwa zinatokea. Siku zote tunapojenga lazima tutabomoa, na tukibomoa lazima kuna kasoro zitajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuambia Mheshimiwa Mama Sitta kwamba tuko tayari kushirikiana na Wizara inayohusika kwa maana kwamba Wizara nyingine za kisekta. Lengo na madhumuni ni wanapojenga au wanaporekebisha miundombinu ya barabara wahakikishe kwamba wanatengeneza mazingira mazuri ya kupitisha maji ili kipindi cha mvua nyingi maji yaweze kupenya na yaende baharini yasiathiri makazi ya watu, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante naona Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Bashungwa.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Natumia nafasi hii kuwaelekeza Meneja wa Mikoa *TANROADS*

kote nchini kwenda kwenye maeneo ambayo yana changamoto kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema na kuleta haraka iwezekenavyo namna ambavyo tunaweza tukakabiliana na jambo hili kwa dharura, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 92

**Muundo wa Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha muundo wa Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mnyeti, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agness Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo *(organization Structure)* wa Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi yaani *Fisheries Education and Training Agency - FETA* uliokuwa ukitumika ulipitishwa tarehe 1 Oktoba, 2018. Muundo huo ulikuwa unaendana na matakwa ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi yaani *National Council for Technical and Vocational Education and Training - NACTVET*, ambalo ndio linaratibu vyuo vya ufundi stadi ikiwemo *FETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto ya vyuo vinavyoratibiwa na *NACTVET* kuwa na miundo isiyofanana, *NACTVET* walihuisha miundo ya vyuo wanavyo viratibu ili kuongeza tija katika utoaji elimu na pia kupunguza gharama za uendeshaji. Hivyo, kufuatia uhuishaji huo wa *NACTVET*, muundo mpya wa *FETA* uliidhinishwa Novemba, 2022 na kwa sasa Serikali inaendelea na taratibu za kujaza nafasi za uongozi katika muundo huo mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Agnes swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya vyuo katika taasisi hizo kama vile Mtwara–Mikindani, Kibirizi–Kigoma, Gabimori–Rorya mameneja wake wamekaimu kwa kipindi kirefu sana kuanzia miaka saba mpaka kumi na moja;

i. Je, Serikali haioni inafifisha malengo ama maelekezo ya Chama cha Mapinduzi katika vyuo hivyo kutoa mafunzo kwa sababu havina mameneja wa kudumu?

ii. Je, Serikali itakapokamilisha mchakato huo wa kujaza hizo nafasi kwa muundo uliokamilika tangu Novemba 2022, iko tayari kuwalipa mameneja hao wanaokaimu akiwemo meneja wa Mtwara-Mikindani aliyokaimu kwa miaka 11 kwa nafasi hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nampongeza sana dada yangu Agnes kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia sana chuo hiki na kwa kweli kama Wizara tunatumia nafasi hii kumpongeza sana kwa jinsi ambavyo anafuatilia habari hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kweli kwamba kuna makaimu katika vyuo vingi vinavyohusiana na masuala ya uvuvi. Napenda kutumia nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba makaimu hao sasa watakwenda kuthibitishwa, wale wenye vigezo. Jambo hili liko kwenye upekuzi na upekuzi upo katika hatua za mwisho namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba linakwenda kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili alilosema kuhusu mameneja waliokaimu kwa muda mrefu taratibu za kiutumishi zinafahamika. Kama watakuwa na sifa za kulipwa basi watalipwa, Serikali iko tayari kuwalipa na kama watakuwa hawana sifa za kulipwa basi hawatalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Kilimo, swali namba 93 limeshajibiwa na limeshatekelezwa kwa hiyo tunaendelea na Swali Namba 94. Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Kyela sasa aulize swali lake.

Na. 94

**Mfumo wa uuzaji wa zao la Kokoa – Kyela**

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itahakikisha mfumo wa uuzaji wa zao la Kakao unaomnufaisha mkulima badala ya wafanyabiashara wachache?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Ernest Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Jimbo la Kyela kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la kakao huuzwa kupitia mfumo wa Stakabadhi Ghalani chini ya utaratibu wa minada inayoratibiwa na vyama vya ushirika. Mfumo huo ulianza kutumika mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo bei ya kakao imeendelea kuimarika kulingana na mahitaji ya soko. Wastani wa bei ya kakao kwa kilo kuanzia msimu wa 2018/2019 ilikuwa shilingi 4,611; 2019/2020 ilikuwa shilingi 5,034, mwaka wa fedha 2020/2021 ilikuwa shilingi 4,818, mwaka wa fedha 2021/2022 ilikuwa shilingi 4,711 na hadi kufikia tarehe 23 Oktoba msimu wa mwaka wa fedha 2023/2024 wastani wa bei ya kakao kwa kilo ni shilingi 8,079.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya uuzaji wa mazao nchini ili kuongeza ushindani na kumnufaisha mkulima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Anyigulile swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Serikali ndiyo wanaondesha mfumo huu kupitia vyama vya ushirika, na hapo awali kabla ya kuanza mfumo huu bei ya kakao ilikuwa ni shilingi 7,000 kwa kilo tukiuza kwenye kampuni za *botanical;* na sasa hivi mfumo huu umeingia wizi mkubwa sana ambao unaendelea mpaka sasa. Kwa sasa zao hili halimnufaishi mkulima wa Kyela mpaka Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa *comrade* Homera amekiri wazi kwamba mfumo huu unawanufaisha watu wachache na hela haionyeshi kwamba inaingia kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu una matatizo sana, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa nini Serikali inaendelea kung'ang'ania mfumo huu ambao haumnufaishi mkulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tarehe 7 mwezi wa nane, mwaka 2022 Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara alikiri wazi kwamba mfumo huu utaondoka kwenye zao hili. Je, ni lini sasa Waziri ataenda kuwaambia wananchi wa Kyela kwamba

sasa mfumo ambao utamnufaisha mkulima ni huu ambao na wao watakuwa wameujadili naye? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jambo la kwanza namuondoa hofu Mheshimiwa Mbunge, na ndiyo maana mnaona katika matumizi ya huu mfumo tunavozungumza sasa bei ya zao la kakao kwa kilo imefika shilingi 8,000 kwa hiyo unaona kuna maendeleo makubwa. Bahati nzuri katika mfumo huu mkulima analipwa ndani ya masaa 48 baada ya mnada kuwa umekamilika; kwa hiyo utaona kuna manufaa mengi kwenye huu mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara ya Kilimo kwa sababu tunaendelea kupitia hii mifumo na kuangalia kama kuna changamoto basi tunapokea sehemu ya maoni ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyatoa na tutayapitia tuone kama kuna mahali kuna changamoto ili tuweze kuirekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kueleza kwamba, ni lini mfumo huu utaondoka nafikiri baada ya mapitio ya changamoto tujue kama kweli kuna changamoto lakini jukumu letu sisi ni kuboresha na kuhakikisha mfumo huu unawasaidia wakulima nchini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alishatoa taarifa kwa Umma kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imeshatoa fedha zote kwa ajili ya kuwalipa wakulima wa zao la mahindi kule Ludewa. Je, nini maelekezo ya Serikali kwa watu wa *NFRA* kuwahisha malipo hayo ili wazazi waweze kupeleka watoto vyuo na kununua mbolea? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge ameeleza kwamba tuko katika hatua za mwisho kumalizia malipo kwa watu ambao wapo katika awamu ya mwisho. Kwa maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alikuwa amenipatia, ni kwamba baada ya kumaliza huu mchakato, Serikali itarudi kwa ajili ya kuendelea kununua mazao kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ni kwamba, kwa sababu fedha hizi ziko katika Taasisi za Kibenki, wanamalizia tu huu mchakato na naamini kabla ya mwisho wa mwezi huu wakulima wote nchini watakuwa wameshalipwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Licha ya mkakati wa Serikali kuruhusu minada ya kahawa, Mkoani Kagera, bado changamoto ya bei inabaki kuwa chini ukilinganisha za majirani zetu wa Uganda, hivyo kupelekea watu kutamani kuvusha kahawa. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha bei ya kahawa Mkoani Kagera haitofautiani sana na Uganda ili watu waweze kupata faida ya kahawa zao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Swali la namna hii nilijibu nafikiri ndani ya siku mbili au tatu zilizopita, tukaainisha moja ya mchakato wa Serikali wa kuongeza thamani katika zao la kahawa ambao utachangia ongezeko la bei kwa sababu asilimia kubwa ya kahawa ambayo tunauza sisi ni kahawa ghafi ambayo inapelekea bei kuwa chini. Nimthibitishie kwamba mkakati wetu juu ya uwekezaji katika zao la kahawa uko palepale na tutawasaidia wakulima katika maeneo yote nchini wanayolima ikiwemo katika Mkoa wa Kagera. Kwa hiyo nimwondoe shaka Mbunge katika hili, hii kazi tunaiweza na tutaifanya. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 95

**Kutoa fedha za ujenzi wa barabara ya Karatu – Sibiti**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa fedha zote za ujenzi wa barabara ya lami Karatu – Mbulu – Hydom hadi Sibiti ili ujenzi uendelee?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Kasekenya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti – Lalago mpaka Maswa yenye urefu wa kilometa 389 inatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani na kwa utaratibu wa *EPC+F*. Awamu ya kwanza: Mbulu – Garbabi (kilomita 25) Mkandarasi yupo eneo la mradi anaendelea na kazi. Eneo la Labay – Haydom (kilomita 25) Mkandarasi anakamilisha taratibu za kimkataba ili aweze kulipwa Malipo ya Awali *(Advance Payment)* ili aweze kuanza kazi. Sehemu iliyobaki ya Karatu – Mbulu na Haydom – Sibiti – Lalago – Maswa yenye urefu wa kilomita 339 itajengwa kwa utaratibu wa *EPC+F* ambapo Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 16 Juni, 2023, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa sasa barabara hii ya Mbulu – Garbabi ni kweli Mkandarasi yupo *site,* lakini ana tatizo hilo la kutolipwa fedha baada ya yeye ku-*raise certificate* ambayo iko ofisini kwa Mheshimiwa Waziri. Je, lini atalipwa hiyo fedha ili aendelee kuweka au kumalizia barabara hii ya Garbabi kwenda Mbulu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nashukuru kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwepo katika kusaini Mkataba wa Barabara ya kutoka Haydom kuja Labay. Sasa ni miezi sita, tumesaini tarehe 25 Mei, 2023. Je, ni lini sasa barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ili wananchi waweze kupita? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi ambaye anafanya kazi kati ya Mbulu na Garbabi, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba anaendelea na kazi kwa sasa. Hii ni baada ya Mkataba wake unamtaka asisimame kazi baada ya kuanza kazi. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, nimepata taarifa leo kwamba kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande alichokisema cha Labay – Haydom, ni kweli kilisainiwa. Nataka kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu unaotumika katika kipande hiki ni sanifu na jenga. Wajibu wa Mkandarasi kwanza ni kufanya usanifu wa ile Barabara. Halafu ikishasanifiwa ipate kibali kwamba iko sawasawa na Mamlaka kwa maana ya *TANROADS* ndipo anatakiwa sasa aanze kujenga hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hizo zinaendelea na akishakamilisha, basi

tutamwona *site* akiwa anaanza kuijenga hiyo barabara, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, ni lini Barabara ya Moshi – Arusha hasa kipande cha pale Moshi Mjini itapanuliwa ukilinganisha kwamba tayari Mikataba ilishasainiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli kwamba barabara hii inapanuliwa kutoka Arusha kwenda Moshi ikiwa ni pamoja ya lile Daraja la Kikafu. Hii barabara ambayo ameisema, tunasaidiana na wenzetu wa *JICA*. Ziko taratibu ambazo zikishakamilika, basi barabara hii itaanza kujengwa, lakini iko mbioni kuanza kujengwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Omurushaka kwenda mpaka Mrongo, Mkandarasi amepatikana ni zaidi ya miezi sita lakini bado Mkataba haujasainiwa. Je, ni lini Mkataba utasainiwa ili barabara hii ianze kujengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Moja ya swali ambalo alitolea ufafanuzi Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ni kwamba Barabara aliyoitaja Omurushaka kwenda Murongo, kilometa 50 ni kati ya zile barabara kuu 15 ambazo tayari tumeshaomba kama alivyosema Mheshimiwa Waziri zisainiwe zote kwa pamoja ambazo zinagharimu karibu shilingi Trilioni 2.0. Alishasema kwamba aliomba Mamlaka ziweze kusimamia hilo zoezi, kushuhudia. Kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo ni kati ya barabara

hizo ambazo zitapata kibali cha kuanza kuzijenga, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa Mwezi Juni mwaka huu tulisaini Mkataba wa Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Lalago. Je, ni lini kazi rasmi itaanza ya ujenzi wa kipande cha Karatu – Mbulu ambako kipindi hiki cha mvua wananchi wanapata matatizo makubwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha Karatu – Mbulu ni kipande ambacho kinaangukia kwenye zile barabara ambazo zinajengwa kwa Mpango wa *EPC+F*. Tayari Wakandarasi washasaini, wako *site* wakiwa pia wanafanya, tunasema usanifu wa kina kwa sababu usanifu waliopewa ni wa awali. Baada ya kukamilisha taratibu zote kama tulivyosema, barabara hizi zitaanza kujengwa kuanzia Januari, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge naona mko wengi na muda wetu sio rafiki sana. Mheshimiwa Aysharose, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha Barabara inayoanzia Njuki – Ilongero – Haydom kwa kiwango cha lami hasa ukizingatia ujenzi wake umekuwa ukisuasua. Barabara hii ina ahadi ya viongozi toka Awamu ya Nne? Napenda kupata *commitment* ya Serikali, ni lini barabara hii itakamilika kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama alivyosema ahadi za viongozi, namhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara hizi zote ambazo zimepangiwa bajeti kwa mwaka huu, yako maandalizi ambayo yanaendelea kuhakikisha kwamba tunaanza ujenzi kama tulivyopanga kwenye Bajeti ya mwaka huu 2023/2024, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Je, ni lini Serikali itajenga Barabara ya kutoka Kalela – Munzeze – Buhigwe kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Genzabuke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni barabara ya mkoa ambayo namkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba ilikuwa haijafanyiwa usanifu. Sasa hivi barabara hiyo inakamilishwa kufanya usanifu kutoka Kalela – Munzeze – Buhigwe. Baada ya hapo gharama zitajulikana, Serikali sasa itatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, sasa aulize swali lake.

Na. 96

**Ujenzi wa vibanda vya wajasiriamali pembezoni mwa barabara Kimara hadi Kiluvya**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Vibanda vya Wajasiriamali pembezoni mwa Barabara ya Njia Nane Kimara hadi Kiluvya utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS,)* imekamilisha Usanifu wa Vibanda 950 vya Wajasiliamali vitakavyojengwa pembezoni mwa Barabara ya Morogoro kuanzia Kimara hadi Kiluvya. Zabuni ziko katika hatua ya uchambuzi *(evaluation)* na ujenzi unatarajiwa kuanza Mwezi Desemba, 2023 na utekelezaji wake unakadiriwa kuchukua muda wa miezi sita, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza natumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kupitia Serikali anayoiongoza ya Awamu ya Sita kwa kuwa msikivu sana kwa kilio cha wajasiriamali, Wilaya ya Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maswali mawili ya nyongeza, swali la kwanza; kwa kuwa ni kawaida sana vinavyotengenezwa vibanda hivi vya wajasiriamali, wananchi mbalimbali kutokea kwenye maeneo mbalimbali ya nchi wanavamia na kusababisha walengwa kutofikiwa.

Je, Serikali au Wizara ya Ujenzi mko tayari kuiachia Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo kupanga wajasiriamali hao ili kufikia malengo tuliyotarajia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa mpaka sasa wajasiriamali wanateswa sana kupitia Wizara ya Ujenzi katika eneo lao la *TANROADS* katika maeneo haya waliyopo.

Je, Serikali ipo tayari kuchukua ombi la kuwaacha kipindi hiki wajasiriamali mpaka mradi utakapokamilika katika maeneo haya ya pembezoni mwa barabara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Serikali nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua kazi nzuri anayofanya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nasema tu kwamba, kwa kuwa tunaowalenga ni wajasiriamali wa eneo husika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatafuta mpango mzuri ambao utahakikisha kwamba wale walengwa ndiyo wanaopata vibanda hivi. Ofisi ya Mheshimiwa Mbunge mhusika tutahakikisha kwamba inashiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, naomba tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kikubwa ambacho hapa tunaangalia ni kulinda usalama wa hawa wanaofanya biashara. Tunaweza tukawaacha wakaendelea kufanya biashara, lakini kukatokea madhara. Hata hivyo, nasema tu tumelipokea, tutatafuta namna nzuri ya kuona namna gani wanaweza wakafanya biashara bila madhara. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Jimbo la Kawe kama ilivyo Jimbo la Kibamba, lina wajasiriamali wengi sana barabarani. Kwa kuwa tuna barabara yetu kubwa kutoka Mwenge – Bagamoyo, kwa nini mpango huo mzuri wanaofanya Kibamba wasiulete pia Jimbo la Kawe ili wajasiriamali waweze kupangwa vizuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja tu ni kwamba, eneo hili la barabara hata wakati wa *design* yaani wakati inafanyiwa usanifu, hivi vibanda vinavyojengwa vilikuwa tayari viko kwenye usanifu. Sasa, itategemea na barabara kutoka Mwenge – Tegeta – Bagamoyo kama itakuwa ina *design* na eneo ambalo unaweza ukaweka vibanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tulichukue hilo kwamba katika barabara nyingi zinazodizainiwa mjini basi ni vyema suala hili la kuweka vibanda liwe limefanyiwa usanifu. Lisipofanyiwa usanifu halitawezekana kufanyika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Namwona Waziri wa Ujenzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Katika kuongeza jibu alilojibu Mheshimiwa Waziri, nampongeza sana Mheshimiwa Gwajima, Mbunge wa Jimbo la Kawe, kwa namna ambavyo anapambana. Hapa kabla ya swali, amekuja kuniona kuhusu changamoto ya mafuriko ambayo ipo Barabara ya Mwenge kwenda Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemuahidi Serikali kupitia Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, tutakaa na kujipanga ili tuweze kwenda *site* na kuona cha kufanya ili kuwatoa wananchi kwenye adha ambayo Mheshimiwa Gwajima ameitaja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Gwajima una swali la nyongeza?

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Waziri, nakumbuka tulisaini Mkataba wa Barabara ya Mwendokasi inayoanzia Mwenge – Tegeta – Basihaya. Je, ni lini barabara hiyo ambayo Mkataba wake tumeshasaini itaanza kujengwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba tu kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wabunge naomba tuongee kwa sauti ya chini ili tusikie majibu ya Serikali. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri siku ya kusaini hiyo barabara mimi mwenyewe nilishiriki. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua iliyopo sasa hivi iko kwenye zile hatua za awali, yaani *mobilization* kwa ajili ya kuanza kuijenga hiyo barabara. Wakandarasi tayari wako wanafanya *mobilization* kwa ajili ya kujenga, yaani maandalizi ya awali kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Cosato Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kama ambavyo ilivyo Kawe, Barabara ya Mafinga – Mgololo ambayo tulisaini Tarehe 26 mwezi Juni. Wananchi wananiuliza na juzi nilikuwa pale Kanisani pale Bwawani kwa Mzee Mahimbi, Wachungaji wakanivuta pembeni wakasema hii barabara inaanza lini? Ninayo majibu lakini wananchi wangetamani kusikia majibu ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mafinga – Mgololo ina urefu wa kilometa 81 na ni kati ya zile barabara ambazo zinatekelezwa kwa Mpango wa *EPC+F*. Hii barabara ndiyo ambayo ni ya kiuchumi ambayo karibu sehemu kubwa ya magogo na mbao zinapita kwenye hii barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia kama nilivyosema kwenye swali la msingi la Mheshimiwa Flatei, tayari wakandarasi wako *site* wanafanya usanifu wao wa kina na tunategemea kuanzia Januari watakuwa wameanza kazi hiyo. Kwa sasa wako wanaandaa maeneo ya kuchukua *materials*, maeneo ya kujenga hizo *site* zao na kama kutakuwa na uwezekano wa kuigawa hiyo barabara mara mbili ili waweze kuifanya hiyo kazi kwa uharaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, mradi huo upo na tayari wakandarasi wapo *site* japo hawajaanza ile *earth work,* yaani kazi ya kuanza kuchimba Barabara, lakini wako wanafanya maandalizi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 97

**Kupunguza msongamano wa malori barabarani**

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kupunguza msongamano wa malori barabarani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya Serikali na jitihada za kupunguza msongamano wa magari ikiwemo malori barabarani ni pamoja na kujenga Madaraja na Barabara za juu kwenye majiji makubwa nchini, kufanya upanuzi wa barabara kutoka njia mbili kwenda njia nne hadi nane kwa maeneo yenye msongamano mkubwa, ujenzi wa maegesho ya malori, ufungaji wa mifumo ya

kielektroniki ya kupima uzito wa malori yakiwa kwenye mwendo *(Weigh in Motion System – WIMS)* katika vituo vya mizani na barabara za michepuo katika miji na majiji mbalimbali, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa sasa hivi.

Je, Serikali inasema nini katika kufuatilia utendaji katika mizani ili kupunguza msongamano wa malori barabarani?

Swali la pili, nini mkakati wa muda mrefu wa upanuzi wa barabara kiwango cha njia, hasa barabara kuu ziingiazo nchini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, kwamba moja ya maeneo ambayo yameonekana yanakuwa na msongamano mkubwa ni kwenye mizani. Utaratibu ambao sasa tumeanza kuufanya, kwanza ni kubadilisha mizani ile ambayo ilikuwa siyo ya kieletroniki ambayo inatakiwa gari lisimame ndiyo lipime. Sasa tunatumia mizani ambayo tunasema *weigh in motion* yaani gari linakuwa linatembea huku linapima, kwa hiyo litumia muda mfupi sana, ikiwa ni pamoja na kuweka mizani pande zote mbili. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo kwenye mizani hiyo kumepunguza sana changamoto ya msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa kuzipanua barabara kwenye mipaka yetu ama njia zinazoingia nchini, ziko barabara hasa kwenye vituo vyetu vya forodha vikubwa kama

Tunduma, ambako sasa hivi tunafikiria namna ya kuongeza njia kutoka njia mbili kwenda njia nne ili kupunguza msongamano katika maeneo hayo. Ndiyo maana katika mradi wa sasa ambao unakwenda kwa mfano mpaka wa Tunduma, barabara inayojengwa ni ya njia nne. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Mwanyika swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini barabara ya mchepuo katika Mji wa Njombe kutoka Kibena kwenda mpaka maeneo ya Kobe itaanza kujengwa kuondoa adha ya malori?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sasa hivi kilichofanyika katika Mji wa Njombe ambao Mji unakua kwa kasi sana, wameshafanya usanifu wa awali kabisa *(reconnaissance survey)* ili kuona namna wapi barabara ya mchepuko itapita katika Mji wa Njombe. Kwa hiyo mipango hiyo ipo kinachofatia sasa hivi ni kutafuta fedha kukamilisha huo usanifu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shally Raymond swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kuniona. Niipongeze Serikali kwa kutenganisha Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi.

Kwa kuwa, vyombo vya usafiri barabarani vimeongezeka, ukianzia baiskeli, bajaji, bodaboda, magari madogo mpaka malori lakini barabara hizo zimebakia ni zile zile mbili. Nikifatilia majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri amezitaja zote kwamba zitapanuliwa lakini mimi nauliza kabisa, ni lini haswa Barabara ya kutoka Dar es Salaam mpaka Arusha - Namanga na

inayokwenda mpaka *Cape Town* itapanuliwa ili basi ianzie hapo tuende ile ya Dar - Mbeya, Dar - Lindi, Dar – Mwanza, Dodoma - Arusha?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa swali la nyongeza ni moja, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakiri kwamba barabara nyingi ambazo tulijenga zamani, zilijengwa kulingana na mahitaji ya wakati huo na lazima tukiri kwamba tunapoona magari mengi yameongezeka maana yake uchumi wetu, umezidi kukua na ndiyo maana tunaona magari makubwa na malori makubwa. Kwa hiyo, sasa hivi tunachofanya hizi barabara zote tunapotakiwa kuzipanua ni kwamba ni lazima tufanye usanifu upya, halafu tuzijenge kwa kiwango cha sasa. Kwa hiyo Serikali imeliona hilo ikiwa ni pamoja na barabara hiyo ya kutoka Chalinze kwenda Mombo hadi Moshi. Kwa hiyo, tayari zimeainishwa, kinachotegemewa sasa ni kutafuta fedha ili kuanza kuzitengeneza hizo barabara mpya kwa kiwango cha sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata sasa barabara tunazozijenga upana wake ni tofauti kabisa na upana wa barabara zile zilizojengwa zamani ikiwepo barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge., Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Josephat Kandege swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa, msongamano uliopo Mji wa Tunduma ni mkubwa sana na katika hali ya kawaida upanuzi wake utakuwa gharama kubwa sana, bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri alipita akaona uwezekano wa kujenga barabara kiwango cha lami kuanzia Laela kwenda kuunganisha ile barabara kwenda Kasesha.

Je, nini mpango wa Serikali katika kuondoa msongamano huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tu niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba pamoja na mchango wa barabara kuleta msongamano Tunduma lakini kuna mambo mengine ambayo ni ya kiforodha ambayo yanasababisha msongamano katika Mji wa Tunduma ikiwa ni pamoja na wenzetu wa upande wa pili ambao hawaendani na kasi ya kwetu. Sisi tunafanya masaa 24 wao wanafanya masaa 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kumjibu Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba tunafikiria kama Serikali kwanza kutengeneza *bypass* kutoka Mpemba kwenda kuunganisha na barabara inayokwenda Sumbawanga ili magari ambayo yanaenda njia ya Sumbawanga yasilazimike kupita Tunduma, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kweli nimepita kwenye barabara aliyoisema ambayo kama tutaijenga kwa kiwango cha lami itasaidia sana magari mengi kwenda Bandari ya Kasanga ikiwa ni pamoja na mpaka wa Kasesya. Kwa hiyo, hiyo mipango ipo kinachosubiriwa tu ni Serikali itakapopata fedha kuijenga hiyo Barabara. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa unatoka Kibaha unaenda Dar es Salaam kwenye njia nane, kuna Maliasili Idara ya Misitu wanakagua malighafi za misitu kwenye hiyo njia nane barabarani kabisa, kitu ambacho kinasababisha msongamano na ajali.

Ni kwa nini Serikali isiweke mchepuko kama wanavyofanya kwenye mizani waweze kuwajengea wakifika pale wanachepuka, wanakaguliwa, wanaingia kwenye *highway* wanaendelea, kuliko kukaguliwa kwenye *high way*?

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza ni moja Mheshimiwa Esther, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nilichukue suala hilo kwa ajili ya kulifanyia *study* na kuona uwezekano wa hicho alichokisema Mheshimiwa Esther Matiko Mbunge. Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eric Shigongo swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Hivi karibuni tulisaini mkataba wa Barabara ya Sengerema - Nyehunge kwa kiwango cha lami na Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwepo lakini imekuwa kimya. Je, tunaweza kufahamu tatizo hasa ni nini mpaka muda huu kazi hiyo haijaanza?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge Eric Shigongo, kwamba tulisaini mkataba lakini maendeleo ni madogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari Mkandarasi huyo ameshaitwa na Wizara na Mheshimiwa Waziri kujua changamoto yake ni nini ili tuone taratibu za kuchukua za kimkataba kama itaonekana kwamba huyo Mkandarasi ana changamoto ili taratibu za kimkataba ziweze kuchukuliwa, ili tuone kwamba hii kazi nzuri anayoifanya Daktari Samia isikwamishwe na huyu Mkandarasi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshaliona na hatua tayari tumeshaanza kuchukua. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri sana kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 98

**Kurudisha masomo ya ziada ya kazi za mikono mashuleni**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itarudisha masomo ya kazi za mikono kama useremala, mapishi, kushona, kilimo, ujenzi kwa shule za Msingi na Sekondari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Kipanga majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha taratibu za kufanya mapitio na kuboresha mitaala ya ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu. Katika maboresho hayo, fani za ufundi zaidi ya 55 zikiwemo useremala, mapishi, kushona, kilimo na ujenzi zimejumuishwa katika mitaala mipya. Hivyo, wanafunzi watapata fursa ya kujifunza kazi za mikono kupitia chaguzi za mikondo ya masomo kwa kadri ya amali watakazozipenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo haya katika ngazi ya Sekondari yatatolewa kwa kutumia mtaala wa *VETA* na yatatahiniwa na *NACTVET* kwa lengo la kuwezesha wahitimu kupata vyeti vitakavyotambulika katika soko la ajira,. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Najma swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nitumie fursa hii kuipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Elimu, kwa kuendelea kuboresha sekta ya elimu nchini, hususan katika masuala ya kazi ya masomo ya kazi za mikono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la nyongeza ni moja tu. Kwa vile Baraza la Taifa la Mitihani pamoja na Elimu ya Juu ni masuala ya Muungano au ni mambo ya Muungano, na kwa madhumini ya kuwajengea msingi wa aina moja, vijana wetu wote wa Kitanzania. Je, Serikali ya Muungano kupitia Wizara ya Elimu inashirikiana vipi na Wizara ya Elimu Zanzibar ili kuhakikisha kwamba misingi yao ya elimu inakuwa ya aina moja na waweze kufanya mitihani ya aina moja? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Giga Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba wakati wa uandaaji wa mitaala hii, uratibu ulifanyika kwa kutumia taasisi zetu zote mbili ile Taasisi ya Elimu Zanzibar pamoja na Taasisi ya Elimu ya Tanzania Bara. Vilevile Wajumbe wa Kamati waliohusika katika marekebisho ya mitaala hii walitoka katika pande zote mbili za Muungano, kwa maana ya Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile maoni juu ya mtaala huu yalipokelewa katika pande zote mbili za Muungano. Tulifanya makongamano pamoja na mikutano kule Zanzibar, vilevile tulifanya makongamano na mikutano mbalimbali huku Tanzania Bara. Kwa hiyo, nimuondoe wasiwasi hili limezingatiwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tuliweza kuwasilisha rasimu hii ya mitaala kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar pamoja na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kabla ya mitaala hii haijaenda kwenye ithibati nyingine. Nimwondoe

wasiwasi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tutaendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania Bara katika kuhakikisha kwamba mitaala hii inatekelezwa na wenzetu vilevile wa Zanzibar nao vilevile wafanye mapitio ya mitaala yao, ndiyo itakayokwenda kutekelezwa na tutakuwa sasa tunakwenda pamoja. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu kwa majibu ya maswali hayo. Tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa Daktari David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 99

**Tatizo la Mawasiliano ya Simu Kata ya Same**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Je, lini Kata za Ruvu, Msindo, Mshewa, Vudee, Mhezi, Tae na Suji - Same zitapelekewa mawasiliano ya simu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa Mhandisi Andrew Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Jimbo la Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeainisha Kata Sita kati ya Kata Saba za Jimbo la Same Magharibi zenye changamoto kubwa ya upatikanaji wa huduma za Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Vudee, Suji na Ruvu zitafikishiwa huduma ya mawasiliano kwa kupitia Kampuni ya *Horora PLC (TiGo)*, wakati Kata ya Mshewa itafikishiwa huduma za

mawasiliano kupitia kampuni ya simu ya Airtel. Kata ya Msindo itafikishiwa huduma za mawasiliano na kampuni ya simu ya *TTCL* na Kata ya Mhezi itafikishiwa huduma ya mawasiliano ya simu kupitia kampuni ya simu ya Halotel.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kata ya Tae, *USCAF* itaifanyia tathmini Kata hiyo ili kubaini mahitaji halisi ya huduma za mawasiliano na hatimae kuiweka katika mpango wa zabuni zijazo zitakazotekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Dokta David Mathayo swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, jana Tarehe 06 Novemba, 2023 kulikuwa na tatizo kubwa la mtandao wa Vodacom. Shughuli nyingi za kutuma fedha zilikwama, mambo mengi yalikwama kabisa, mawasiliano hata kutuma miamala ya fedha kwenye benki na kwenye simu.

Je, Vodacom jana ilipatwa na changamoto gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Kata hizi ambazo Mheshimiwa Waziri amezitaja zimefikia hatua gani, katika utekelezaji wake, maana wameshazipitia tayari, zimefikia hatua gani ili wananchi wa Kata hizi za Ruvu, Msindo, Mshewa, Vudee, Mhezi na Suji waweze kupata mitandao ya simu?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na kipengele cha kwanza ni kweli kabisa, jana kumekuwa na changamoto kupitia mtandao wa Vodacom, tunasema kwamba kulikuwa na *technical hiccups. Technical hiccups* maana yake kwamba, ilitokea katika *network service* ambapo iliathiri masuala ya kupiga, *sms*, pamoja na kutuma pesa kwa mtandao wa M-Pesa, lakini wenzetu wametoa taarifa wanaendelea kuifanyia kazi na leo tumeona kuna *improvement,* pia wateja ambao waliathirika ni Watanzania milioni 1.8. Kwa hiyo, tunaamini kwamba wanaendelea kulifanyia kazi na baadae watatupatia mrejesho wa hatua ambayo wameifikia na tunaamini kwamba hili tatizo litakuwa limeisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kata za Ruvu, Msindo, Mshewa, Vudee, Mhezi pamoja na Suji ukiachilia hili suala la Kata ya Tae ambayo tutaiingiza katika mpango wa utekelezaji wa minara mingine inayokuja, hizi Kata ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kwanza naomba uniruhusu nitoe ufafanuzi kidogo hapa. Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla tumekuwa na maswali mengi sana kuhusiana na minara hii 758, tulichokifanya pale mwanzoni ni kubainisha Kata ambazo zina changamoto ya mawasiliano, lakini hatukubainisha maeneo ya kwenda kujenga minara hii. Kwa hiyo, tunachokifaya ni kuhakiksha kwamba tunaenda kubainisha maeneo sasa ambapo tunaenda kujenga minara na baada ya kufanya hivyo tunaenda kuhakikisha kwamba sasa tunaomba vibali. Wakati haya yote yanaendelea labda nikupe takwimu kidogo kwamba, mpaka sasa Airtel kati ya maeneo 188 mpaka sasa ameshaainisha maeneo 140 ambayo ni zaidi ya asilimia 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *TTCL* yeye ameshamaliza maeneo yote pia ameshaingia mikataba na wahusika wa maeneo. Tigo kati ya maeneo 137 tayari maeneo 133 yameshakamilika. Halotel maeneo 22 yote ameshakamilisha kulingana na mkataba wake lakini *Vodacom* maeneo 133 kati ya 137. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba kuna hatua ambazo Waheshimiwa Wabunge hawatoziona kule zinatokea katika Majimbo yao ni kwa sababu kuna hatua ambazo ni za kiufundi na ni lazima tuzifuate na ni lazima zikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tunahitaji minara hii ijengwe kwa kasi, lakini ni lazima tuhakikishe kwamba, tunafuata utaratibu ambao hautakuja kuingiza Taifa katika janga la minara ambayo itajengwa halafu idondoke. Kwa hiyo ni lazima haya yafanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie kwamba, kampuni zote mpaka sasa zimeshaandika kuomba vibali na wakati wanaandika kuomba vibali bado wameagiza vifaa kwa ajili ya ujenzi. Kwa hiyo, kuna hatua mbalimbali ambazo zinaendelea kufanyika kuhakikisha kwamba minara hii itakapokuja kuanza kusimamishwa, nakuhakikishia kwamba inaweza ikasimama kwa pamoja na Watanzania, Waheshimiwa Wabunge, wote tutashangilia kazi kubwa ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana lakini kwa ndugu yangu wa Same, bahati nzuri yeye yuko katika minara ya Halotel ambapo wao kazi kubwa imeshafanyika, Halotel wameshaanza kujenga minara mitano. Katika minara hiyo mitano kuna mmoja ambao unajengwa katika Kata ya Mheshimiwa David Mathayo David. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, naona mpo wengi na kwa maelezo haya nadhani maswali yote ya nyongeza yote yameshajibiwa. Kwa hiyo naomba tuendelee. Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, sasa aulize swali lake.

Na. 100

**Hitaji la mawasiliano ya simu Kata ya Masaka – Kalenga**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka huduma ya mawasiliano ya simu Kata ya Masaka – Kalenga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* iliingiza Kata ya Masaka katika zabuni ya kufika huduma ya mawasiliano Vijijini kupitia Mradi wa Tanzania ya Kiditali, ambapo Kampuni ya Simu ya *Vodacom* ilishinda zabuni hiyo ya kufikisha huduma hiyo katika Kata ya Masaka yenye Vijiji vya Kaning'ombe, Saadani pamoja na Makota. Mpaka sasa *Vodacom* inaendelea na hatua mbalimbali za utekelezaji katika ujenzi wa mnara huo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru sana Serikali kwa kuwahakikishia wananchi wa Masaka kwamba sasa unapeleka mawasiliano. Pamoja na majibu mazuri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Jimbo la Kalenga lilipewa minara kumi: Je, hizo Kata nyingine za Kihanga pamoja na Ulanda nazo zitajengwa kwa pamoja? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jackson, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimetoa ufafanuzi, miradi yote ambayo imeshaainishwa katika Mradi wa Tanzania ya Kidigitali upo katika hatua ambazo nimemaliza kuzielezea na tuwe na subira Waheshimiwa Wabunge. Naamini kabisa kwamba, hatua zote ambazo ni za ndani zikishakamilika, sasa tukishahamia *site* na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kusimamisha ile *passive structure* haimalizi hata wiki tatu na ukija kuhakikisha kwamba unafunga zile *active equipment* haimalizi hata wiki moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukishamaliza *process* za ndani hizi, tukahamia *site* nina uhakika ndani ya mwezi mmoja au miwili minara hiyo itakuwa inakamilika katika kila eneo ambalo tutakuwa tunapeleka huduma ya mawasiliano, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kingu, swali la nyongeza.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Nilikuwa nataka niulize swali la nyongeza. Ni lini Serikali itakwenda kutatua changamoto ya upatikanaji wa mawasiliano kwa wananchi wa Kata ya Igombwe pamoja na Ihanja ambapo kuna minara inasuasua sana ikizingatiwa kwamba Kata ya Igombwe ndiyo Kata inayochangia kwa kiwango kikubwa pato la Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Elibariki Kingu, Mbunge kuhusiana na changamoto ya Kata ya Igombwe pamoja na Ihanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu minara tayari imejengwa, ipo. Changamoto ni kwamba Mheshimiwa Mbunge, amesema inasuasua. Tutawaelekeza *TCRA* kwa sababu kwa mujibu wa sheria, wao wana dhamana ya kuhakikisha kwamba watoa huduma wote wanazingatia *quality of service*. Kwa hiyo, tutahakikisha tunawatuma watalamu wetu wakajiridhishe, tatizo liko wapi? Kama mnara umezidiwa, basi tujue kwamba tunaongeza nguvu na kama mnara una changamoto ya kiufundi, basi wachukue hatua kuhakikisha kwamba wananchi wa Igombwe na Ihanja ambao ni wananchi wa Mheshimiwa Kingu na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wanapata huduma ya mawasiliano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa hii nafasi. Kwa kuwa Naibu Waziri amesema upembuzi yakinifu wa ujenzi wa minara umeshafanyika na katika Kata ya Iseke tayari walishafika: Je, ni lini sasa ujenzi wa mnara wa mawasiliano utaanza katika Kata ya Iseke? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi, kwa sababu ulishatoa maelezo ya awali.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Dkt. Chaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Iseke kama ambavyo nimejibu katika majibu mengine ni kwamba, vifaa vikishaingia nchini na hatua za kiufundi na za kiutaratibu na za kisheria zikishakamilika, tutahakikisha kwamba Kata ya Iseke tunaanza ujenzi mara moja na kuhakikisha kwamba Wananchi wa maeneo hayo wanaendelea kufurahia matunda ya nchi yao, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kata ya Mlowo ni Kata ambayo iko katikati ya Mji ndani ya Wilaya Mbozi, lakini kuna baadhi ya maeneo kumekuwa na changamoto kubwa ya mawaliano ikiwepo eneo la Saganoti na maeneo mengine ya *Forest*. Serikali ina mkakati gani wa kurekebisha mawasiliano katika maeneo haya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stella, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti ni dhamira ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kupitia utekelekezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma ya mawasiliano. Kwa sababu hiyo, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha

kwamba tunajiridhisha kila sehemu ambayo ina changamoto ya mawasiliano, basi tunafika na kuchukua hatua stahiki ili Watanzania wote waweze kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Stella, baada ya Bunge hili tuweze kuwasiliana ili tuweze kuchukua taarifa kamili kuhusiana na maeneo husika ili sasa tutume watalamu wetu wakajiridhishe ni nini kikafanyike katika eneo hilo ili kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto ya mawasiliano, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano katika Kata ya Masisiwe katika Wilaya ya Kilolo? Kwa sababu wananchi wamekuwa wakipata mateso makubwa sana, hawana mawasiliano kwa muda mrefu sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Iringa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyeki, hii Kata ya Masisiwe Mheshimiwa Mbunge alishaiongea zaidi ya mara tatu mwaka 2022. Baada ya kuongea, tukaiingiza kwenye utekelezaji wa mradi wa Tanzania ya Kidigitali na sasa tunasubiri katika hatua mbalimbali za utekelezaji zikishakamilika Kata ya Masisiwe itapata mawasiliano, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jonas Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Kikolo

katika Jimbo la Mbinga Mjini ina changamoto kubwa sana ya mawasiliano: Ni lini Serikali itapeleka huduma hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilipokee na nilichukue kama changamoto ambayo tutaenda kuifanyia kazi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu mengi ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na maelezo yako yale mazuri. Tunashukuru sana.

Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, sasa aulize swali lake.

Na.101

**Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo Tarafa za Morogoro Vijijini**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Mahakama za Mwanzo katika Tarafa za Bwakira, Mvuli na Matombo – Morogoro Vijijini?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Katika na Sheria, Mheshimiwa Pauline Gekul, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu sasa swali la Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango na Bajeti ya mwaka 2023/2024, Mahakama ya Mwanzo katika Tarafa ya

Bwakira, Kata ya Bwakira Chini itajengwa ili kuwawezesha wananchi katika maeneo hayo kupata haki kwa wakati. Tayari zabuni imetangazwa kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mahakama za Mwanzo; Matombo na Mvuha, majengo yaliyopo ni chakavu sana na hivyo kuhitaji ujenzi mpya. Hata hivyo, kutokana na mahitaji makubwa yaliyopo katika maeneo mbalimbali, ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Matombo na Mvuha utazingatiwa kwenye Mpango ujao wa ujenzi wa Mahakama, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Innocent, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali na hasa, sasa tunakwenda kujenga Mahakama katika Tarafa ya Bwakira Kata ya Bwakira Chini. Naipongeza Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tarafa ya Bwakira Chini kuna hakimu ambaye anaitwa Deogratius Amatungiro, ni Hakimu ambaye amegeuza Mahakama kama duka la kuuza haki kwa wananchi kiasi ambacho wananchi wa Tarafa ya Bwakira Chini wamemchoka: Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari kwenda nami katika Kata ya Bwakira Chini, Kata ya Kisaki na Kata ya Mngazi ambayo ndiyo Tarafa ya Bwakira, ukasikilize malalamiko ya wananchi? Kwa sababu viongozi mbalimbali wamepita lakini hakuna hatua yeyote ambayo imechukuliwa ili yeye kama msimamizi au ndiyo msimamizi katika Mahakama na Wizara ya Sheria uondoke naye huyo hakimu kwa sababu tumemchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini tunatarajia kwamba hiyo Mahakama ya Bwakira Chini itaanza kujengwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, naomba sasa nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Innocent, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ameuliza ni lini Mahakama hii katika Kata ya Bwakara Chini itajengwa? Nilijibu katika majibu yangu ya msingi kwamba mwaka huu wa fedha mhimili wetu wa Mahakama imetenga kujenga Mahakama za Mwanzo zaidi ya 60 na tuna zaidi ya shilingi bilioni 88 ambazo Bunge hili wametupitititishia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Innocent Mahakama hii tunajenga mwaka huu na ndiyo maana nimesema Mkandarasi sasa anatafutwa ili kazi hii ianze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza, amemlalamikia Mheshimiwa Hakimu katika Mahakama hii ya Bwakira ambayo tunakwenda kujenga, japo inaendelea katika eneo la godauni. Naomba nimwelekeze Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wenzangu kwamba tuna Kamati zetu za Maadili kwa Maafisa wa Mahakama na Wenyeviti wa Kamati hizi ni Ma-*DC* wetu katika Wilaya zetu lakini na Waheshimiwa Ma-*RC*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Innocent kwa kuwa kanuni zetu zinatuhitaji, kama kuna malalamiko yoyote kwa Maafisa wetu wa Mahakama, tunapaswa kuandika kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge aandike kwa maandishi ampelekee Mheshimiwa *DC* wa Morogoro ili Kamati ya Maadili ya Maafisa wa Mahakama katika Wilaya yake sasa waanze uchunguzi, na kama kuna tuhuma zitakuwa zimethibitika, basi hatua zitachukuliwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, sasa aulize swali lake.

Na. 102

**Kumega Hifadhi ya Kisiwa cha Maisome**

**MHE. ERIC J. SHIGONGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawamegea eneo Wananchi wa Visiwa vya Maisome katika Hifadhi ya Kisiwa cha Maisome?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Luka Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mhehimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mhehimiwa Mwenyekiti, katika kutatua changamoto ya mwingiliano wa shughuli za uhifadhi na zile za kibinadamu, Serikali iliwasilisha taarifa ya umuhimu wa kumega hifadhi hiyo kama sehemu ya utatuzi wa migogoro ya Vijiji 975. Katika maelekezo ya Baraza la Mawaziri; Baraza liliridhia hifadhi imegwe na vijiji kupatiwa maeneo ya kuendeshea shughuli zao kwa uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshachukua hatua katika kutekeleza maelekezo ya Baraza la Mawaziri kwa kufanya mapitio ya mpaka wa msitu wa Hifadhi ya Maisome ambapo hekta 2,943.8 zimetolewa kwa wananchi na eneo hilo na kubakiwa na hekta 9,319.2. Kwa sasa taratibu za kubadili mpaka kisheria na kupata ramani mpya zinaendelea. Mara zoezi hilo litakapokamilika, Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi watajulishwa ambapo watakuwa na muda wa siku 90 kutoa maoni yao kabla ya tangazo rasmi la kutangaza eneo jipya la hifadhi baada ya mabadiliko niliyoyasema hapo juu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eric Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemwelewa vizuri sana Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kwamba Serikali imekubali kutoa hekta 2943.8 kwa wananchi wa Kisiwa cha Maisome. Kwa niaba ya wananchi hao naomba niwasilishe furaha yao kwa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa Bunge lako Tukufu kwani kwa muda mrefu wameishi kwa mateso sana wakiwa hawana eneo la malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu ni moja tu ni lini? Ni lini? Ni lini, kwa mara tatu mchakato huu wa kuweka mpaka utatekelezwa ili wananchi waifurahie Serikali yao? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria, zoezi hili linapaswa kuchukua miezi sita. Siku 90 za kuweka mipaka, kutengeneza ramani na vilevile siku 90 ambayo ndiyo itahusisha lile tangazo nililolisema. Tumefika hatua nzuri, naomba Mheshimiwa Mbunge atupe muda, tunalikamilisha muda siyo mrefu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mohamed Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni Septemba niliuliza swali Na. 76 juu ya wananchi ambao wamevamia Msitu wa Bono uliopo Kijiji cha Mswaki kwenye Kata ya Msanja na Serikali ilisema itawaondoa itakapofika Desemba 30, kwa maana ya mwaka 2022. Nataka kujua: Ni nani ambaye anazuia kuondoa wananchi wale ambao wanafanya uharibifu mkubwa na msitu huo tunaoutegemea kwa ajili ya mvua? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali inasimamia maazimio yake yale kwamba wananchi wale wataondolewa kwenye msitu ule. Naomba Mheshimiwa Mbunge, atupe fursa tulifanyie kazi ili tutekeleze kusudio letu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, sasa aulize swali lake.

Na. 103

**Kutenganisha malipo ya majengo kwa nyumba yenye zaidi ya mita moja ya umeme**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kutenganisha malipo ya majengo kwa nyumba yenye zaidi ya mita moja ya umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha ukusanyaji wa mapato kupitia mfumo wa luku kwa nyumba ambayo ina mita zaidi ya moja kwa kuhakikisha inalipiwa mita moja pekee. Aidha, pale inapobainika majengo mawili au zaidi kutumia mita moja tumekuwa tukifanya maboresho ya utozaji kwa kutoza kiasi kinachopaswa kutozwa kwa kila jengo kwa mita iliyopo. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha msingi wa utozaji wa kodi ya majengo unazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kutokana na malalamiko ya majengo machache kujitokeza kwa uchache katika kusajili na kutoa taarifa sahihi za majengo yao, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* iliendelea na zoezi la uhakiki kwa kutumia vyanzo kutoka Mamlaka mbalimbali za Serikali. Aidha, *TRA* inaendelea na maboresho ya taarifa za wamiliki wa majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie Bunge lako Tukufu kwa kuwataka wamiliki wote wa majengo ambao watakuwa na changamoto za ulipaji kodi ya majengo kupitia ununuzi wa umeme ikiwa ni pamoja na uwepo wa mita zaidi ya moja katika

jengo moja, kufika katika Ofisi za Malamka ya Mapato Tanzania iliyokaribu nao kwa ajili ya kufanya maboresho ya taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimeridhika na majibu ya Serikali, lakini mngeweka msisitizo pale kwenye msingi wa jibu la mwisho kwamba, maboresho ni muhimu sana kwa sababu tunafahamu Watanzania wengi wanaishi kwenye nyumba za kupanga na wenye nyumba wameamua kutenga mita kwa kila nyumba ambayo mtumishi yupo na nyumba inakutwa ni moja, hivyo tunajikuta nyumba moja inalipa kodi zaidi ya mara tatu jambo ambalo siyo zuri sana. Kwa hiyo, nadhani msisitizo uwekwe pale kuhakikisha kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania ihakikishe kwamba, kwenye kila nyumba ya namna hiyo kuwe na mita moja peke yake ambayo itakuwa inalipiwa jengo na nyingine zibaki kama huduma kwa wapangaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri nadhani ameridhika na jibu, tunakushukuru sana kwa majibu. Tunaendelea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 104

**Usajili wa Taasisi na Madhehebu ya Dini**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** aliuliza:-

Je, maombi mangapi ya usajili wa Taasisi na Madhehebu ya Dini yamewasilishwa tangu 2016 na hazijapatiwa usajili na sababu za kutosajiliwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi Septemba, 2023, jumla ya maombi ya Usajili wa Taasisi na Madhehebu ya Dini 1,858 yalipokelewa katika Ofisi ya Msajili wa Jumuiya. Kati ya maombi yaliyopokelewa, Taasisi na Madhehebu ya Dini 419 yamesajiliwa, maombi manne yamekataliwa na maombi 1,435 yapo katika hatua mbalimbali za usajili. Sababu zinazosababisha baadhi ya Taasisi na Madhehebu ya Dini kuchukua muda mrefu kusajiliwa au kotosajiliwa ni pamoja na baadhi ya Taasisi na Madhehebu ya Dini kukosa vigezo vya kusajiliwa, kubadili anwani za Posta au Makao Makuu ya Taasisi bila kutoa taarifa na hivyo kukosekana kwa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, baadhi ya Taasisi na Madhehebu kukosa maeneo stahiki ya kuendeshea shughuli zao na kuingia katika migogoro ya ndani, migogoro na jamii inayozunguka taasisi hizo au Mamlaka za Serikali zilizopo katika maeneo hayo au kukabiliwa na kesi katika mamlaka za utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya, inaendelea kushughulikia maombi ya Usajili wa Taasisi na Madhehebu ya Dini na kutoa usajili kwa wakati kwa taasisi zenye sifa stahiki na kuhakikisha kuwa Serikali haisajili taasisi na Madhehebu ya Dini ambayo yanaweza kuleta madhara kwa jamii au kuhamasisha vitendo ambavyo ni kinyume cha mila, desturi, utamaduni na maadili ya Kitanzania, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabani Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia takwimu zilizotolewana Serikali, kati ya maombi 1,858 ni maombi 423 tu ndiyo yaliyoshughulikiwa. Maombi manne yamekataliwa, 419 yamekubaliwa. Hii ni sawa na 22.7% kwa

kipindi cha miaka saba kutoka 2016 mpaka 2023. Je, Serikali haioni kwamba inachukua muda mrefu kutoa uamuzi? Ingekuwa ni vyema wakachukua muda mfupi kusema wamekubaliwa au wamekataliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, je, hamjui kwamba zipo athari zinazotokana na kuchelewa kufanya maamuzi haya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, baadhi ya maombi yamechukua muda mrefu lakini kama nilivyoeleza katika jibu la msingi. Sababu nyingine za kuchelewesha zinatokana na waombaji wenyewe kama nilivyoeleza, kutokidhi vigezo, kutoa muda wa matazamio lakini tunataka tujiridhishe pasipo mashaka kwamba, taasisi za jumuiya tunayoisajili haiwezi kuleta athari katika jamii ya watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwepo wa athari tunatambua uwepo wake. kwa mfano, taasisi itashindwa kufungua akaunti benki, taasisi inaweza ikashindwa kumiliki ardhi na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, tunaomba pale ambapo wanatafuta harakati za kusajiliwa wafuatae vile vigezo wanavyopewa na wataalam ili isichukue muda mrefu, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya swali la Mheshimiwa Mbunge. Twende Wizara ya Maji, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba sasa aulize swali lake.

Na. 105

**Ukarabati wa Mradi wa Maji wa Makonde**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na mrefu wa kukarabati Mradi wa Maji wa Makonde Mkoani Mtwara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Jimbo la Nanyamba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua Mradi wa Maji wa Makonde ni chakavu na unahitaji ukarabati. Katika mpango wa muda mfupi kwa mwaka 2023/2024, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.5 ambapo tayari zaidi ya shilingi milioni 200 zimetolewa kwa ajili ya kufanya ukarabati wa mabomba ambapo, kazi ya ulazaji mabomba inaendelea na tayari umbali wa kilometa tano umekamilika kati ya 31 zilizopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mrefu, Serikali inaendelea na ukarabati mkubwa wa mradi wa Makonde kupitia mradi wa Maji wa Miji 28 utakaogharimu shilingi bilioni 84.7. Utekelezaji wa mradi huu umeanza mwezi Juni, 2022 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Hadi sasa utekelezaji 40% umekamilika. Kwa mradi huu kutaondoa tatizo la maji katika Halmashauri ya Mji wa Newala, Wilaya ya Tandahimba na Halmashauri ya Mji wa Nanyamba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chikota swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza. kazi aliyopewa sasa hivi Mkandarasi ambaye anafanya ukarabati mkubwa ni kupeleka maji katika matenki makubwa na hakuna fedha za *distribution*.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura kutenga fedha nyingi kwa ajili ya usambazaji wa maji kwenye vijiji husika na mradi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili ni kutaka kujua maendeleo ya mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma na kupeleka Mtwara Manispaa ambao utanufaisha Wilaya ya Mtwara na Halmashauri ya Mji wa Nanyamba.

Je, mradi huu utaanza kutekelezwa lini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chikota kama ifuatavyio:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *distribution,* katika miradi yote ambayo fedha zinaanzisha miradi ya kutengeneza vyanzo, *distribution* huwa zinafanywa na mamlaka zetu. Hivyo Mheshimiwa Mbunge mpango wa Wizara ni kuhakikisha mara baada ya kukamilika eneo la kwanza la utekelezaji, namna ya kufanya *distribution* ndiyo kazi ambayo itafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili, maendeleo ya matumizi ya Mto Ruvuma kupeleka maji Mtwara, hiki ni kipaumbele cha Wizara. Mto Ruvuma ni Mto ambao tunautegemea sana kama chanzo cha uhakika hivyo na chenyewe pia kitaendelea kutumika kadri fedha tunavyopata kwenye Wizara, tutahakikisha tunatekeleza Mradi huu wa Maji wa Mto Ruvuma.

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Tunaenda Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 106

**Wakandarasi wa Kagera waliopata kazi ujenzi Bomba la Mafuta**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza: -

Je, wakandarasi wangapi kutoka Mkoa wa Kagera wamepata kazi katika mnyororo wa ujenzi wa Bomba la Mafuta la Hoima – Tanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakandarasi Wakuu wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Chongoleani (Tanga) wameendelea kushirikiana na Wakandarasi wadogo wajenzi pamoja na watoa huduma mbalimbali katika maeneo yote inayopitiwa na mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mkoa wa Kagera hadi sasa, jumla ya wakandarasi na watoa huduma 42 wamepatiwa kazi mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa ujenzi wa mradi huu, zikiwemo uuzaji wa vifaa vya ujenzi, huduma za usafirishaji, ulinzi, usambazaji wa mafuta, huduma za umeme na hoteli, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Neema, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufanya rejea kwenye zana nzima ya *local content* ambayo imeweka takwa la kisheria kwamba, katika miradi wakandarasi kwa maana fursa za zabuni pamoja na ajira ziweze pia kupatikana kwa wale wanaotoka kwenye maeneo ya mradi *(host community)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, katika hao 42 waliowasilishwa hapa na Serikali ambao amesema kwamba ni wakandarasi pamoja na watoa huduma. Ukweli ni kwamba hao

42 ni watoa huduma *(local suppliers)* na siyo wakandarasi *(local contractors)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, swali langu la kwanza. Je, Serikali ipo tayari kufanya tathmini ya kina, kuweza kuainisha maeneo na fursa ambazo wakandarasi wa Mkoa wa Kagera wanaweza wakapewa kinyume na ilivyo hivi sasa? Fursa zingine wamepewa wakandarasi kutoka mikoa mingine, kama Mwanza ili hali Mkoa wa Kagera wanao wakandarasi wanaoweza kufanya kazi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali kupitia Wizara ya Nishati wapo tayari kuja Mkoa wa Kagera ili kukaa na Uongozi wetu wa Mkoa wa Kagera chini ya Mkuu wa Mkoa wetu Mheshimiwa Fatma Mwasa, kujadili na kuona namna bora ya kuhakikisha kwamba Wakandarasi wa Mkoa wa Kagera wanapata fursa *(local contractors),* jambo ambalo litaweza kuhakikisha ulinzi wa mradi *(host community)* kinyume na ilivyo hivi sasa jambo ambalo linasikitisha, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu waiziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Neema Kachiki Lugangira, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kufanya tathmini, kwa kuwa Mradi huu wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima Uganda mpaka Chongoleani Tanga umefikia 32.6%. Nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunavyoendelea kwenye utekelezaji wa mradi, tutahakikisha wakandarasi wadogo ambao wanatokea maeneo ambapo mradi unatekelezeka wanaendelea kupewa fursa, kadri ambavyo tunaendelea na utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kutemebelea Mkoa wa Kagera Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie, tutakuja ili kuweza kuona ni namna gani tunaweza tukashirikiana kwenye masuala haya ya msingi ambayo tunaamini yanagusa jamii ya watu wa Kagera. Lakini vilevile kwa kwa jamii zote ambazo mradi

unatekelezeka tutahakikisha tunafanya hivyo kwa maslahi ya wananchi vile vile kwa maslahi ya utekelezaji wa mradi, ahsante

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hoja ya Dharura

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae nitakupa nafasi.

Waheshimiwa Wabunge tunashukuru sana kwa maswali ambayo mmeuliza Serikali na Serikali tunashukuru kwa majibu ambayo tumeyapata nashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, yapo matangazo; tangazo la kwanza ni wageni walioko Bungeni asubuhi hii, wapo wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wageni wa Mheshimiwa Spika na Rais wa *IPU* ambao ni viongozi wa Benki ya *NMB* ni Bi. Ruth Zaipuna, Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB; Bwana Filbert Mponzi, Afisa Mkuu Biashara na Wateja Binafsi; Bi. Vicky Bushubo, Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Serikali na Ofisi Ndogo ya Makao Makuu Dodoma; Bi. Rahma Mwapachu, Mkuu wa Kitengo cha Masoko Mawasaliano na Mahusiano; Bi. Janeth Shango, Meneja wa Kanda ya Kati – Dodoma; Bi. Qeen Uroki, Msaidizi Binafsi wa Mtendaji Mkuu; na Bi. Grace Matemu, Meneja wa Tawi la Bunge hapa Dodoma, ahsante. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine watatu wa Mheshimiwa Spika na Rais wa *IPU* ambao ni Wakimbiza Mwenge wa Kitaifa; tunaanza na Bwana Emmanuel Hondi, Atupokole Mhalila na Martha Mkanga. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni 38 wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Mbunge na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kutoka Rombo Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 33 wa Mheshimiwa Omary Kipanga, Mbunge ambaye pia ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia

ambao ni Wenyeviti na Makatibu wa Wilaya na Tawi kutoka Jimbo la Mafia Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 119 wa Mheshimiwa Husna Sekiboko ambao ni Viongozi wa UWT kutoka Mkoa wa Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni tisa wa Mheshimiwa Joseph Thadayo ambao ni Wachungaji Wanawake wa KKKT kutoka Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge, ambaye ni Mchungaji wa Kanisa la KKKT kutoka Mkoa wa Iringa, Ndugu Ombeni Martin Ulime, ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa John Pallangyo, Mbunge, ambao ni wapiga kura kutoka Arumeru Mashariki Mkoa wa Arusha, ahsante. *(Makofi)*

Mgeni wa Mhe. Mwita Waitara Mbunge, ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Kata ya Binagi Wilaya ya Tarime, Ndugu Richard Matiko Masana, ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Moshi Kakoso ambaye ni Mwalimu Renatus Patrison Benson ni Mwenyekiti wa Wakuu wa Shule za Msingi Wilaya ya Tanganyika, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mgeni wa Mheshimiwa Mary Masanja ambaye ni mfanyabiashara kutoka Jiini Dar es Salaam, Ndugu Happyness Biringi, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 27 wa Mheshimiwa Edward Olelekaita ambao ni Madiwani, Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Siasa kutoka Kiteto Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kwanza, wageni watano wa UWT kutoka Ukerewe. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 80 wa *British English Centre* kutoka Jijini Dodoma, ahsante karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 74 na walimu saba wa shule ya msingi *Alliance* kutoka Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni mmoja Ndugu Shose Susan Katende kutoka *UK*, ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge; Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wetu kuwa yale mafunzo yaliyopangwa kutolewa na Serkretarieti ya Maadili ya Viongoizi wa Umma, kuhusu Mfumo wa Uwasilishaji Tamko kwa Njia ya Mtandao ambayo awali yaliahirishwa, sasa yatafanyika kesho Siku ya Jumatano tarehe 8 Novemba, 2023 mara baada ya kusitishwa kwa shughuli za Bunge saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kuhudhuria mafunzo haya muhimu, ili kupata uelewa wa utendaji kazi wa Mfumo huo wa Kuwasilisha Tamko kwa Njia ya Mtandao.

Lipo tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania. Anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wanawake *(TWPG)* kuwa, tarehe 9 Novemba 2023, kuanzia saa nane mchana kutakuwa na uzinduzi wa Programu ya Malezi *(Mentorship Program)*. Uzinduzi huo utafanyika takika Ukumbi wa Msekwa. Wanaombwa wote kushirirki, tangazo hilo kutoka *TWPG*.

Waheshimiwa Wabunge naomba nirudie tangazo la wageni wa Mheshimiwa Spika, wapo wageni waliokaa Jukwaa la Spika ni wageni wa Mheshimiwa Spika na Rais wa *IPU* ambao ni viongozi wa Benki ya *NMB,* naomba niwataje kama ifuatavyio: - *(Makofi)*

Wa kwanza ni Bi. Ruth Zaipuna ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya *NMB,* karibu sana; Bwana Filbert Mponzi, ambaye ni Afisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi, karibu sana; Bi. Vicky Bushubo, ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Serikali na Ofisi Ndogo ya Makao Makuu Dodoma, karibu sana; yupo Bi. Rahma Mwapachu ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Masoko Mawasaliano na Mahusiano; yupo Bi. Janeth Shango

ambaye ni Meneja wa Kanda ya Kati Dodoma; yupo Bi. Qeen Uroki ambaye ni Msaidizi Binafsi wa Mtendaji Mkuu, ahsante sana; na yupo Bi. Grace Matemu, Meneja wa Tawi la Bunge, ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa.

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Spika na Rais wa *IPU* ambao ni Wakimbiza Mwenge wa Kitaifa; Bwana Emmanuel Hondi, karibu sana, na Atupokole Mhalila, karibu sana na Martin Mkanga, karibu sana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Innocent.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali langu la msingi namba 101, katika majibu ya Serikali kwenye swali la nyongeza sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu hayo maeneo yote aliyosema kwa *DC*. Nimeandika barua kama Mbunge na Ofisi yangu ya Bunge, kulalamika suala hilo vilevile nimeenda kumfata Msajili wa Mahakama aliyekuwa Ndugu Kaida ni kutoa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nataka nipate mwongozo wako, ninapoambiwa kwamba niandike barua sasa nandika barua kwa watu gani? Wakati huko kote nimeshaandika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Innocent Kalogeris kwa mujibu wa kanuni zetu, Kanuni ya Mwongozo ni Kanuni ya 76 ya kanuni zetu, akielezea swali lake 101 lakini swali la nyongeza kwamba hakupata majibu sahihi kama alivyotarajia.

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni zetu, Kanuni ya 53(4) inasema, iwapo Spika ataridhika kuwa swali la Msingi au la nyongeza halijapata majibu ya kuridhisha ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika kikao kingine cha Bunge. Sasa, kwa kuwa jibu hilo siwezi kuwa nalo kwa muda huu hapa, kwa maana hiyo nitajiridhisha basi katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)* halafu baadaye tutaendelea, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DEUS C. SANGU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya dharura.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deus Sangu.

**HOJA YA DHARURA**

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nasimama kwa Kanuni ya 79 ili niombe Shughuli za Bunge ziahirishwe tuijadili jambo mahususi liliotokea Jimboni kwangu. Kwa ruhusa yako nitatoa maelezo ya mwanzo ili niombe Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono tujadili jambo hili kwa uzito wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara zaidi ya mara tatu nimesimama ndani ya Bunge hili, kulalamika juu ya mgogoro uliopo kati ya wananchi wa Kata ya Msanda Muungano, Kijiji cha Sikahungu na Songambele Azimio juu ya mgogoro walionao na mwekezaji wa Shamba la Malonje anayeitwa *Efatha Ministry.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelalamika sana hapa kwenye Wizara ya ardhi wanapo-*table* bajeti yao, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Isitoshe Bunge la Bajeti lililopita Mheshimiwa Spika, alimuelekeza Waziri wa Ardhi wakati huo Mama yangu Mabula kwamba aende ahakikishe mgogoro huu unaisha kwa sababu umekuwa wa muda mrefu lakini bado hamna hatua iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimeuliza swali hilo hilo ndani ya Bunge hili kuomba Serikali ichukue hatua kumaliza Mgogoro Mheshimiwa Waziri Jerry Silaa, ameahidi atakuja tarehe 17 lakini

kabla hajafika kumetokea jambo la ajabu sana. Askari wanaolinda shamba la mwekezaji huyo wamewapiga wananchi risasi walikuwa shambani, wanaendelea na shughuli za kilimo kwenye shughuli zinazoendelea tunajua mvua zinanyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamefika na silaha za moto na kuwapiga risasi wananchi na kuwanyang'anya ng'mbe 42. Wananchi waliopigwa risasi ni, wa kwanza anaitwa Eliudi Kauzeni, yeye amepigwa risasi tano kichwani na yuko Hospitali ya Rufaa Mbeya anaendelea na matibabu na hali yake si nzuri.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Heee! Risasi tano!

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, hajafariki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilizane.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwananchi mwingine anaitwa Dalson Charles, yeye alipigwa risasi ya tumboni, na mwananchi wa tatu anaitwa Festo Kamwanga, yeye amepigwa risasi moja ya shavu na nyingine kifuani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo nimeyaeleza, na wakati fulani nilieleza kwa uchungu mkubwa ndani ya Bunge hili, lakini Serikali sijui ni nini kinachotokea. Aidha ni kwa makusudi au kwa sababu ya *interest* fulani zilizojificha jambo hili halijashughulikiwa. Na haya matukio ni kwa uchache tu, hawahawa walinzi hawa wamekuwa wakifanya shughuli za kuwabaka akina mama. Nina orodha ya akina mama 10 walioripoti kwangu ambao walibakwa kwenye jambo hili la hawa askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawaishii, mama mmoja mwezi wa kumi na moja mwaka jana, mjamzito, akiwa anafanya shughuli kwenye bustani shambani, askari hawa walinzi wa shamba hili wameenda pale. Yule mama mjamzito katika

purukushani za kukimbia akaanguka akapoteza maisha. Isiishie tu, kuna wananchi walikatwa masikio na hawa walinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inasifika duniani kote kwa suala la utawala bora. Ni tunu hiyo ambayo imekuwepo enzi na enzi katika tawala zote za Serikali ya Tanzania. Sasa huyu mwekezaji ni nani ambaye anachukua mamlaka makubwa ya kutaka kuua watu kwa risasi? Ni akina mama wangapi wanatakiwa wabakwe ili Serikali ichukue hatua? Ni wananchi wangapi, yaani idadi gani inatakiwa ifikiwe wafe ili Serikali ichukue hatua? Inatakiwa wananchi wangapi wakatwe viungo vyao ili Serikali ichukue hatua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa uzito wa jambo hili, naomba nitoe hoja Waheshimiwa Wabunge, ili muniunge tujadili. Naomba Kutoa Hoja.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsanteni Waheshimiwa Wabunge. Naomba mketi.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Deo Sangu, Mbunge, kwa Kanuni ya 79, akielezea haya ambayo ameyaeleza na sina sababu ya kuyarejea na ni mambo kidogo mazito. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Sangu umesikika vizuri, lakini kwa sababu, Serikali ipo humu ndani, tuko na Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri na Serikali nzima, naomba niwape nafasi upande wa Serikali, uweze kutoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge wote ambao tuko kwenye kikao chetu cha leo, maelezo ya tukio la jana aliyoyaeleza Mheshimiwa Mbunge ni kweli, imetokea hiyo. Nitangulie kwanza kutoa pole kwa waathirika wote na kwa namna yoyote ile nimepata ushirikiano mkubwa sana kutoka

kwenye uongozi wa Mkoa ambao wamefuatilia mienendo na mwelekeo wa hao majeruhi. Kwa hiyo, mgonjwa mmoja kweli alikimbizwa Mbeya kwa ajili ya kuangaliwa zaidi, lakini kwa mujibu wa *RCO* pale Rukwa amesema majeruhi wanaendelea vizuri, mmoja yupo rufaa Kanda ya Mbeya na mwingine yuko rufaa Sumbawanga, yule wa tatu hata hakwenda hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati najibu lile swali la mdingi la Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Waziri alisimama na kutoa mwelekeo wa kwenda kule kwa ajili ya kwenda kulitatua hili jambo. Limekuwa ni la muda mrefu, ni kweli, lakini niwaombe tu, nikuombe Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wawe na utulivu wakati ambapo Serikali sasa tunaenda kuchukua hatua za haraka katika kuliondoa hili kwenye migogoro ya wananchi na wawekezaji, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wetu wa Ardhi.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo naomba usubiri.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Deo Sangu pamoja na Waheshimiwa Wabunge, tumesikia maelezo ya Serikali kuhusu jambo hili ambalo limetokea katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge, lakini ambalo linahusu mgogoro wa shamba kati ya wananchi na Taasisi ya *Efatha Ministry.*

Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa, Serikali imetoa maelezo hayo, nadhani jambo la msingi sasa hapa niiombe Serikali kwanza kwenda kwenye eneo la tukio haraka iwezekanavyo na kwenda kuangalia hali ya majeruhi ilivyo kwenye hospital izote, kwa maana ya Hospitali ya Mkoa wa Rukwa pamoja na Mkoa wa Mbeya na kuangalia namna ya kuwasaidia matibabu haraka iwezekanavyo wananchi hawa ambao wamepata matatizo haya makubwa yaliyofanyika. Pia washiriki mazishi kwa hao ambao pengine wamepoteza maisha, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Lakini pia, tuombe sasa mwende haraka iwezekanavyo sio tarehe 17 kama ulivyosema, nadhani kuna haja ya kuwahi

mapema, ili kuona changamoto hii kubwa inafika mwisho katika eneo letu hili la Kwela kwa Mheshimiwa Mbunge wetu Deo Sangu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Deo naomba kwa sababu, Serikali ni sikivu na iko hapa, naomba iji-*commit*. Naomba tuwaelekeze waje washughulikie jambo hili kwa haraka iwezekanavyo. Ahsanteni sana.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**na**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge tunaanza mjadala ulio mbele yetu ambao unahusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Ninayo orodha hapa ya wachangiaji wetu mchana huu. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita. Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa ajiandae.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge waliochangia jana kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na mawaziri wote wawili ambao wamewasilisha mpango wao. Lakini pia nitumie fursa hii kukupongeza wewe na Kamati yako ya Bajeti kwa kazi nzuri ya uchambuzi ambayo mmeifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi ya muda sitaweka utangulizi mrefu, lakini nitajikita kwenye hoja moja ambayo ninadhani ni muhimu sana kwa maslahi mapana ya Taifa letu, ili tuweze kupata ile picha kubwa ya Tanzania tunayoitaka katika kipindi cha miaka mitano, miaka 15, miaka 25, miaka 50, kadiri ya malengo makubwa ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Muda Mrefu. Miongoni mwa vitu ambavyo vimejitokeza kwenye tathmini ya mwenendo wa uchumi wa Taifa letu ni ukubwa wa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii umeionesha kwanza kwenye ripoti yako, ukurasa wa sita, umeichambua vizuri sana, ninakupongeza. Lakini pia Mheshimiwa Waziri ameichambua na kuieleza vizuri sana kwenye hotuba yake, ukurasa wa 20. Kwamba, moja katika changamoto ambazo zinatukwamisha sana ni hii nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa na huduma ambayo kwa sehemu kubwa ndio imechangia hata kuadimika kwa dola, lakini pia imekwamisha ufanyaji biashara. Wafanyabiashara wengi wakubwa leo wanashindwa kuagiza bidhaa nje ya nchi kwa sababu hawana Dola. Na hili ni tatizo kubwa sana kiuchumi na hatuwezi kulichukulia katika uzito mwepesi, ni lazima tulichukulie katika uzito wake mkubwa. Ninakushukuru Mheshimiwa Waziri, Profesa wangu, Mheshimiwa Profesa Mkumbo, umelifafanua kwenye ukurasa wa 20 wa hotuba yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa sita wa kamati unaeleza namna ukubwa wa tatizo hili; inaeleza kwamba, kati ya mwaka 2021 na 2022 nakisi imeongezeka kwa asilimia 54.8; hili ni ongezeko kubwa sana. Kamati kwenye taarifa yake inaeleza sababu, Mheshimiwa Waziri hajazisema, lakini Kamati imeeleza sababu za ukubwa wa nakisi hiyo ambayo ina madhara

makubwa sana kiuchumi. Nitazitaja zile sababu ambazo ziko ndani ya uwezo wetu kwa sababu, nyingine ziko nje ya uwezo wetu na mimi sipendi kushughulika na mambo ambayo hatuna uwezonayo. Masuala ya vita ya Urusi na Ukraine hayatuhusu, hatuna uwezo nayo, nitazungumza sababu ambazo Kamati imezieleza zile ambazo tuna uwezonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni uagizaji wa bidhaa nyingi za ujenzi kutoka nje ya nchi. Hilo tunalijua, tunajenga *SGR,* tunajenga miradi mikubwa ya umeme, Bwawa la Mwalimu Nyerere, hayo yamechangia kwa asilimia kubwa sana kuongeza ukubwa wa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa na huduma katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiachana na hayo ambayo hatuna uwezo wa kuya-*control,* kwa sababu tuna miradi hii mikubwa tunaijenga, tunazo bidhaa nyingi ambazo tunaziagiza kutoka nje ambazo zimechangia pia ukubwa wa nakisi hiyo. Moja wamesema mbolea, mbili wamesema mafuta ya kula, tatu wamesema ngano, nne wamesema mazao ya petroli. Kwa hiyo, hayo kwa sehemu kubwa yamechangia ukubwa wa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yaliyotolewa; mapendekezo haya yapo kwenye ukurasa huohuo wa 20 wa Serikali. Wamesema suluhisho ambalo limependekezwa ni kwamba, kupunguza nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa kwa kuongeza mauzo ya nje ya nchi. Yaani tumalize hilo tatizo kwa kuongeza mauzo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *it is very logical,* ni sahihi kabisa, tuongeze mauzo ya bidhaa nje ya nchi ili tuka-*attract* dola ije, ili tupunguze hiyo nakisi, na ikiwezekana kuiondoa kabisa. Hata hivyo, changamoto yangu ni mapendekezo ya aina ya bidhaa ambazo tunataka tuzipeleke nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo matatu ninakubaliananayo vizuri kabisa. Mheshimiwa Waziri ameeleza kuhusu madini, tunaweza kufanya vizuri tukauza madini sana nje ya nchi. Ameongea kuhusu mazao ya misitu, *excellent,* tuna

uwezo nayo hayo mazao ya misitu, tukayauza nje, tumefanya vizuri. Lakini pia kwenye eneo la huduma ameeleza umuhimu w kupanua huduma ya utalii. *Excellent,* tutafaulu sana kwenye eneo hilo na tayari tupo vizuri tunaongeza nguvu tu hapo, tuna-*concentrate efforts* zetu kwenye maeneo hayo matatu tayari tupo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna eneo moja ambalo tunalisahau sana; tunalisahau lakini lina manufaa makubwa sana katika uchumi wa Taifa letu. leo walaji wakubwa wa nyama wako *Middle East,* wapo Mashariki ya Kati, na sisi tupo katikati ya Mashariki ya Kati na nchi ya Brazil. Ni kichekesho sana kuliona Taifa letu katika mwaka 2022 limesafirisha nyama tani elfu 10 pekee ilhali Brazil wamesafirisha tani za nyama milioni 2.9, ilhali tupo karibu zaidi na soko kuliko Brazil. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Mipango, kwenye vipaumbele na mwenyewe umetwambia kupanga ni kuchagua. Hatuwezi kufanya kila kitu, hatuwezi kuwa *junk of all trades,* lazima tuchague, umechagua utalii, umechagua misitu, umechagua madini, ninaomba uongeze nyama kwenye sekta hiyo. Na sababu, zipo wazi, kwanza, *critical mass* ambayo itapata faida kutokana na biashara hiyo; tunao wafugaji wengi tunachohitaji ku-*coordinate* ufugaji tupate nyama tukatumie hilo soko. Kwa hiyo, sehemu hiyo naomba iwe mchango wangu; kwamba, kwenye kupunguza nakisi ya urari wa biashara kwa kuongeza mauzo ya nje tuongeze na biashara hiyo, tuwe na vitu walau vinne, vinne vitoshe, kwa sababu tumevifanyia *study* kwamba vinaweza kuchangia uchumi mkubwa wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sehemu ya pili. Mheshimiwa Waziri hajasema, naomba nimuongezee kwenye mkakati wa kupunguza hiyo nakisi. Ameongelea zaidi kwenye kuongeza mauzo ya nje. Na nimesema kwenye hoja ya Kamati, imeeleza vizuri sana, changamoto ni mauzo yetu ya nje madogo, lakini pia tunaagiza bidhaa nyingi sana toka nje ya nchi *unnecessarily.* Tunalazimika tutoe dola yetu ya ndani tuipeleke nje tukanunue vitu ambavyo tuna uwezonavyo, tuna uwezo wa kuzalisha mafuta ya kula Watanzania, leo tuna …

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhagama kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kingu.

**TAARIFA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa kaka yangu anayechangia hoja *very scientific,* Mheshimiwa Dkt. Mhagama, kwamba, nakisi iliyotajwa katika ripoti hii kwa Mkoa wa Singida peke yake kwa juhudi zilizofanywa na Serikali ya Rais huyu huyu chini ya Wizara ya Kilimo inayoongozwa na Mheshimiwa Bashe, uzalishaji wa mafuta, mbegu za mafuta na ukamuaji wa mafuta umepanda kwa kiwango ambacho kimesababisha sasa hivi bei ya mafuta imeshuka sana. Kwa hiyo, ninampa taarifa msemaji kwamba, moja ya bidhaa zilizotajwa zinazotoa fedha nyingi za kigeni ni uagizaji wa mafuta, na nchi mwaka huu imejitosheleza sana na uzalishaji wa mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa msemaji kwamba, achukue na hilo kuiambia Serikali hii sikivu kwamba habari ya kuagiza mafuta tunaweza tuka-*adjust policy* zetu katikati kulingana na uzalishaji mkubwa uliofanikiwa kutokana na juhudi kubwa za Wizara ya Kilimo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Dkt. Mhagama, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nipokee kwa mikono miwili taarifa ya *comred* Kingu, mwamba na *main campaigner* wa ushindi wa Mheshimiwa Spika. Ninampongeza na ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndio hoja yangu. Kwa sababu ya muda nimuombe Mheshimiwa Waziri, kwenye hoja namba sita, kwenye ukurasa ule wa 20 ameweka hoja namba sita

ambayo inahusu kuongeza mauzo ya nje. Naomba aongeze hoja namba saba, kupunguza ununuaji wa bidhaa ambazo tunaweza kuzizalisha ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nina takwimu, lakini kwa sababu ya muda naomba nizitaje tu; mbolea mpaka mwaka jana, Mheshimiwa Bashe nampongeza sana, asilimia 12 ya mbolea tuliyotumia nchini tumezalisha ndani ya nchi hii. Asilimia inayobaki kama tani 617,000 bado zinaagizwa nje. Mheshimiwa Bashe umeshaweza kwa asilimia 15, unaweza kwa asilimia 80, *we can make it. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo la pili, petroli. Wizara ya Nishati mmepambana sana mna masuala ya gesi, n.k. Tupunguze uagizaji wa petroli, tutumie bidhaa zetu za ndani zinazoweza ku-*solve,* hizo ni *alternative products. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye mafuta ya kula inatudhalilisha Watanzania kuona kwamba mpaka leo asilimia 60 ya mafuta tunayokula nchini tunaagiza kutoka nje, *what a shame? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kwa Tanzania hatustahili hilo. Mheshimiwa Bashe umepambana kwenye eneo hilo. Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ongezeni nguvu kwenye sekta hiyo tuimalize na tuweze kutatua tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna eneo la ngano limefafanuliwa vizuri. Hayo ni mazo ambayo unapozidi kuyaagiza nje unawanyima Watanzania fursa ya masoko, unawanyima Watanzania fursa ya kukua, halafu unaendelea kuendeleza uchumi wan je wakati tuna nakisi kubwa ya fedha za kigeni kwa hiyo, tuna eneo la sukari na mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, sehemu ya mchango wangu nitaiandika na nitaiwasilisha Serikalini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama kwa mchango mzuri sana.

Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mheshimiwa Festo Sanga jiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwa sababu ya muda niruhusu nimpongeze Rais peke yake. Tunampongeza Rais kwa kuleta mapendekezo ya Mpango huu na mpango huu kwa mara ya kwanza unakuja wakati tuna Tume mpya ya Mipango na sheria mpya na Wizara maalumu inayoshughulikia mipango ya Serikali. Kwa hiyo, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa ukweli kwa *direction* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nampongeza Rais kwa hatua ambazo zina maana kubwa sana, maridhiano, ustahimilivu, mageuzi na kujenga upya. Nilivyokuwa nasoma Hotuba ya Profesa Kitila Mkumbo, kwanza *is very radical*, hotuba Fulani, imechukua *angle* fulani hivi ambayo ndiyo tunataka. Tunataka mipango ambayo inaelekezwa kwenye vijiji vyetu. Watanzania walio wengi wako vijijini, hivyo, tunataka *focus* ya mpango huu iende kweney *rural development*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *data* za Serikali hapa, mikopo ya biashara shilingi trilioni 22 halafu *second percent* peke yake ndiyo imeelekezwa kwenye kilimo, wafugaji na wavuvi. Hii haiwezekani, hapana. Kama ni kweli tunataka twende kwenye *rural development*, lazima tuweke pesa nyingi sana kuelekeza kwenye kilimo, mifugo na uvuvi. Kwa sababu, ndiyo Watanzania wengi wako huko. Tukiwa na mipango ambayo ina-*move* na watu walio wengi, hapo ndiyo tunazungumzia habari ya maendeleo. Maendeleo ni watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kila wakati tunakuja hapa halafu tunasema tunawekeza kwenye kilimo, kwenye ufugaji na uvuvi lakini hatuoni, haiwezekani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Profesa Kitila *assignment* yako ya kwanza sasa, tunataka hii *rural economic development* tuione, huko vijijini siyo

kwenye vitabu. Tunataka tutoke kwenye vitabu sasa. Hii nchi ina *documents* nyingi, nzuri sana, lakini tukienda kule kwenye vijiji vyetu hatuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naangalia hii, ni kweli wafugaji wametajwa, wakulima wametajwa na wavuvi, lakini ukisoma hii huoni *tangible*, vitu ambavyo vinamhusu mtu anaitwa mfugaji. Waziri amezungumzia habari ya kuwa na viwanda na kuziongezea thamani *products* zinazotokana na mifugo. *Honestly* hivi ipi ya kwanza, ni mahali pa kuhifadhia hii mifugo au wanataka viwanda? *I think* Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi ukurasa wa 52 tuliweka *commitment* kwamba, kuhakikisha tunatenga maeneo ya ufugaji yapimwe na *infact* tumeweka mpaka *statistics,* mpaka zifike hekta milioni sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kabla hatujazungumza habari ya viwanda, lazima tuwe na maeneo ambayo yamelindwa kisheria. Tukishakuwa na maeneo hayo ndiyo tuzungumze habari ya viwanda. Kwa hiyo, tunataka bajeti zijazo na Mpango wake tuone bajeti kubwa ikienda kwenye maeneo haya. *We are not interested in reading nice documents,* tunataka kuona *tangible results*. Nilikuwa nasoma hapa mpango wetu huko kwa wakulima; "kuendeleza juhudi za kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula nchini na kuendelea kuongeza matumizi ya mbolea, mbegu bora na kilimo na umwagiliaji". *That's fine,* lakini trekta ziko wapi hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali inataka wakulima hawa na wakulima wa nchi hii wanafanya kazi kubwa sana, pamoja na kwamba wakati mwingine wanapata *statements* za ajabu ajabu. Wanaambiwa wanalima kienyeji, wanafuga kienyeji, lakini hizi hizi *documents* ndizo zinazosema *the reason we have fought self-sufficient* zaidi ya asilimia 120, ni kwa sababu ya wakulima hawa. Wanalima hivyo hivyo mnavyoita kienyeji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona hapa tunaona hifadhi ziko nyingi sana, karibu sijui ishirini na ngapi na mapori tengefu. Ukiangalia *size* ya hiyo, lakini uki-*compare* na nchi kama Namibia, ina *National Parks* saba tu. Halafu ukiangalia tunapata nini

kutokana na mapori haya au na sisi tuseme mnahifadhi kienyeji kienyeji hivi? *I think it is high time* twende kwenye *quality*. Alizungumza Mheshimiwa Mbunge wa Mbarali jana hapa, "*Development must be people centered. There is no question of development where by human beings in individuality is being destroyed for the sake of wildlife,"* haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima watu kwanza. Hata hili lililotokea hapa leo tusipoweka *emphasis* kwenye kutetea watu, maendeleo hayana maana. Lazima, *a true definion* ya maendeleo *must start from a human perspective*. Mheshimiwa Profesa Kitila, hapa tunazungumzia habari ya utawala wa sheria, kama nguzo ya maendeleo yetu kama Taifa, nakubaliana, *as a lawyer I agree*. *But what is the rule of law* kama sheria zetu na hapa naongelea msingi huo wa *reforms*. Mheshimiwa Rais anataka *reforms,* lakini tuna sheria za kikoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eti mfugaji ng'ombe wameingia shambani halafu *we are not interested with a fine*, eti una-*forfeit*. Una wa-*impoverish* watu halafu tunazungumza habari ya mipango, wakati sisi na mpango huu tulitaka Watanzania watajirike. Sasa, lazima tuamua, tuendelee kuwa na sheria ambazo zinawa-*impoverish* watu ama tuwe na sheria ambazo nia yake ni kukataza matatizo yasitokee. Unapo-*forfeit* ng'ombe leo unam-*impoverish* huyo mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokea kwa sababu ya kuwa na sheria tu ya kikoloni. Mheshimiwa *Attorney General*, sijui kama yuko hapa. Hii *forfeiture,* hii *section* ipo, tangu Sheria ya mwaka 1958 na tumepata uhuru. *We cannot question … (Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edward Olelekaita kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa kaka yangu Mwanasheria kwa mchango mzuri sana

kuhusiana na masuala ya utekelezaji wa sheria. Hivi tunavyoongea Jimbo la Bunda Mjini, Kata ya Kunzugu, familia 16, ng'ombe 500 wameshikiliwa na *TANAPA* na wana mpango wa kuwataifisha, lakini Mahakama imetoa *ruling* walipe faini. Wananchi wanataka kulipa faini ili waokoe ng'ombe wao, lakini *TANAPA* wanakataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nampa hiyo taarifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Olelekaita, unaipokea taarifa?

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba Mheshimiwa Bulaya atupe uthibitisho wa hiyo hukumu inaelekeza nini ili na sisi tuweze kuthibitisha kwa upande wa *TANAPA* na kuweza kuchukua hatua kama ni kweli Mahakama imeruhusu waweze kulipa faini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Edward Olelekaita, malizia mchango wako.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Sasa, sijui hata nisemeje. Siji nipokee ile ama nifanye nini, *anyhow*. Niseme hivi, *in fact* kama Mheshimiwa Waziri, anataka tulete hizo kesi ziko nyingi sana, lakini iko hivi, kwa sababu lazima sasa twende *a step further*. Tukileta atafanya nini? *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilindie muda wangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Lulida.

**TAARIFA**

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sheria na kuna mipaka ilishatengenezwa, *corridor* za wanyamapori na binadamu, lakini vile vile hao wafugaji. Leo wako katika Mkoa wa Lindi. Vurugu za wafugaji kuvamia maeneo na mashamba ya wananchi zimekuwa kubwa, mpaka *wananchi wameuawa na wafugaji. Tusiendelee kukubali vitu ambavyo havitaki kufuata sheria.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende na sheria, Serikali ina sheria yake na wafugaji watii sheria ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa hiyo. Sasa hivi twendeni Lindi mkaone migogoro ya wafugaji kuvamia maeneo ya wakulima na kuleta kero kubwa katika mazingira haya, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Ngoja, Mheshimiwa Riziki, tunashukuru kwa taarifa yako. Hii taarifa ulikuwa hunipi mimi, ulikuwa unampa Mbunge anayechangia. Mheshimiwa Olelekaita, endelea na mchango.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na namheshimu sana mama yangu Mheshimiwa Lulida. Nilikuwa naongelea kitu tofauti kidogo. Nilikuwa nasema

hivi, hapa tunaongea na Waziri wa Mipango ya Nchi hii *by the way*. Kwa hiyo, wengine watulie kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema hapa mipango ya nchi na Mheshimiwa Profesa Kitila amesema vizuri sana hapa, amezungumza jambo sawa. Amesema, Mpango wa Maendeleo wa Taifa siyo mpango wa Serikali *and it is true*. Tutatarajia sasa kabla ya ule mpango mkubwa kuja, sasa waje watwambie wamewa-*consult* watu akina nani. Pengine *this time*, hebu waanzishe mjadala wa Kitaifa tuzungumze habari ya Mpango huu wa Taifa, kwa sababu nakubali, siyo mpango wa Serikali, ni mpango wa Taifa letu. Kwa hiyo, hiyo *statement* ni nzuri sana, tunataka tuone. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa wameongelea kuhusu watumishi wa umma na ni kweli, *engine* ya mipango ya yote ya Serikali ni watumishi wa umma *and I agree with you,* amem-*quote* mpaka Waziri Mkuu wa *Singapore*. Kama tunataka kufuata njia ya *Singapore* unajua lazima tuwe na *discipline* sasa. *It is not enough* kusema twende kama Singapore, *no*! Lazima tujue *Singapore* wamefanya nini ili tutembee kwenye hiyo barabara. Hapa Waziri ametengeneza *quotation* nzuri sana na watu wengine huwa wanafikiri, kuna wakati *Singapore* pia walianza kufikiri mfumo wa elimu yao pengine sio mzuri kama tulivyo leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengine wanasema hivi, unajua kwa nini Marekani watu wao ni *innovators* na ukiangalia wale watu wakubwa, sio kwamba walikuwa na *distinctions* kwenye *universities, no!* tofauti ya vyuo vyetu na nchi nyingine, kwa mfano kama Marekani, wao wanachoangalia *they are interested in who you are as person rather than the test* ulizopata kwenye *distinction* yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *they appreciate those who take bold decisions, those who do nothing, do things differently, those who overcome problems, those who are street smart, those who see the world for what they can do, not what they cannot do. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na sheria ambazo zinaleta *barriers* leo, badala ya ku-*support* hizo *innovation* na watu wa umma, sisi tumeletewa Ripoti ya *CAG* hapa. *That is a very good test,* kama tunataka nidhamu kwa sababu Waziri amesema ndio nguzo ya mpango huu, ni kutekeleza ripoti kama za *CAG*, lakini tutakwenda *a step further* na kusema *what is wrong with recruitment*? Halafu tubadilishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Olelekaita, kwa mchango wako mzuri sana.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo, Mheshimiwa Ole-Sendeka.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama chini ya Kanuni ya 76 kuomba mwongozo wako kwa maneno yaliyosemwa na mtu ambaye namheshimu sana mama yangu, dada yangu, Mheshimiwa Lulida akieleza kwamba jinsi ambavyo wafugaji wameenda mpaka huko Kusini na akasema kuna wafugaji ambao wamekuwa wanaua watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lugha ya wafugaji wanaua watu, wafugaji bila shaka pia ni watu nina hakika, ni kupanda mbegu ya uhasama kati ya wafugaji waonekane ni watu wa hatari katika nchi hii. Bila shaka anayeua atakuwa ni mtu mwenye jina lake mahususi na kama akiua mtu ambaye ni wa jamii ya kifugaji ni mtu. Siyo wafugaji wameua, siyo Wamasai wameua, siyo Wasukuma wameua, sio Watatoga wameua. Ni mtu mmoja kaua ambaye anapaswa kupelekwa Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge afute kauli hii ya jumla ambayo inapanda mbegu ya ubaguzi na kuchochea kuhasimiana kwa makabila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unakubaliana na mimi, kauli hiyo siyo sahihi kutumika katika Bunge hili. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro kwa Kanuni ya 76, akiomba Mwongozo wa Kiti kutokana na maneno aliyoyasema Mheshimiwa Lulida.

Sasa, kwa sababu kanuni inaniambia nitoe Mwongozo hapa au baadaye, kwa hiyo nitarejea kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge, *then* tutatoa mwongozo huo baadaye. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kuendelea kuna tangazo la wageni wa Mheshimiwa Riziki Lulida ambao ni wageni wastaafu kutoka Shirika la Ndege la *ATCL*. Viongozi wa *ATCL* waliopo humu ndani karibuni. Ahsante. *(Makofi)*

Wapo pia viongozi kutoka *TAZARA*, shsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa, nilimtaja Mheshimiwa Charles John Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Sanga na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango, lakini na Mwongozo wa kutengeneza Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa nakubaliana na Hotuba ya Waziri mwenye dhamana ya Mipango na Uwekezaji. Nakubaliana na maelezo ya Waziri wa Fedha kwa mwongozo

alioutoa, tunapotengeneza mpango na tunapotengeneza bajeti. Nina imani kwamba tukifuatilia tutaweza kutoka na mpango mzuri na bajeti nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoanza kuzungumza, naipongeza Kamati ya Bajeti ya Bunge letu, kwa uchambuzi waliofanya katika maandiko haya mawili. Wametoka na maeneo ambayo tukijumlisha na michango yetu sisi, tutaweza kutoka na mchango mzuri. Jambo la kwanza, katika uchambuzi wa kazi ya Waziri wa Fedha lakini hata kwenye wasilisho la Waziri, nachukua fursa hii kipekee kuwapongeza wakulima wa Tanzania tena wakulima wadogo, kutokana na kwamba kazi yao imeweza kuzalisha chakula, tukawa na chakula cha kutosha uwezo wa asilimia 124, tani milioni 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapowapongeza wakulima, sifa zimwendee Mtumishi Mwandamizi lakini ambaye hastahili kupokea sadaka au kuungamisha watu, Msimamizi wa Sekta ya Kilimo na kiongozi wetu mkuu Mheshimiwa Rais ambaye ndiye anampa maelekezo. Mimi ni mmoja ya wakulima ambao tumefaidika na jitihada za Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na mchango wa Kamati yako unayoiongoza, nizungumze kidogo juu ya urari wa biashara ya bidhaa. Naenda kwenye nini kifanyike. Kupita kwenye historia yetu, tulikuwa na *re-export, e-export* ya nchi hii imepungua. Dawa nyingine ni kukimbilia *re-export*. Sina muda wa kulielezea, lakini Wizara ya Fedha na *TRA,* wapitie mjiulize, ni kwa nini *re-export* ilianguka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunafanya *re-export* wakati ule ilipoanguka. Jiulize, kwa nini Kariakoo ilikufa Dar es Salaam lakini ikazaliwa Kariakoo Kampala, ikazaliwa Kariakoo Zambia? Vitenge vinanunuliwa kutoka vitokako, vinakwenda Zambia vinarudi Dar es Salaam. *Re-export, re-export*. Tunapokuja kuwa na bandari yenye ufanisi, kama tusipokuwa na *re-export Policy*, tusipoitengeneza Dar es Salaam au Pwani yenye Kariakoo mpya ambako nchi zilizotuzunguka watu watakuja kwa wingi Dar es Salaam na kufanya biashara hapa. Faida tunayoitegemea

kwenye Bandari ya Dar es Salaam yenye ufanisi, itakuwa ndogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Mipango kwa kusisitiza jambo lililokuwepo ambalo lilikuwa halionekani. Kuchochea na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii vijijini. Serikali imekuwa ikijitahidi kufanya maisha ya vijijini yawe mazuri, yaani maisha ya vijijini sasa yanapendeka na unaweza kuishi. Sasa, Waziri anakuja na jipya kwamba, tuchochee zaidi na anakwenda kwa kuelezea kwamba, tuanzishe utaratibu wa viwanda vijijini, amekuja na falsafa ya *SIDO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuishauri Serikali, hii inawezekana na yenyewe itatusaidia kwenye urari wa biashara ya bidhaa, kwamba watu wazalishe kule. Hii itaendana na lile tatizo linalotusumbua la kuwepo kwa pesa za mikopo na watu wasiweze kukopa. Kumbe unapotaka kuipeleka *SIDO* kule vijijini karibu na wananchi, tofauti na taasisi zingine *SIDO* inafundisha. Mfuko wa Pesa wa *NEDF* ulioko chini ya Wizara ya Viwanda na *SIDO*, hawakupi pesa mpaka wakufundishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wengine wanatoa pesa hata hawamwambii mtu ni pesa ya kufanyia nini. Unampa mtu pesa atengeneze kiwanda, kumbe kiwanda anachokifikiria ni kwenda kulipa mahari. Sasa, unapokuja kukusanya huwezi kukusanya hiyo pesa. Namuunga mkono Mheshimiwa Waziri, haya mawazo yake yafanyiwe kazi kweli. Mimi ni muumini wa viwanda vidogo, ujenzi wa viwanda kwa kutoka viwanda vidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wanavyo zungumza leo Mheshimiwa Waziri wa kilimo anajua, tunayo mafuta mengi ya alizeti lakini kitu ambacho watu hawakijui ni kwamba mafuta ya alizeti ni *royal product*, yanatumiwa na watu wenye uwezo wa hali ya juu, nimemweleza Mheshimiwa Waziri, nimpeleke Ulaya nimuoneshe wanaokula yale mafuta. Kwa hiyo, tupeleke mafuta hayo tuuze tupate pesa nyingi ili tuzalishe zaidi. Kwa hiyo, naunga mkono wazo hilo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Kamati yako, kuhusu suala la riba, mmehoji kwa nini riba hizi hazishuki. Bahati

nzuri nimemuona Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya *NMB*. Benki zinapata faida kubwa, kupata faida kubwa siyo sifa, mimi nilikuwa nafanya kazi huko 'Utashani' nilitaka kufukuzwa kazi kwa sababu nilikuwa napata faida kubwa. Anakwambia *no* unawaonea wateja hiyo riba ipunguzwe na watu wafundishwe, wakifundishwa waweze kukopa, wakikopa waweze kuzalisha ili wachangamshe uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida yake ni kwamba itaweza kutusaidia kutengeneza shughuli ambayo, shughuli zitatengeneza ajira, ajira hizo zitazalisha bidhaa na zitatuepusha katika kuagiza bidhaa ambazo hazina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la urali, umezungumza matumizi ya gesi asilia, matumizi ya gesi asilia kutuokoa haiwezi kuwa mchakato. Mimi nilikuwa *Marketing Manager* wa mambo haya mnayozungumza mwaka 2000, ni miaka zaidi ya 24 tunataka *radical change*, tunataka *reform,* tuanze leo, tunataka mpango unapokuja utamke kwamba magari mangapi ya Serikali Dar es Salaam mpaka Dodoma yanaanza kutumia gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea leo na mtaalam wa gesi, akaniambia gesi inayotakiwa kwa magari yote ya Tanzania ni kiasi kidogo wanayo. Akanihakikishia kwamba tunayo *gas* ya kutosha, sasa *walk the talk* rafiki yangu, litoke tamko magari yote yabadilike. Ukisikia mambo ya *gas* haya yatakuchanganya, wanakuambia *gas* ni nafuu, mafuta ni aghali. Sasa kama *gas* ni nafuu na mafuta ni ghali, kwa nini mnaagiza mafuta ambayo ni aghali mnakataa kutumia *gas* ambayo mnayo ninyi wenyewe, *walk the talk*! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka mpango ambao utakuja unatuambia kesho magari yote yawe *converted* na *TRA* mvumilie kama vifaa vya *gas* vyote vinaushuru samehe ushuru kwa kipindi fulani tuweke hizo *petrol station* za *gas*, tuweke *converter,* tu-*convert* magari halafu watu waende mtaani tupunguze nakisi. Mafuta hayana mbadala, mbadala wake ni kuweza kutumia *gas*, lakini matumizi ya *gas* katika usafirishaji ni kinga la tatizo la ugawaji wa mafuta kama ikitokea majanga huko mbali, kama ikitokea

matatizo huko yanapotoka wewe una *gas* yako utatembea wakati wenzako wanatembelea magoti wewe utaendesha vifaa vyako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine nataka kukiona, nimeusoma mpango siyo kwa ndani, ningependa msitumie vilinganisho vya asilimia..

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoe takwimu baadala ya vilinganisho vya asilimia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Mwijage, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Askofu Gwajima.

**TAARIFA**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa Kaka yangu mtaalam wa biashara, maneno anayosema siyo yake lakini maneno anayosema amevuviwa na Mungu. Kule Jimbo la Kawe *TPDC* kampuni mojawapo yetu ya taasisi ya *energy*, wameanza kuweka *cable* kwenye nyumba za watu wakitumia *gas*. Tumepita sisi mguu kwa mguu, mtu aliyekuwa analipa bili ya shilingi 20,000 kwa mwezi analipa shilingi 3,000. Sasa kwa nini tusichukue maamuzi ya kutumia *gas*. Kwa hiyo, mtaalam wa biashara yupo sahihi kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwijage taarifa unaipokea?

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba Askofu amesema hili nimepewa na Mwenyezi Mungu na mimi Frateri wa kudumu sistahili wala kubisha, nakubali huo upako. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kidogo. Moja; nimeomba wataalam wa Serikali msituletee ulinganisho wa asilimia kama ni

tanzi sema tanzi, kama ni urefu sema kilomita. Hizi asilimia zina udanganyifu, unaweza kuwa na asilimia ndogo lakini wewe ni mkubwa. Mtuambie mpango uje unatamka, lakini tuchague maeneo mahsusi. Kwa mfano, upande wa ufugaji wa Samaki, tunayo *potential* ya kufuga samaki hapa, Tanzania leo tunafuga samaki tani 18,000, Uganda wanafuga 120,000, Egypt wapo milioni 1.2 na wanakwenda milioni mbili. *Quantify* hiki kitu Serikali muwape watu *task,* kama ulivyosema Mheshimiwa Waziri, unataka watu wenye weledi umkabidhi mtu kwamba wewe shughuli yako ni uvuvi na ufugaji wa samaki, tunataka bilioni kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo mtu tumuwajibishe asubuhi au saa sita akishindwa. Haya mambo ya holela holela unatoka unakwenda huku, unasubiri Mheshimiwa Waziri apende nini, ukimuuliza mtaalam wa Serikali, anasema maelekezo. Ni mtaalam kweli lakini hawezi kukwambia chochote anasubiri maelekezo. Tafuta taasisi uwakabidhi vijana kazi washindwe waache kazi. Naunga mkono, kazi ni nzuri, mengine nitawasilisha kwa maandishi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Mwijage, kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Festo Richard Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mheshimiwa Joseph George Kakunda jiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupewa nafasi niweze kuchangia kwenye Mpango wa Serikali. Kwanza ninaipongeza Serikali, kwa mapendekezo waliyonayo kwenda kwenye bajeti ijayo ya trilioni 47 na katika hizo shilingi trilioni 47 Serikali imetoka kwenye trilioni 14 za maendeleo kwa sasa imeenda kutenga trilioni 15 kwa ajili ya maendeleo. Kwa hiyo niipongeze Serikali kwamba inaenda kuongeza zaidi ya shilingi trilioni moja kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha kabisa dhamira ya Mheshimiwa Rais ipo wazi kwenye kuhakikisha kwamba miradi ya maendeleo haisimami kwenye nchi yetu na inaweza kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwenye suala la *financing* ya Mpango wenyewe, kwenye Kamati wamezungumzia hata Serikali imezungumzia kwenye *financing* ya mpango wenyewe. Tuna Mpango mzuri sana lakini ku-*finance* Mpango wenyewe inatakiwa tufanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najikita kwenye mambo matatu. Nitajikita kwenye kodi, mifumo lakini nitazungumzia suala la utalii kwa maana ya Sekta ya Utalii. Ukisoma kwenye Mpango, Mheshimiwa Waziri anazungumza kwamba moja kati ya changamoto ya Serikali ya ukusanyaji wa mapato ni wigo mdogo wa vyanzo vya mapato. Ukienda kwenye mifumo mingi ya Serikali na ambayo tunategemea ndiyo *source* ya ukusanyaji wa mapato, kumekuwa na changamoto kubwa ya mifumo kusuasua, lakini pili kumekuwa na changamoto kubwa ya mifumo kutokusomana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inakusanya mapato lakini mapato yanayokusanywa ni theluthi ndogo tu kuliko mapato mengi zaidi ambayo yangekusanywa kwa ajili ya ku-*finance* mipango na miradi yetu ya maendeleo. Changamoto hii naweza nikatolea mfano, kwenye mfumo mmoja tu ambao umefungwa kwenye Daraja la Kigamboni, Daraja la Kigamboni wamefunga mfumo wa ukusanyaji wa mapato, kabla ya ukusanyaji wa mapato kupitia mfumo, daraja la Kigamboni lilikuwa linaingiza Shilingi milioni 150, 200 hadi 300, baada ya kuweka mfumo Daraja la Kigamboni la Mwalimu Nyerere pale linaingiza Shilingi bilioni moja na milionii 300 kwa mwezi. Hii inamaanisha nini? Watu wengi wanakwepa mifumo Serikalini kwa sababu inawabana na wizi ambao wanaufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupa mfano mwingine, hospitali ya Kibaha pale Tumbi. Kabla haijafunga mfumo kwa mwezi walikuwa wanaingiza shilingi milioni 13, 12, baada ya Serikali kwenda kufunga mfumo wanaingiza shilingi milioni 350, 400 kwa mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatafsiri ya *magnitude* kubwa iliyopo kati ya wizi na ukwepaji wa kwenye mifumo. Ukienda kwenye Wizara ya Ardhi, hapa tukiondoka tukienda pale

TAMISEMI au kwenye Wizara ya Ardhi hapo, mfumo sasa hivi utakuta upo chini. Ukienda kwenye afya hospitalini kuna wagonjwa inawezekana wanatusikiliza sasa hivi wapo kwenye foleni mfumo upo chini. Ukienda *TRA* mifumo ipo chini, lakini hatujawahi kuona hata siku moja mfumo wa ulipaji mishahara ukiwa chini hata siku moja kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatupa *alarm* kwamba siyo kwamba mifumo ina changamoto, changamoto ipo na watu wanaoitumia hiyo mifumo, kwa sababu wanatumia mifumo hiyo kama njia ya wizi. Ndiyo maana *CAG* anasema wana uwezo wa kuzima *POS* kwa siku elfu moja na Serikali isifanye kitu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi mapendekezo yangu kwa Serikali, tuiiombe ione dhamira ya wazi kwanza ya kufanya mifumo isomane, kilio cha Mheshimiwa Rais kwa muda mrefu ilikuwa ni hicho, hasa hasa pale bandarini na maeneo mengine. Pili, kuhakikisha mifumo hii inafanyakazi, kwa sababu tunaweza tukafunga mifumo lakini isifanye kazi. Hilo ni pendekezo langu kwenye suala la mifumo, nikiiomba Serikali, hatuna sababu ya kuruhusu watu waendelee kukutana *face to face*, kukutana kwa watu *face to face* kwenye suala la *payment* kunasababisha majadiliano na rushwa, Serikali inaenda kupoteza fedha nyingi kwa sababu watu wanajadiliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tukifunga mifumo kwenye maeneo mengi kutatusaidia sana kwenye kusimamia fedha na kukusanya mapato mengi ili Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa Waziri wa uwekezaji tuweze…

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kingu.

**TAARIFA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji Kaka yangu Festo, Mbunge makini kabisa. Hospitali ya Taifa ya Bugando kabla ya kufungiwa mifumo

ilikuwa inakusanya shilingi milioni 800 baada ya kufungiwa mfumo wanakusanya shilingi bilioni 3.5. Mifumo hii imefungwa na kampuni ya vijana wa Kitanzania wazalendo, Mheshimiwa Ummy Waziri wa Afya ni shahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya *KCMC* kabla ya kufungiwa mifumo ilikuwa inakusanya *only* shilingi milioni 300, 400 na baada ya kufungiwa mfumo wanakusanya mpaka 1.5 *billion*. Hospitali ya Amana ya Serikali, haya nayasema Mheshimiwa Waziri wa Afya yupo hapa kama nasema uwongo atasimama kunikanusha. Kabla ya mifumo walikuwa wanakusanya milioni tisa, leo tunazungumza baada ya kufungiwa mifumo tena mifumo imebuniwa na vijana wazalendo wa Kitanzania, wapo hapa lakini bado kigugumizi pia cha kuwatumia vijana hawa ni kikubwa. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Festo, kwamba watu wanakataa mifumo kwa sababu ya *corruption* na wizi wa fedha za Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Festo Sanga, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa hii kwa sababu ninatambua anachokizungumza ni sawasawa na kile ambacho nilikuwa nakizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda Morogoro kituo cha mabasi wana zaidi ya miaka mitatu wanahangaika kuvutana kwenye Baraza la Madiwani jinsi ya kufunga mfumo, kwa sababu pale *junction* ya mabasi mengi lakini watu hawataki, wanataka waendelee kutumia *cash*, fedha mbichi kuliko kutumia mifumo. Kwa hiyo ni kweli Serikali inachangamoto ya ufungaji wa mifumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la ulipaji wa kodi. Serikali, kwanza lazima tutambue wafanya biashara nchini ni sekta binafsi, Serikali haifanyi biashara. Kama mtu anafanya sekta binafsi, kuna siku anaweza akaamua aamke aende ofisini au asiamke kwenda ofisini. Kwa hiyo, unapoenda kudai kodi lazima tuwe na lugha ya *customer care*, lugha nzuri, lugha yenye kumshawishi mtu alipe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwigulu, kwenye kitabu chake cha bajeti anasema; "Mheshimiwa Spika, katika kutatua kero hizo napendekeza kuanza matumizi ya mfumo wa pamoja wa ukusanyaji wa ada, tozo na adhabu za taasisi, udhibiti, '*single window payment system* na taasisi za udhibiti kuweka utaratibu mzuri wa ukaguzi ambao hautasababisha usumbufu kwa wafanyabiashara bila kuathiri majukumu ya msingi ya taasisi hizo napendekeza hatua hizo zianze kufanyika mwaka 2023/2024". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi ambao Mheshimiwa Mwigulu, tunakufahamu hili limekuwa ni moja kati ya maono yako ya muda mrefu. Leo Mheshimiwa Mwigulu, ukienda kwa mfanyabiashara, watu wa leseni asubuhi wameingia dukani, watu wa *OSHA* asubuhi wameingia dukani, watu wa *fire* asubuhi wameingia dukani, watu wa *TRA* asubuhi wameingia dukani, watu wa *service levy* asubuhi wameingia dukani! Hatuwezi kuwa na Taifa la walipa kodi wa aina hiyo ambao wanafanya kazi ya kupokea wataalam wa Serikali kila asubuhi kuliko kupokea wateja wanaokuja kununua bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya Serikali lazima iwe ni jinsi gani ya kuisaidia sekta binafsi ya wafanyabiashara ifanye biashara katika mazingira mazuri. Kuliko hiki cha kuruhusu asubuhi watu wanaacha kazi maofisini wanapanga foleni kwenye maduka ya watu, kiasi kwamba kuna Watanzania wengi wamekufa mioyo kufungua maduka kwa sababu ya mifumo hii ya ufanyaji biashara. Ndiyo maana mataifa yanayotuzunguka Zambia, wameweka mazingira mazuri, watu wanakimbilia Zambia. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ili upate kodi kwa Watanzania tengeneza kwanza wafanya biashara wawe marafiki wa *TRA*, fanya *reformation* kule *TRA*, *reform TRA* yote jinsi gani inavyo-*operate* na wafanya biashara. Tatu, kwa nini leo mfanyabiashara ukienda kununua mzigo anakwambia mimi nakukatia risiti ya shilingi milioni moja, huu mzigo wa Shilingi milioni 10 sitaki kukukatia risiti ya shilingi milioni 10, kwa nini wanakwepa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuende *far* kwa wataalam wetu kufikiria kwanini wafanya biashara hawopo tayari kukatia

risiti ya milioni 10, wapo tayari kudanganya watoe risiti ya milioni moja. Wafanyabiashara lazima wataalam wetu wawaze mbali ili kuweza kukusanya hizo fedha za ku-*finance* huu mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu zisije zikaisha niende kwenye Sekta ya Utalii. Mheshimiwa Rais, juzi alizungumza kuhusu utalii. Kwanza ni *support* kwamba utalii wetu unaongezeka, unakua kutokana na jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais, aliondoa mguu wake ofisini na akaenda *site* kwenda kutengeneza *The Royal Tour*, ambayo leo kila mmoja na Wizara inajinasibu kwamba utalii umekua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu linabaki kwenye sekta hii, utalii kwa asilimia 90 inafanya kazi sekta binafsi. Mtalii akishuka *Airport* anakutana na dereva, mtalii akienda *site* kwa maana kwenye hifadhi atakutana na dereva na *tour guides*. Leo hii wizara inampango gani wa kukutana na *drivers*, kukutana na *tour guides* kukutana na hao wote ambao ni mnyororo wa thamani kwenye utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtalii anayetoka nje akija Tanzania ana uwezo wa kutumia masaa arobaini, katika masaa arobaini, masaa thelathini anakuwa kati ya yeye na dereva au na *tour guides*. *Tour guides* tumewapa *level* gani ya ubalozi wa kuelimisha kuhusu utalii? Kumekuwa na changamoto kubwa sana kwenye sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba dakika mbili nimalizie. Ukija kwenye suala lingine, Mheshimiwa Rais amezungumza, Serikali inatakiwa iwe na mpango, kuna changamoto ya malazi kwenye sekta yetu ya utalii, malazi imekuwa ni changamoto ya watu kwa kulala. Ukienda Serikali ilishawahi kuwa na *lodge* na hoteli 23, leo hii nataka nikuambie katika mchakato ambao Serikali inaufanya, hoteli hizo zimekufa, hoteli hizo hazifanyi kazi. Nakupa tu mfano mmoja hapa nazungumza. Mfano katikati ya Jiji la Dar es Salaam, *premium area* kuna hoteli inaitwa *Embassy Hotel*, kwa muda wa miaka 14 haieleweki ni ya Serikali, haieleweki ni ya uwekezaji, lakini Taifa letu linachangamoto kubwa ya kutokuwa na hoteli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoteli ya Ngorongoro, kuna hoteli ya *Seronera Wildlife, Lobo Wildlife*, *TRA* wanasema hawajui hizi hoteli zinamilikiwa na nani. Mheshimiwa Rais, anazungumza kwamba Taifa letu lina changamoto ya maeneo ya malazi, lakini hoteli hizi ni za Serikali zipo kwenye *potential area,* kuna haja ya Serikali kuwa na mpango mahsusi kuufanya utalii ukue, kuufanya utalii uonekane. Tunazungukwa na Rwanda na Mataifa mengine yanafanya vizuri, hata juzi tulijiuliza tupo kwenye kufungua michuano ya kimataifa ndani la Taifa letu ambalo tunajinasibu kutangaza utalii lakini tunatangaza *visit* nchi nyingine wakati sisi tulikuwa na uwezo wa kufanya matukio makubwa kwa ajili ya Taifa hili. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, ajiandae.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi nichangie hoja ya mpango iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wezangu kuendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri sana anayoifanya yakutuletea maendeleo watanzania. Kuna ule usemi wa Kiswahili unaosema kwamba, mwenye macho haambiwi tazama, kwa sababu tunaona maendeleo ambayo anatuletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia vipaumbele viwili ambavyo ni kukuza uwekezaji na biashara, lakini sambamaba na hilo nitazungumzia kuchochea maendeleo ya watu. Sina shaka kabisa kwamba Serikali yetu inafanya kazi kubwa sana katika kuleta maendeleo ya wananchi, sambamba na hilo Serikali yetu ina nia ya dhati kabisa kuwawekea mazingira wezeshi wafanyabiashara ndogo ndogo wakiwemo wamachinga, wakiwemo boda boda, waendesha bajaji, kina mama ntilie na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi hili ni kundi kubwa sana ambalo kama litatumika zile kodi zake vizuri, zikakusanywa vizuri, mwisho wa siku Serikali itapata tija kubwa sana kutokana na kundi hili na mwisho wa siku tuweze kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba hebu utafutwe mfumo mzuri wa kuona namna bora ya kuweza kufanya makusanyo katika kundi hili ili kuepuka ile mianya kwa baadhi ya Watendaji wachache ambao wamekuwa wakitumia fursa vibaya kwa kuyapindisha haya makusanyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kuzungumzia ni hili ambalo lipo kwenye shabaha ya mpango ambayo shabaha hiyo ni kuzalisha ajira kwa wingi ambayo ni pamoja na upatikanaji wa mikopo ya riba nafuu na mikopo isiyokuwa na riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuipongeza sana Serikali kwa kuwa na mazingira ya kuhakikisha kwamba kundi hili la vijana wanapata mikopo iwe yenye riba nafuu au mikopo ambayo haina riba. Tukiangalia katika zile asilimia 10 ni kwamba hakuna riba yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nikumbushe kwamba kuna ile mikopo ya maendeleo ya vijana ambayo inatolewa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Mikopo hii kwa kweli ikiwekwa kwa umuhimu mkubwa sana na vijana wengi sana wakapata mikopo hii, naamini kabisa hili suala la kusema kwamba tunahitaji kukuza ajira, kweli linaweza likafanikiwa, kwa sababu vijana wengi sana wakipata mikopo mwisho wa siku wataweza kufanya kazi na wataweza kujitegemea. Wakiweza kujitegemea, maana yake ni kwamba hata suala la tabia zisizokuwa na maana zitapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kumekuwa na matukio, watu wamekuwa na *stress* hasa vijana, wengine kufanya mambo yasiyofaa, wengine kujiua na kuchukua maamuzi mengine ambayo hayafanani. Kwa hiyo, naamini kabisa kuwa iwapo kundi hili likipata mikopo ya kutosha, basi

suala la ajira litawezekana na hatimaye tutaleta maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusiana na suala la kuchochea maendeleo ya watu. Nafahamu kabisa kwamba suala la kuchochea maendeleo ya watu ni pamoja na suala la elimu, suala la afya, suala la maji, sambamba na hilo suala la ustawi na maendeleo ya jamii. Suala hili ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niishauri Serikali katika mpango huu, kwamba suala la malezi na makuzi nalo linabidi liwekewe mipango ya uhakika na bajeti ya kutosha ili kuweza kunusuru hiki kizazi kilichopo. Nasema hivyo kwa sababu gani? Natamani Serikali izingatie ule mpango wa kuwezesha malezi na makuzi ambao uliandaliwa na Serikali mwaka 2021/2022 ambao unaendelea hadi 2025/2026. Iwapo mpango huu utahusishwa vizuri na ukaweza kujenga vituo vya huduma mbalimbali vya malezi na makuzi, itawawezesha wanawake wengi kuwapeleka watoto wao katika maeneo yale na mwisho wa siku wanawake hawa wataweza kufanya shughuli zao za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiona akina mama mbalimbali wamekuwa wakitembea na watoto migongoni, wamebeba mabeseni vichwani, wanafanya kazi, wanatembea na wale watoto juani. Kwa hiyo, inawezekana kabisa afya za watoto hawa zinaweza zikapata madhara. Kwa hiyo, nilikuwa naomba niishauri Serikali kwamba kwenye suala zima la malezi na makuzi na kujenga hizi nyumba salama ni jambo jema ili kuwanusuru watoto wa kizazi hiki na mwisho wa siku akina mama waweze kufanya kazi zao bila kuwa na mashaka yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa natamani kulizungumzia ni suala zima la mmomonyoko wa maadili. Hili ni tatizo kubwa, tumekuwa tukipata matukio mbalimbali kila kunapokucha. Hili suala na mmomonyoko wa maadili, iwapo kutaimarishwa huduma ya ustawi wa jamii; kwa taarifa zilizopo ni kwamba wanataaluma wa ustawi wa jamii walioajiriwa ni wachache sana, ni kama 4%. Kwa hiyo, nilikuwa natamani katika mpango huu Serikali ingeweza kuona umuhimu

wa kuweza kuweka mpango wa muda mrefu kuhakikisha kwamba Maafisa Ustawi wa Jamii wanaajiriwa kwa wingi ili kusudi kuweza kuiponya mioyo pamoja na akili za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna matukio mengi sana ambayo yamekuwa yakitokea, watu kujiua, watu kufanya ukatili, kufanya mambo ambayo hayaeleweki, lakini yote hii inawezekana kabisa inatokana na ukosefu wa kupata ile huduma ya ustawi wa jamii. Kwa hiyo, nilikuwa naomba katika mpango huu pia, jambo hili wangeweza wakalitilia maanani ili kusudi tuweze kuwaponya hawa vijana wetu na jamii kwa ujumla, kwa sababu Maafisa Ustawi wa Jamii wanahitajika sana katika nchi hii kwa ajili ya kuleta faraja kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitamani nizungumze ni kwamba naungana sana na ushauri wa Kamati, pale ambapo Kamati ilibainisha kwamba Wizara, Idara, Mamlaka na Taasisi za Umma kutoshirikiana wakati wa kutekeleza baadhi ya miradi, hivyo kufanya ufanisi uwe hafifu au kuwa chini ya kiwango. Nataka nitoe mfano. Katika ujenzi wa zile Ofisi za Machinga ambazo zinatakiwa zijengwe kila mkoa, zilizopo chini TAMISEMI, pesa zimeshapelekwa kule, malekezo yote yameshapelekwa kule, Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake na Watoto wao ndio wanaoratibu shughuli ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo linakuja kwamba pesa zipo kule lakini baadhi ya mikoa hawajajenga zile Ofisi. Sasa kama kukiwa kuna utaratibu mzuri kwamba Wizara hiyo hiyo inapewa fursa ya kusimamia hilo jambo, pesa zikakaenda kule na usimamizi ukaenda kule, naamini kabisa ufanisi unaweza ukapatikana. Kwa sababu, kama Wizara tatu au nne zikiwa zinashughulikia jambo hilo kwa kweli ufanisi wake unakuwa ni hafifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba kama itawezekana katika mpango huu basi hebu Serikali ione kwamba Wizara moja iweze kusimamia na kuleta ufanisi wa jambo fulani badala ya Wizara zaidi ya moja au tatu au nne, hiyo inaweza ikasababisha ufanisi usiweze kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kushukuru sana. Yangu yalikuwa ni hayo. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Sana Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq. Mheshimiwa Joseph George Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi na Mheshimiwa Juma Hamad Omar, ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami nianze na pongezi, kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha uanzishwaji wa Tume ya Mipango chini ya Ofisi yake. Pili, uwasilishwaji uliofanywa na Mawaziri; Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha, umekuwa mzuri na wenye weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango yaliyowasilishwa yamezingatia mambo mawili muhimu. Kwanza, yamezingatia hali ya uchumi wa dunia ambayo imeanza kuimarika kwa sasa hivi baada ya janga la UVIKO; vile vile, yamezingatia hali inayoridhisha ambayo tunaendelea nayo hapa nchini (hali ya ukuaji wa uchumi wa Taifa), ambayo imekuwa bora zaidi hata kuzidi baadhi ya mataifa jirani. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anajiandaa kuwasililisha vipaumbele, Waziri amezungumzia pia mambo mawili makuu. Jambo la kwanza amezungumzia ni shabaha kuu, akasema shabaha kuu ni kuchochea uchumi jumuishi unaolenga kupunguza umaskini, kuzalisha ajira, kutengeneza utajiri na kuongeza mauzo ya bidhaa nje ambazo zimeongezewa thamani. Jambo la pili, akazungumzia msukumo ili kufikia mafanikio hayo yanayolengwa, kwamba msukumo utakuwa ni kuongeza tija ya uzalishaji, kuongeza thamani ya ambazo kabla hayajauzwa nje, ambayo hii ni kazi ya sekta binafsi. Hayo ni mambo mawili. Halafu jambo la tatu akasema ni kuongeza uwekezaji wa Serikali kwenye sekta za elimu, TEHAMA na huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na shabaha, lakini nauona msukumo kama umezingatia *supply side* zaidi kuliko

kuzingatia *demand side*. Tungeweza kujenga vizuri msukumo na hivyo kujenga msingi wa vipaumbele kwa kuangalia *demand side*. Kama tunalenga kuchochea uwekezaji, lazima tujiulize maswali kama matano hivi. Wawekezaji wanahitaji nini? Kwenye maeneo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nilijaribu kujiuliza kwa niaba ya Serikali; swali la kwanza, wawekezaji wanahitaji nini? Nikajipa majibu kama matano hivi. La kwanza, nikapata kwamba wawekezaji wanahitaji kuwe na gharama nafuu kwenye sekta ya usafiri na usafirishaji. Kusafirisha nini? Kusafirisha malighafi kutoka zinakozalishwa, kuja viwandani na baadaye kusafirisha bidhaa kutoka viwandani kwenda kwenye soko. Wanahitaji gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama wanahitaji gharama nafuu, Serikali ijielekeze kuwekeza wapi? Lazima ijielekeze kuwekeza kwenye sekta za miundombinu zinazohudumia usafiri na usafirishaji. Kwa hiyo, hicho nikakipa kipaumbele cha kwanza. Lazima Serikali iendelee kuwekeza kwenye Barabara zinazopitika katika kipindi chote cha mwaka, lazima Serikali iendelee kuwekeza kwenye bandari na bandari zetu za Dar es Salaam, Bagamoyo, Tanga, Mtwara, Bandari za Maziwa kama Mwanza, Kigoma na kadhalika. Vile vile, viwanja vya ndege, madaraja makubwa, vivuko na mawasiliano (TEHAMA). Kwa hiyo, ni kipaumbele cha kwanza ni miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wawekezaji wanahitaji kuwe na gharama nafuu za uendeshaji wa mitambo inayotumika kwenye uzalishaji, usafiri na usafirishaji. Kwa hiyo, Serikali kama kipaumbele cha pili lazima iendelee kuwekeza kwenye sekta ya nishati. Vyanzo vya uzalishaji wa umeme, mitambo ya kupooza umeme na kuimarisha njia za usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye hili ni kuimarisha uthibiti wa bidhaa za mafuta tangu zinapoagizwa kutoka nje mpaka zinaposambazwa hapa nchini. Vilevile, ni muhimu sana kuendeleza utafiti wa mafuta. Kwa hiyo, hivyo ni vipaumbele ndani ya vipaumbele. Tatu, kuendeleza miradi ya

kuzalisha miradi ya kuzalisha na kusambaza gesi asilia. Kwa hiyo, kipaombele cha pili kilikuwa ni nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha tatu kutokana na swali, wawekezaji wanahitaji upatikanaji wa uhakika wa malighafi wanazohitaji viwandani muda wote wa mwaka. Viwanda vingi wawekezaji wana kilio, hasa viwanda vya kuzalisha mafuta hata alizet; unakuta *supply* ya alizeti inapatikana viwandani kwa muda wa miezi mitatu au minne. Kwa hiyo, viwanda vinakuwa vinasimama miezi saba, miezi nane havizalishi. Kwa hiyo, kunahitaji msukumo wa Serikali kuwekeza kuisaidia sekta ya kilimo kuzalisha zaidi malighafi viwandani. Sasa hii ingekuwa ni kipaumbele cha tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha nne, wawekezaji wanahitaji upatikanaji wa nguvu kazi nyingi na ya kutosha na ya gharama nafuu. Kuna baadhi ya viwanda hapa nchini vinalazimika lazima kuajiri watu kutoka nje kwa ajili ya viwanda vyao. Kwa mfano, viwanda vya sekta ya Ngozi na viwanda vya sekta ya maziwa. Ukienda *VETA* yoyote ile hakuna watalamu wanazalishwa pale. Hamna! Kwa hiyo, lazima sekta ya elimu, tunaipa maua yake kwa kuwekeza kwenye *VETA* kila mkoa, *VETA* kila wilaya lakini lazima waangalie mitaala, ni watu gani wanazalishwa ili waende wakatumike kwenye sekta za uzalishaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine, wawekezaji wanahitaji huduma za Serikali. Kwa hiyo, lazima Serikali iendelee kuwekeza kwenye huduma za afya ili wafanyakazi kwenye sekta wanakoajiriwa wawe na afya nzuri. Serikali lazima iendelee kuwekeza kwenye huduma za maji, ulinzi na usalama na huduma nyingine. Kwa hiyo, hicho kingekuwa kipaumbele cha tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili vipaumbele vyote hivyo vitekelezwe vizuri, lazima kama nchi kuwe na mfuatano *(sequencing)* ambao unazingatia mahitaji ya hali halisi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua hiyo ni kengele ya kwanza hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Serikali izingatie mahitaji ya sasa. Nimejaribu sana kupitia mifano. Kwa mfano tuna shehena kubwa sana ya chuma kule Liganga imelala chini, hatujaanza hata kuitumia, lakini ni mwaka uliopita 2022 Serikali imewekeza kujenga *foundry* ya kuyeyusha chuma katika Kiwanda cha *KMTC* kule Moshi. Kwanza tu hata ujenzi wa *KMTC* kule Moshi na ujenzi wa Mang'ula yote yalikuwa ni makosa. Kama Mang'ula na *KMTC* ingejengwa kiwanda kimoja tu maeneo ya Iringa au Njombe, ina maana tungetoa chuma pale chini tukakiyeyusha tukatengeneza *pulley* kule kule kwenye eneo la kupatikana chuma badala ya chuma kipatikane Mchuchuma na Liganga halafu usafirishe kilomita 800 kwenda kuyeyusha kule *KMTC* ni uwekezaji ambao hauna tija katika nchi. Ni muhimu sana kuangalia mambo kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili, miaka ya 1970, Serikali ilianzisha Mashirika kama *TIRDO, TEMDO* na *SIDO*. Lengo kubwa lilikuwa ni kusaidia uendeshaji wa viwanda vya Serikali wakati huo ambavyo vyote tumeshaviuza. Hivi kwa nini haifanyiki tathmini ya mahitaji ya mashirika hayo? Je, katika mazingira ya sasa yatakuwaje na tija katika uchumi wa nchi? Sijaona kwenye mpango, lakini nilikuwa nafikiri kwamba kuna baadhi ya mashirika yanahitaji kuunganishwa na kuna baadhi ya Mashirika yanahitaji kujiunda upya. Kuna baadhi ya Mashirika yanahitaji kufa ili kuweza ku-*fit* kwenye mazingira ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa ujumla naunga mkono Mpango, isipokuwa tu maboresho hayo machache yafanyike. Sina matatizo na malengo ya ukuaji wa uchumi, ni mazuri, malengo ya Mpango ni mazuri, nguvo kumi za utekelezaji ni nzuri, tuboreshe mpangilio wa vipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kakunda. Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, atafuatiwa na

Mheshimiwa Juma Hamad Omar na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kutuwezesha kuwepo hapa. Kwa nafasi ya pekee niwapongeze wawasilishaji wa taarifa zote mbili, ni taarifa nzuri na mpango ni mzuri. Nami mapema kabisa nitamke kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu kama ulivyosomwa inaonesha namna gani kiuchumi tunaenda vizuri. Kwa mujibu wa taarifa hii, kwa taarifa iliyotolewa na Benki ya Dunia mwezi Septemba, kwa miaka mitatu mfululizo uchumi wetu kama Taifa umeendele kukua. Achilia mbali kwamba kidunia uchumi umekuwa unapungua lakini kwetu imekuwa kwa asilimia kadhaa uchumi unaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matarajio kwamba mwakani uchumi utaendelea kuongezeka. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa sababu pamoja na changamoto kadhaa, kwa miaka takribani minne mitano mfululizo ame-*stabilize* hali na uchumi wetu umeendelea kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukua kwa uchumi, kimaandishi uchumi wetu unakua, ni lazima sasa tutakafari zaidi je, hali ya watu wetu inaendana na kukua kwa uchumi huu katika maandishi (katika tarakimu)? Ni lazima tuone je, kuna uwiano? Kwenye mpango kama ulivyosomwa na Mheshimiwa Waziri, kuna mabadiliko makubwa yamefanyika kwenye hali ya kiuchumi ya watu wetu na hili limetokea kwa sababu ya uwekezaji uliofanyika kwenye sekta za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tufanye vizuri zaidi na ili tufikie athari chanja kwenye eneo hili, ni lazima uwekezaji zaidi uwe kwenye maendeleo ya watu, hasa kwenye eneo la kijamii na kwenye maeneo ya kiuchumi hasa tukiweka mkazo kwenye maeneo ya vijijini. Ni lazima tuimarishe uwezo wa uzalishaiji kwenye sekta muhimu kama kilimo, uvuvi na nyinginezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili nimekuwa najiuliza, tuna rasilimali nyingi sana kama Taifa, lakini kwa mtazamo wangu, bado hatujaweza kuzitumia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna rasilimali maji ambayo tungeweza kuitumia kwa ubora zaidi na kwa ufanisi kufanya kilimo cha umwagiliaji kuwa msingi wa Uchumi wa Taifa letu. Bado pamoja na jitahada kubwa sana zinazofanywa na Serikali ninatambua mwaka jana tumeongeza bajeti kwenye Wizara ya Kilimo, Wizara ya Kilimo inafanya kazi kubwa sana kujaribu kufufua kilimo kwenye nchi hii. Tunahitaji tufanye zaidi ya hapo tuweze kutumia rasilimali tulizonazo kama maji, tuweze kuitumia vizuri ili kukuza kilimo chetu vilevile kufanya wakulima wetu waweze kunufaika na rasilimali hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa ninatafakari eneo kama Ukerewe ambako tunazungukwa na maji. Katika eneo la *square* kilometa karibu 6,400 zaidi ya asilimia 90 ni maji. Tuna eneo pale, ni kwa nini Ukerewe watu walalamike kukosa chakula, kuwa na upungufu wa chakula kila mwaka? Ni kwanini, tusiwekeze kwenye umwagiliaji kwa kutumia rasilimali maji yaliyopo kwenye eneo hili kufanya kilimo cha umwagiliaji, kutumia eneo dogo lililopo kwa ufanisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sehemu moja lakini kuna maeneo mengi ambayo kwa rasilimali tulizonazo tunaweza tukatumia vizuri tukaweza kuwekeza tukafanya watu wetu kwenye maeneo yaliyopo kule chini kuweza kutumia rasilimali hizo kujiimarisha kiuchumi. Niombe kama nilivyotoa mfano kwenye eneo la Ukerewe pamoja na maeneo mengine, tutumie rasilimali hizi kwa ufanisi ili kuweza kufanya watu wetu kule chini wawe imara kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwenye kilimo hata kwenye uvuvi bado kama alivyokuwa anachangia Mheshimiwa Sanga bado kuna vikwazo vingi sana kwa watu wetu kule chini wanapokuwa wanafanya biashara lakini wanapokuwa wanafanya shughuli za uzalishaji vilevile. Sekta ya uvuvi ni sekta muhimu sana kwenye Taifa hili katika kuimarisha uchumi wetu, wavuvi wetu wanakutana na vikwazo vingi sana vya tozo

mbalimbali. Kwa mfano, leo kwenye maeneo ya kanda ya ziwa kuna kitu kinaitwa tozo ya *control* namba na kadhalika ni kikwazo kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ningeshauri kupitia Wizara ya Uvuvi, ondoeni tozo hii. Inaleta kero kubwa, inaathiri uzalishaji kwa wavuvi wetu kwenye maeneo yale jambo ambalo kiujumla linaathiri uchumi wa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyotajwa kwenye mpango, tukiwekeza kwenye huduma za kijamii, uchumi wetu utaendelea kukuwa kwa kiwango kikubwa sana. Na hili ndiyo maana nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji mkubwa sana alioufanya kwenye Sekta ya Huduma za Kijamii, kwenye elimu, afya, kwenye maji, kazi kubwa imefanyika hata miundombinu na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna maeneo ambayo miundombinu yetu hasa ya usafirishaji kuna changamoto kubwa sana. Niki-*sight* kwa mfano eneo la Ukerewe, kwenye ilani yetu ya uchaguzi ili kurahisisha mazingira ya watu wetu, kufanya waimarishe uchumi wao kupitia sekta ya usafirishaji, Ilani ilielekeza kujenga vivuko kwa ajili ya kusaidia wananchi wetu kusafiri kutoka eneo moja kwenda eneo jingine kusafirisha mazao yao. Leo eneo kama la Ihugwa kisiwa cha Ilugwa pale Ukerewe, mwananchi anasafiri masaa matano eneo ambalo angeweza kusafiri kwa nusu saa kwa sababu tu mazingira ya usafiri kwenye eneo lile sio bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilani imeelekeza vivuko vitengenezwe kwenye eneo lile. Niombe Wizara zinazohusika katika mpango wa bajeti unaokuja, pesa kwa ajili ya kuelekeza kwenye eneo hili kukamilisha miradi hii iweze kutengwa na iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kitila katika hotuba yake ameelezea kwamba katika nguzo zinazoshikilia mafanikio ya utekelezaji wa mipango yetu, moja ni kuwa na nidhamu ya utekelezaji wa mambo tunayoyapanga. Wakati Mheshimiwa Sanga anachangia hapa, ameelezea namna ambavyo ni

muhimu sana kuwekeza kwenye mifumo ya kiteknolojia (Mifumo ya *TEHAMA*), lakini mifumo hii hata kama tutaifunga, kama hakutakuwa na ufuatiliaji na tathmini ya namna gani mifumo hii inafanya kazi bado hatutakuwa na mafanikio katika mifumo hii hata kama tutaiweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita tulikuwa tunajidili Ripoti ya *CAG*. Mambo mengi sana, miradi mingi inakwama kwenye utekelezaji kwa sababu hakuna mfumo wa tathimini na ufuatiliaji. Ndiyo maana niombe Mheshimiwa Kitila, bado kama nilivyosema wiki iliyopita ni muhimu sana tuwe na sera ya kitaifa ya ufuatiliaji na tathmini ili mipango yote hii tunayoipanga tuhakikishe kwamba kweli inatekelezwa kwa namna ambavyo tumedhamiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, tukiwa na *national policy* ya *monitoring and evolution* itasaidia kwanza kuongeza uwajibikaji, itasaidia miradi yetu kufanyika katika kiwango bora na thamani ya pesa tuliyowekeza kwenye miradi ile kuonekana. Itaongeza uwazi kwa sababu kutakuwa na ufuatiliaji lakini kutakuwa na tathmini itakayokuwa inafanyika, kutakuwa na ujumuishaji wakati wa utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, achilia mbali hiyo bado maadili ya watumishi wetu katika kusimamia na kutenda kwenye usimamizi wa miradi hii utaongezeka jambo ambalo litasaidia rasilimali pesa tunazozitomia kuwekeza kwenye miradi mingi ya maendeleo, tathmini yake ikifanyika inakuwa na tija na inakuwa na maslahi kwa Taifa letu. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Kitila katika *plan* zako zote ulizonazo, bado kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na *national policy* ya *monitoring and evolution* ili kuhakikisha rasilimali pesa tunazowekeza kwenye miradi yetu ya maendeleo inafanyika kwa tija na yale tunayotarajia kwa maslahi ya maendeleo ya Taifa letu yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nilitaka niuweke kwenye eneo hilo. Ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Mkundi. Nimemtaja Mheshimiwa Juma Hamad Omar atafuatiwa na

Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni ajiandae. Waheshimiwa kabla ya Mheshimiwa Hamad samahani kuna Tangazo la Wageni waliopo Bungeni muda huu.

Tunao wageni 38 wa Mheshimiwa Anna Lupembe (Mbunge) ambao ni wanamaombi kutoka Jiji la Dodoma. Ahsante karibuni sana.

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Patrobass Paschal Katambi (Mbunge) ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu ambao ni wastaafu wa *NSSF* kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini. Karibuni sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Juma Hamad Omar, karibu.

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, tulipata nafasi ya kuchakata wasilisho zote hizi na kwa kweli tunakubaliana nao. Nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais anayeshushulikia masuala ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wasilisho la Profesa Mkumba, Profesa Kitila Mkumbo. Mjina magumu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Hamad anaitwa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo. Naomba endelea na mchango wako.

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa samahani kwa kukosea jina hilo. Ni wasilisho zuri sana limetupa hali ya uchumi, matarajio yetu na huko tunakokwenda. Ninasema tuna mtu ambaye alikuwa *very brilliant* katika mambo haya ya uchumi. *Congrats Prof*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu *as usual,* ni very *ductile* wakati wote amekuwa akikubaliana na hoja kwa hiyo amekuwa *very ductile* anakubaliana na hoja na ninafikiri tunafika mahala Kamati ya Bajeti tunamwelewa tu. Tunafika mahala tunakwenda vizuri na yeye. Kubwa zaidi nimpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuunda Tume ya Mipango, kwa kweli kama kuna jambo amelifanya na litatutoa hapa tulipo kwenda kwenye uchumi mwingine ni hilo. Sasa kwa maoni yangu, ili uweze kufanikiwa, ili nchi iweze kufanikiwa kiuchumi kuna mambo kadhaa lazima uyatekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza iwe na sera sahihi za kifedha *prudent, physical and monetary policies.* Pili iwe na sera sahihi za kiuchumi lakini ikishirikisha watu binafsi au kampuni *(Private public participation),* la tatu iwe na *prudent taxation policies* na bila kuwa na *prudent taxation policies* utakuta kodi unayokusanya hasa kwa wakati wetu huu sasa ambao ndiyo wa mitandao wa *TEHAMA* unaweza ukakuta kwamba kodi ni ndogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne uwe na wafanyakazi ambao ni bora na ninafikiri katika mwisho wa hotuba ya profesa Mkumbo amesema kwamba *prime minister* wa Singapore alifanikiwa kwa kuwa na wataalam na wafanyakazi ambao wana uwezo wa kufanya kazi. Katika kuona hii hali halisi nasema yote haya manne lakini yawe chini ya *umbrella* ya *good governance*. *Without good governance* yote haya hayawezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikitoa mfano wa *tiger economies* ambazo zipo Asia na nikisema *tiger economics* nakusudia *economy* za nchi nne. Ambazo ni Singapore, Hong Kong, South Korea na Taiwan. Hizi nchi wakati tunapata uhuru miaka ya *1960's* zilikuwa na uchumi kama zetu. Baada ya kufanya *major industrialization* kwanzia Miaka ya 1950's wali-*invest* sana katika *industries* na kwa kutumia watu wao ambao walikuwa ni bora sasa hivi kwa kweli ni nchi ambazo ni za kupigiwa mfano ulimwenguni. Kwa kweli ni *more than first one*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano *GDP per capital* ya Singapore sasa hivi kama sikosei imefikia dolla 67,359. Nichi ya pili inafuatia Taiwan, *GDP* kwa miaka 2020/2022 ilifikia 61,371. Hong Kong, *GDP per capital* ni 49,000 na mwisho South Korea *GDP per capital* ni dolla 48,309, wakati sasa hivi katika Africa nchi yenye *GDP* kubwa ni Mauritius ambayo nafikiri kama sikosei imefikia dolla 9,005. Inafuatiwa na Botwasa ambayo imefikia 6,610, kwetu sisi kama sikosei tunakaribia dolla 1,200 hivii, Kenya wenzetu wapo mbele kidogo kama 2,080.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hawa watu wamefanya kazi kubwa sana. Maendeleo yao ya kiuchumi ni makubwa na hii imetokana na kona zote hizi nne nilizosema lakini chini ya utawala bora wa kisheria. Sifa tumpe, wanasema mnyonge mnyongeni lakini sifa mpeni, tumpe mama yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana alipokuwa akichangia Mheshimiwa Reuben alisema mama ni kama vile alitutoa msituni, *it is very true*. Mama baada ya UVIKO ndiyo akaingia madarakani na alipokuja jambo la kwanza alilofanya ni ku-*negotiate* na *IMF* tukapata ule mkopo wa *COVID* ambao ni karibu shilingi trilioni 1 na bilioni 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kama hiyo haitoshi, ame-*negotiate* na *IMF* na *World Bank* tukapata ile *credit facility* ya shilingi trilioni 2.2 yaani trilioni mbili na bilioni 200. Kama hiyo haitoshi, akaenda akaweka trilioni moja za kuwasaidia wakulima ili wakulima waweze kupata mikopo. Sasa, mama kafanya mengi sana na anaendelea kufanya mengi. Kwa hiyo tumpe sifa kubwa, tumpe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Bajeti namba 11 ya mwaka 2015 ina kifungu ambacho huwa inataka ianzishwe fungu ya dharura. Kwa nini? Kwa sababu katika hizi tunasema vigezo tarajiwa, moja katika vigezo tarajiwa ni kwamba tutajitahidi kuhakikisha kuwa kuna utoshelevu wa chakula. Suala la pili, tutahakikisha tunahimili tabia ya nchi au tunashughulikia tabia ya nchi. Sasa hizi ni *unforeseen emergences* kama huna *contingency* hauwezi kuhimili vitu kama hivi ambavyo ni *unforeseen*. Sheria ya

Bajeti ya hiyo Na. 11 ya mwaka 2015 kifungu cha 35(1) mpaka cha (4) kinazugumzia uwepo wa kuwa na *contingency* lakini na *fund* au *sources* za *contingency* zitakuwa vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika Kifungu cha 36(1-3) kinampa uwezo Waziri wa Fedha ku-*administer* au kuishughulikia hili suala la fungu la *contingency*. Jambo hilo halijafanyika na mimi ninasema Waziri wa Fedha pamoja na mazuri yako yote lazima tufike mahala tuwe na *contingency* kwa ajili ya *unforeseen emergences* na sheria yenyewe inampa Waziri wa Fedha atenge asilimia tano ya *total budget* ambayo sidhani kama Mheshimiwa Dkt. Mwigulu umefanya hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua una fungu lako 21 lakini hili fungu la 21 ni fungu ambalo kuna mambo mengi. Kuna malipo ya wastaafu, majaji, sijui stahili za viongozi nakadhalika. Sasa tusichanganye mambo hayo na fungu la dharura. Fungu la dharura ni lazima liwepo kwa mujibu wa Sheria hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *private sector* ndiyo injini ya uchumi. Ninajua kwa mujibu wa takwimu tulizonazo, mikopo kwenda kwenye *private sector* imekuwa ikiongezeka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia mchango wako.

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mwaka 2021/2022 mikopo kwa sekta binafsi ilikuwa asilimia 9.9, iliongezeka katika 2022/2023 imekuwa 10.3 lakini hii ni sehemu ndogo sana. Pesa hizi nyingi zipo maana yake *private sector* huwa hawakopi benki, Benki Kuu huwa haikopeshi *private sector* inakopa kwenye Benki za Biashara. Benki za Biashara zinaendelea kupata faida kubwa sana mpaka zinafika mahala zinaanza kuuza hati fungani kama tulivyotamkiwa. Kwa sababu ukishafika mahala hapo kwamba unainyima *private sector* mkopo, kwa kweli utakuwa huwasaidii kuendeleza uchumi na tumesema *private sector* ndiyo injini ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu *private sector* wao wanapewa mkopo kutoka Benki Kuu na Benki Kuu wana *instrument* mbili*,* Moja, wanapunguza ile wanaita *SMR*

*(statutory minimum reserve),* na la pili wana *discount rate* ya *landing* wanayompa *private sector*. Sasa, kama Benki Kuu ndiyo anayefanya *bank supervision* ninashangaa kwa nini Benki Kuu hawasimamii hizi benki za biashara kuhakikisha kwamba nayo mikopo kwa *private sector* inakuwa na riba ndogo, sijui kama naeleweka hapo. Inakuwa na bei ndogo na vilevile kwa kiasi kikubwa zaidi ya asilimia 10.3 kama tunavyosema inakwenda kwa *private sector. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivi tutakuwa tumewasaidia priv*ate sector* na tutakuwa tumewachachua katika kujenga uchumi. La mwisho…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia sentensi mbili za mwisho.

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema hivi, tatizo si wigo wa kodi. Wigo wa kodi tunao wa kutosha maana ukienda ukiagiza kitu sijui lipa, *income tax,* sijui *VAT*. Wigo wa kodi ni mkubwa lakini *problem* kubwa ni kuwa *tax payers* tunaolipa kodi *we are talking of population of 61 million* lakini *tax payers* wanaolipa kodi ni *6.7 million.* Ndiyo kusema ni asilimia 4.5 tu ndiyo wanaolipa kodi katika *population* yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wenzetu wana tax payers around 2.5 *million* lakini *population* yao ni *around 19* kwa hiyo, *they are talking of 13.2%.* kwa hivyo tupo chini sana, wengi hatulipi kodi. Wengi ni watu tegemezi. Ukishafika hapo ndiyo unakuta mara nyingi mapato yanayotokana na kodi hayatoshi kuendesha Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Hamad Omar.

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Hamad Omar kwa mchango mzuri sana. Mheshimiwa Ng'wasi Damas

Kamani atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni ajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi ili nichangie kwenye mpango wetu huu wa mwaka 2024/2025. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya yeye pamoja na wasaidizi wake Mawaziri na Manaibu Waziri, wanafanya kazi nzuri na kubwa kuhakikisha kwamba maendeleo yanawafikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaongozwa na dira na mipango ya miaka tofauti tofauti. Kuna mipango ya miaka mitano, miaka kumi na tano, miaka 30 na mpaka miaka 60. Hii mipango ya mwaka mmoja mmoja ambayo tunajadili hapa kwenye Bunge kila mwaka ningependa niishauri Serikali walau iwe inangalia mambo current zaidi ili tuweze kuisaidia nchi yetu. Kwa nini nasema hivi, mwaka jana taifa letu limepitia mchakato wa Sensa ya Watu na Makazi iliyoongozwa kwa ushupavu mkubwa sana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya mwanzo ya Sensa hii ilitoka Oktoba, mwaka jana lakini mpaka sasa tunapozungumza *final report* bado haijatoka. Sasa tunazungumza mpango ambao ndiyo wa kwanza tangu tufanye Sensa hii. Sisi kama Wabunge, bila hii *final report* tunashauri vipi Serikali namna ya kuboresha mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ni muhimu hii mipango ya mwaka mmoja mmoja iangalie vitu *current*. Tumetumia zaidi ya bilioni 400 kufanya Sensa hii. Sasa, tija ya fedha hizi itaonekana kwa namna gani? Tunatumia ripoti hii kupanga mipango ya muda mfupi na muda mrefu ya nchi yetu. Naishauri Serikali iangalie namna *final report* ije ili Waheshimiwa Wabunge waishauri Serikali kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, kwenye Sensa hii tumeona kwamba kuna idadi ya watu kiasi gani, wanawake kwa wanaume kwa kila mkoa. Kuna mikoa yenye watu wengi na kuna

mikoa yenye watu wachache. Kwa mfano, Mkoa wa Njombe una watu kama laki nane na kitu tu. Kuna Mkoa wa Dar es Salaam ambao tunaongelea una watu zaidi ya milioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango lazima iende tofauti kwa sehemu na sehemu. Pia, ninavyosema tuongelee mipango *current*, namaanisha; siku Serikali nyingi tumeona, Rais wetu na wasaidizi wake wamesaini mkataba mzuri na mkubwa sana wa Bandari ambao unakwenda kufanya na kuleta mageuzi makubwa sana ya kiuchumi nchini kwetu. Hata hivyo bado mpango wetu haujaweza ku-*incorporate* zile *financial implications* ambazo zitaletwa na mkataba huu. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pia, kuna mikataba au miradi mikubwa sana ambayo inaendelea kwenye nchi yetu ambayo tunategemea ndani ya miaka hii 2024/2025 ikamilike na itakuwa na *financial implications* kubwa sana kwenye nchi yetu la. Mpango haujatuonyesha, naongelea kwa mfano, Bwawa la Mwalimu Nyerere, tumekuwa tukisubiri mradi huu kwa muda mrefu na tumepewa matumaini na Serikali yetu na niipongeze sana kwamba mradi huu unakwenda vizuri na unakwenda kukamilika. Faida za mradi huu na *financial implications* zake tuzione kwenye mipango yetu ili tuone namna gani tunasonga mbele kwanzia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Prof*. Kitila Mkumbo akiwa bado Mbunge alikuwa anazungumzia sana Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Sasa amekabidhiwa kijiti, ninashukuru na kumpongeza kwa sababu nimeona kwamba kwenye mpango wake anaona haja ya Serikali kuanza kufanyia kazi mradi huu. Nadhani kuna haja, tofauti na sentensi hii tu aende mbele zaidi kushauri kama alivyokuwa anashauri akiwa amekaa pale; kwamba ni namna gani anafikiri tuende sasa na mradi huu ili ulete tija kwenye taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ni mzuri sana lakini kwa bahati mbaya ninahisi, kaka yangu Mheshimiwa *Prof*. Kitila amewasahau vijana kwenye mpango huu. Kwa nini nasema hivi, nizungumzie suala la changamoto ya upatikanaji wa mitaji kwa vijana. Tukiwa tunazungumzia takwimu ambazo ziliietwa na

Wizara yetu ya Kilimo, ikiwa inaonyesha *justification* za Mradi wa *BBT;* ilionyesha kwamba vijana zaidi ya *16 million* kwenye nchi yetu, wanawake kwa wanaume wana changamoto ya kupatikana kwa mitaji. Yaani hawana *accessibility* ya *financial institutions* zile kubwa kwa maana ya mabenki na hizi ndogo ndogo kwa ajili ya kijipatia mitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru na kuiopongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu iliona haja na changamoto hii ikaleta mpango wa 4:4:2 au mikopo ya asilimia 10 kwenye halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu aliiona changamoto ambazo makundi haya maalum yanapitia kwenye halmashauri zetu na akatoa maelekezo ya mfuko huu. Hiki kitu kilifanyika Aprili mwaka huu, mpaka leo tunavyozungumza ni miezi saba na hakuna hatua ambayo tumeiona kwa macho ikifanyika kuonyesha kwamba kweli mfuko huu utarudishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema *Justice does not have only to be done. It should be seen to be done.* Serikali inatuambia kwamba inafanyia kazi mchakato huu. Ninakataa kuamini kwamba, mfuko huu tayari uko kisheria. Vyanzo vya fedha za mfuko huu zinajulikana lakini maelekezo ya Mheshimiwa Rais yalikuwa mahususi, fedha hizi zipitie kwenye benki. Haimaanishi tunaanzisha benki mpya ili tukae muda mrefu namna hii, ni benki hizi hizi tulizonazo. Ninakataa kuamini kwamba, Serikali hii yenye wataalam wengi wa kutosha wanaofikiri vizuri, wanahitaji zaidi ya mwaka mzima kuweza kuja na mpango huu kwa ajili ya vijana…

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** … lakini, kitendo cha kwamba mpango huu haujataja jambo hili unamaanisha kwamba vijana tusiwe na matumaini…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ng'wasi, samahani kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Festo Sanga.

**TAARIFA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye pendekezo la Mheshimiwa Rais kutumia benki, *in a records* taifa letu limewahi kutumia *DCB Bank* kwenye ya Dar es Salaam na kwenye *records* hawajawahi kuwa na upotevu wa fedha kwa kiwango ambacho sasa zimepotea. Kwa hiyo, Serikali ina *delay* lakini ina sehemu ya kwenda kujifunza *DCB Bank* na kuchukua hatua na kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ng'wasi, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hii na inazidi kuonyesha ni namna gani *it is unjustifiable* kwa Serikali kukaa muda mrefu namna hii bila kuleta utaratibu hii na vijana wakaendela kutumia fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema, kitendo cha Profesa Kitila kutoku-*incorporate* katika mpango wake namna gani fedha hizi zitaenda kurudi kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ina maanisha kwamba tuondoe matumaini katika kipindi hiki cha 2024/2025 kwamba mfuko huu utarudishwa na fedha hizi zitarudi kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani mpango huu Mheshimiwa Kitila unapokuja kutujibu katika mrejesho wako wa mwisho, utuambie namna gani fedha hizi zinakuja kwenda katika *channels* zinazotakiwa na ziwafikie walengwa. Mheshimiwa Kitila, kwa nini nasema hivi, vijana wanawake kwa wanaume, ndiyo *asset* kubwa na nzuri ya nchi yoyote ambayo inajielewa katika dunia hii. Ni kwa sababu vijana ndiyo tunategemea watakuja kuwa wazazi waliobora baadaye, walezi waliobora baadaye, viongozi waliobora baadaye lakini wafanya maamuzi katika taifa hili. Kama tusipoanza kuwawezesha leo, ninaamini tunatishia kesho zilizo salama za taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kusema kitendo cha kuchelewesha mikakati ya kuhakikisha vijana wanapata mitaji katika nchi hii kina *multiplying effects. Effect* ya kwanza ambayo

mimi ninaiona na *immediate* kabisa na imepigiwa kelele na baadhi ya watu ni *issue* ya *gambling,* tunaiita kamari. Vijana wengi sasa wameishia kwenye kucheza kamari. Na tafiti za msingi zimefanyika kwamba, Kamari iwe ni *online,* iwe ni hizi tunaita *sports betting* zote zina *implications* kwenye *psychology* ya kijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *implication* yake kiutafiti ni kwamba, mtu wa kawaida anatakiwa aonyeshwe namna gani anahitaji kukifanyia kazi kitu ambacho anataka kukipata. Hata maandiko yamesema asiyefaya kazi na asile. Lakini Kamari zinajaribu kumuonyesha kijana kwamba kuna njia nyepesi zaidi za kupata kitu kilichokikubwa zaidi. Changamoto ninayoiona hapa ni kwamba, tunaenda kuzalisha watu ambao wataona kwamba wana haja ya kuona namna ya kurahisisha mazingira yao ya kupata fedha. Mtu huyu ukimpeleka kwenye utumishi wa umma huwezi ukamwambia akae afanye kazi asubuhi mpaka jioni, siku saba, mwezi, miaka ili apate kitu fulani ilhali anaona kuna njia nyepesi ya kuweza kufanya ili apate kitu kilichokikubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naona kwa kuendelea kuchelewesha haya, *tuna-multiply effect* kubwa sana. Siyo ya leo tu ya vijana wetu lakini kesho ya taifa letu. Nadhani ni wakati sasa tuchukue hatua, tufanyie kazi shida ya upatikanaji wa mitaji kwa vijana pamoja na kupuunguza changamoto ya ajira. Tunajua kwamba Serikali haiwezi ikaajiri vijana wote lakini tukiwapatia mitaji, tukiwatengenezea mazingira yaliyobora; tunaenda kuzalisha taifa lenye vijana ambao kesho taifa letu litakuwa na nguvu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, Profesa Kitila nakuomba, mjadala wetu wa mpango umetanguliwa na mjadala wa Ripoti ya CAG. Nilichangia mwaka jana, nikashauri kwamba tunahitaji kutengeneza sheria mpya ya uwajibikaji wa watumishi wa umma. Lakini kwa sababu mpango huu tunataka tuuone uki-*reflect* kwenye uchumi wa nchi yetu, na moja kwa moja Ripoti ya CAG ilikuwa inaonyesha namna gani uchumi wetu unadhidi kuathiriwa na matendo ya baadhi ya watumishi wetu, ninadhani kuna umuhimu mpango wako ukaonyesha namna gani unakwenda kufanyia kazi changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kutengeneza mipango ya bajeti ya trilioni 47 tunayoizungumzia sasa ilhali hatujarekebisha changamoto ambazo tumetoka kuzijadili juzi. Maana yake ni kwamba, tunategeneza mazingira yale yale ya viwango vikubwa zaidi kuendelea kupotea kadiri tunavyozidi kuongeza bajeti. Nadhani tutakuwa hatuendi vizuri kama taifa kama tunadhani kutatua changamoto zetu ni kuongeza ukubwa wa bajeti bila kuziba kunakovuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukabaki na bajeti zetu ndogo lakini kama fedha inakwenda kule inakostahili na inatumika vuzuri, bado tukapata maendeleo makubwa kuliko kuwa na bajeti kubwa ambazo zina mianya mingi zaidi inayovuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani kwa mchango wako mzuri. Nilimtaja Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kama ambavyo wengi waliotangulia wamesema, kwamba mpango huu ni matokea ya kazi nzuri ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na mipango mingine. Kwa hiyo na mimi naomba niungane nao kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo ameonyesha umahili mkubwa tangu alipoingia madarakani na kuwa na mipango mingi inayotekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuirudisha Tume ya Mipango. Hii ni dalili njema ya kuonyesha kwamba Watanzania tumeamua kupanga, na kupanga ni kuchangua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaona ndugu zangu wawili pale kutoka Iramba, wanaosimamia mpango huu. Mheshimiwa

Profesa Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Nawapongeza kwa namna ambavyo mmeonyesha kwamba mmejipanga kupanga kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nishiriki kwenye kupanga kwa kuwashauri wapangaji wenzetu. Nadhani wote tunafahamu, ili nchi iendelee inahitaji kuwa na mipango thabiti na endelevu, mipango ambayo Watanzania wakilala wakati wanaamka wanajua nini kitatokea. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali, tunapokubaliana kwamba tumepanga jambo fulani basi sote kwa pamoja tutumie nguvu zetu kulitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakuwa tunakutana hapa kupanga mipango mipya wakati mipango ya zamani hatujaitekeleza, tutakuwa hatutendi haki. Kwa hiyo, niaombe sana ambao mmepewa dhamani hii ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza maono yake kwenye taifa hili, mhakikishe kwamba kila tunachokipanga mnakisimamia kinatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nitoe mfano mdogo, kwa sababu mimi ni moja ya Wabunge wengi wanaotoka vijijini. Mazingira ya vijijini kidogo nayafahamu. Vijiji vyetu wakazi wake wengi ni wakulima na wafugaji. Wakulima wanalima mazao ambayo ni malighafi za viawanda na mazao mengine yanasafirishwa yakiwa ghafi hivyo hivyo kwenda nje ya nchi na kulipatia taifa fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vyetu vinapata malighafi kutoka mashambani kwa asilimia kubwa. Mazao ambayo yanaenda nje moja kwa moja bila kuchakatwa kama hii wanaita korosho, choroko, dengu na pamba inachakatwa kidogo inapelekwa nje; mazao yote haya ni chanzo kikubwa cha mapato ya nchi yetu. Kwa hiyo ni lazima wote tujipange katika mopango yetu kuhakikisha mazao haya yanakuwa na tija. Tija kwa Serikali kukusanya fedha lakini tija kwa wakulima wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tuna shida moja kwenye kupanga. Maeneo ya vijijini ambako mazao haya

yanatoka tumekuwa tukiyasahau. Kwa hiyo nataka niwakumbushe wenzangu, na nitumie mfano huu kumkumbusha kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu; tangu niwe Mbunge wa Sumve na tangu awe Waziri wa Fedha kwenye kila mpango na bajeti tumekuwa tukizungumza kuhusu Miundombinu katika Jimbo la Sumve. Kaka yangu huyu amekuwa mtu mwema sana kwangu. Amekuwa ananiahidi na kuonyesha kwamba atafanya. Kwa kweli kwenye kuniahidi na kunionyesha kwamba utafanya, mimi nakupa *big up* kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi zimekuwepo za uhakika lakini hazitekelezwi. Kwa hiyo ndugu yangu ili twende pamoja na ili tuanzishe mpango mwingine ahadi yako uliyonipa hapa tarehe 22 Juni, 2022, ya kwamba utanijengea kilometa zangu 71 za kutokea Magu – Bukwimba – Ngudu mpaka Nhungumalwa, kwa kiwango cha lami na ukaniambia umepata na mkopo, jenga basi. Ili mpango huu uende uje na mwingine. Lakini kama tutakuwa na mpango ule ule hautekelezwi halafu Watanzania hawa hawa tunakata tena Wabunge wao wasimame wapange mipango mingine inakuwa siyo sawa. Naomba na ninasisitiza kwamba tilichokipanga tukitekeleze *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mheshimiwa Kitila Mkumbo akiwa *back bencher* huku, aliwahi kusema hapa kuhusu Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Madiwani. Kwamba, wale ndio wanaosimamia fedha zetu kule vijijini. Mheshimiwa Ng'wasi Kamani amesisitiza hapa kuhusu Ripoti ya *CAG,* na kwa mfumo wetu wa Bunge kuna Kamati Maalum kabisa inakagua Hesabu za Serikali za Mitaa. Kwa nini Kamati hiyo inazikagua? Na kwa sababu fedha nyingi tunazipeleka kule na kwa mujibu wa mfumo wetu Waheshimiwa Madiwani ndiyo wasimamizi wa hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiamua wenyewe kupiga mpira, tunajirudishia pasi na tunajipiga chenga wenyewe. Wale wanaotakiwa kusimamia fedha hizi hayujawawezesha. Kwa hiyo Mheshimiwa Halima Mdee na Kamati yake wataendelea kila siku kutuletea madudu hapa na Serikali itaendelea kulalamikia wizi na Waheshimiwa Mawaziri mtaendelea kupanga kupeleka

fedha na kutumbua watu kama hamjajipanga kuweka walinzi halisi wa hizi fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia Taarifa za Serikali. Naona juzi kuna nyaraka ilitoka ambayo inawa-*exclude* Wenyeviti wa Halmashauri kwenye kusaini mikataba. Sijui tunaona shida gani kama Madiwani watasimamia ile mikataba. Yaani tunataka Wakurugenzi wetu hawa ambao wakati mwingine hawana uwezo wa kutosha kufanya kazi ya ukurugenzi kwa sababu hawana uzoefu, waende kwa kutumia vichwa vyao wasaini mikataba bila kusimamiwa na Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatengeneza mwanya wa fedha zetu tunazozipeleka huko, ziende zikapotee. Kwa hiyo, mimi naomba niishauri Serikali kwamba, baada ya kupanga kutafuta fedha na kupeleka maendeleo, pia tupange kulinda na kuzisimamia fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nataka kuzungumzia Sekta ya Utalii. Sekta ya Utalii ni sekta ambayo inatuingizia mapato mengi sana; na wote tunafahamu kwamba tuna mbuga nzuri kabisa ya Serengeti na mbuga zingine, lakini wote tunafahamu kutokea Mwanza kwenda Serengeti ni karibu zaidi kuliko popote pale katika viwanja vya ndege nchini. Uwanja wa Ndege wa Mwanza uko karibu zaidi na Serengeti, lakini kwa nini watu hawautumii? Kwa sababu Serikali haijapanga kuuboresha uwanja ule kuufanya uwe wa Kimataifa. Kwa hiyo, hautumiki na sekta yetu ya utalii inakuwa imeng'ang'ania eneo moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitokea Mwanza, ukaenda kwenye Jimbo la Kisesa kwa kaka yangu Mheshimiwa Mpina, pale Mwandoya ukaongea na wananchi kuhusu wanyama pori, ni viumbe anaowachukia kuliko viumbe wowote. Wanajiuliza kwa nini tunafuga tembo ambao wanaharibu mazao yao na wanaua watu wao. Kwa sababu hawafaidiki kabisa na huu utalii, lakini Serikali imeamua kuyatelekeza maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupanga sekta ya utalii, wekeni miundombinu ya kiutalii Mwanza. Kuna barabara za

msingi kabisa za kiutalii. kwa mfano ukitokea Bujingwa kupitia Nyambiti kwenda Malya, ukaenda Ngulyati, ukaenda Itilima, ukaenda Mwandoya mpaka Sakasaka kwenye geti lile la Maswa *Game Reserve* ni karibu zaidi kuliko mtu atokee *KIA* mpaka aje huku. Sasa kwa nini hizi barabara hamziboreshi, hamzijengi halafu tunakutana hapa tunapanga kuboresha sekta ya utalii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba niishauri Serikali kwamba, sasa imefika wakati Maeneo ya Kanda ya Ziwa nayo yaboreshwe ili kukuza sekta ya utalii na iwe na manufaa kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kasalali. Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa na mimi ya kuchangia jambo hili muhimu sana lililopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mola ambaye ametujalia afya njema, uhai, na leo tuko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nimshukuru kipekee kabisa Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo amekuwa akileta fedha nyingi kwenye majimbo yetu. Nawashukuru na wawasilishaji, Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa *Prof*. Kitila, kwa namna ambavyo wameleta wasilisho zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujadili huu mpango ulioko sasa hivi, naomba na mimi niseme maneno machache kama alivyosema Mheshimiwa mwenzangu aliyepita. Ni vizuri tunapoleta mpango hapa tukaangalia umefanikiwa kiasi gani, lakini pia tuangalie takwimu ambazo zinaletwa kwenye hii mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye takwimu za maji wanasema upatikanaji wa maji mijini ni asilimia 88. Jambo hili

katika *logic* sio sahihi, sisi wote tuko hapa mjini, Dodoma hapa tulipo tunapata maji siku tatu kwa wiki, siku tatu maana yake ni 3/7 x 100 = 42%, sasa kama Dodoma ni asilimia 42, wananchi wanapata maji siku tatu kwa wiki, tunawezaji kuandika takwimu asilimia 88. Haya mambo tuyaseme vizuri ili tukapange mipango ya kuhakikisha watu wanapata maji, hawa wataalam wetu sijui wanatumia maarifa gani katika ku-*calculate* haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli Jimboni kwangu alisema siku moja hapa Mheshimiwa Condester, kwake ni asilimia 22 kwangu ni asilimia 33. Sasa tunaweka mipango ambayo haitekelezeki lakini kwenye makaratasi inaandikwa kwamba haya mambo ukiangalia wanataja visima ambavyo tayari vinatoa maji. Mwaka 2022/2023, 2021/2022 mimi nimepewa visima, nimepewa visima 11 mpaka leo vimechimbwa viwili, nimepewa visima vitano bajeti imepita havijawahi kuchimbwa, nimepewa mabwawa ambayo hayajawahi kuchimbwa. Halafu ukiangalia kwenye takwimu wanasema kwamba maji yanapatikana vijijini kwa asilimia 78.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi taarifa zinatuchonganisha na wananchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Monni, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Naomba nimpongeze anayechangia Mheshimiwa Monni, kwenye eneo la asilimia upatikanaji wa huduma ya maji. Wataalam wanakuletea zile *percentage,* wanaangalia ni *coverage* ya miundombinu pamoja na upatikanaji wa maji bombani. Kwa hiyo, suala la visima analoliongelea, visima vyote ambavyo vinaahidiwa tumeendelea kuchimba kadri tunavyopata fedha tunawafikia na yeye mwenyewe kwenye jimbo lake atakuwa shahidi amepata upendeleo mkubwa wa

gari lile ambalo Mheshimiwa, Dkt. Samia, amenunua 25, sehemu ya kwanza kuchimba visima ilikuwa ni jimboni kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa aongee kile kitu ambacho anakifahamu kwa dhati, kama hiki kinamchanganya ni vyema asipotoshe umma lakini kama anahitaji maelezo zaidi kama anavyokuwa anakuja ofisini pale Wizarani, basi aje tuendelee kumuelewesha lakini sio kupotosha umma, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mohamed Monni, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza siipokei taarifa yake, lakini anasikitisha sana halijawahi kuja gari hilo kuchimba maji na tena naomba niseme machache kuhusu haya magari yaliyoletwa. Wabunge ni mashahidi, magari yameletwa lakini hayafanyi kazi, bora wangempa mtu binafsi wamshirikishe yangeleta maji. Kila moa, leo walete takwimu zinazoonyesha magari ya UVIKO, yamechimba visima vingapi? Walete takwimu, kama yamechimba visima, yamechimba visima viwili, vitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Dodoma kwanza sijawahi kupata hilo gari kuja kuchimba hayo maji na huo ndiyo ukweli maana yake Mheshimiwa Waziri, anadanganya na ananitengenezea taswira mbaya kwa wapigakura wangu. Ninachojua, kuna Mkandarasi amepewa kazi ya kuchimba visima 11, tangu mwaka jana gari limekaa pale kwa Mtoro, hawajampa fedha tangu mwaka jana lina miezi 11 mpaka leo. Halafu wale watu hawana maji wanaliona gari la kuchimba maji hili hapa, halafu nauliza nini kimetokea, naambiwa hawajapewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kusema maneno mengi zaidi. Nikisema maneno mengi zaidi nitakuwa mahali fulani naumiza. Nataka niwahakikishie Wizara ya Maji, imekuwa inaletwa kuwa inapewa fedha kwa asilimia 96, kwenye bajeti hapo ilisema hayo maneno. Hizo fedha zinapelekwa wapi, maana yake zinapelekwa sehemu nyingine, jimboni kwangu haziletwi sio sahihi, sio kweli kwa sababu Jimboni kwangu visima 11 vya 2021/2022 havijachimbwa,

vimechimbwa viwili. Visima vitano vya 2022/2023 mpaka leo havijachimbwa na muda umeisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa, Kidoka kulikuwa na bwawa la bilioni tatu, tumeweka bango mpaka leo tuna mradi kule Machija, mpaka Katibu Mkuu, amekuja bado hakuna kitu kilichoendelea, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, tuna mradi wa milioni 600 Chandama, mpaka leo Katibu Mkuu, amekuja tumempeleka, miradi yote haijakamilika, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisimame hapa, wakati watu wangu wanajua hawapati maji, halafu niseme kwamba mipango hii inapangwa na inaenda vizuri, haiwezekani! *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Monni, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namuunga mkono Mheshimiwa Mbunge, kwa mchango wake anaochangia. Nataka nimpe taarifa na niwaombe na Waheshimiwa Wabunge wengine, kwamba wala hatuna haja ya kugombana isipokuwa hali ya masuala ya maji imebadilika sana kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa maana hiyo fedha tumetoa, wakati tuko kwenye bajeti tulitoa bilioni 104 kwenda tu Wizara ya Maji na hizo zilikwenda lakini kwa sababu kila kijiji pana mabadiliko makubwa ya tabianchi wale watu ambao zamani walikuwa wanapata maji, kila Mbunge hapa atashuhudia waliokuwa wanapata maji tu yanatiririka sasa hivi hayapatikani maji ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *concentration* ya watu wote kutakiwa wachimbiwe maji ni kubwa sana na vijiji vinaongezeka na vitongoji vinaongezeka. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameleta gari kila mkoa. Pamoja na kuwa gari liko kila Mkoa WAbunge watakubaliana nami kwamba halitaweza kuchimba kila kijiji siku moja. Kwa hiyo, Mheshimiwa

Mbunge, tumepokea hoja yake hiyo na tunaichukua kama *special case,* tumewasikiliza na Wabunge wengine na juzi hapa Waziri wa Sekta alipokuwa anahitimisha hoja amepokea na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea mchango wa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge, waendelee kuiamini Serikali, hili ni moja ya jambo la kipaumbele kwa Mheshimiwa Rais na sisi kama wasaidizi wake tunaweka uzito huo huo na sisi Wizara ya Fedha, tutaendelea kutoa fedha katika maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante. Mheshimiwa Mohamed Monni, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kiungwana kwa sababu ametoa maneno ya kunifariji na kwa sababu yeye ndiye Waziri wa Fedha, naamini sasa akirudi ofisini atatoa fedha maalum kwa ajili ya Jimbo la Chemba na Wilaya ya Chemba. Namshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisiseme tena kuhusu maji. Ukiangalia mpango unaeleza kwamba sasa tunaenda kuchochea maendeleo vijijini na watu hawa ni matajiri. Mimi natoka Jimbo la Vijijini ambapo kura ndiyo rahisi zaidi kuzipata kwa Chama chetu Cha Mapindizi, lakini tunawakwaza. Kwanza nishukuru kwa barabara, ile barabara ambayo tayari Mkandarasi amepewa kutoka Kibirashi – Handeni – Chemba – Singida inakata katikati mwa Jimbo langu, niwashukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba barabara ile kidogo itapunguza namna ambavyo watu wanaweza kusafiri. Hata hivyo, zipo barabara ambazo ndiyo maeneo ya uzalishaji, kuna barabara ya kutoka kwa Mtoro hadi huko maeneo ya mashambani kilometa 56, huko ndiko alizeti zote zinazalishwa, huko ndiyo ufuta wote unaouzwa Dodoma unapozalishwa, lakini gharama ya kuzileta Dodoma ni kubwa sana. Fedha zinazotengwa kwa ajili ya ukarabati wa hizo barabara milioni 30, nataka niwaombe kwenye mipango hii lazima takwimu zionyeshe uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru Kamati ya Bajeti, wameeleza wazi kwamba takwimu zilizowekwa sio halisia, wanaomba watu wa mipango wakafanye upya tafiti ya takwimu zilizopo kwenye makaratasi ili sasa tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo lingine la muhimu sana. Sisi ambao tunatoka majimbo ya vijijini sijui changamoto ni nini, lazima tukubali kwamba kule kama wanataka kuwarudisha watu vijijini, lazima Serikali itengeneze mazingira mazuri, huo ndiyo ukweli. Ukienda vijijini tunajenga sasa hivi madarasa, lakini hakuna mpango wowote wa namna gani sasa hata hayo madawati yanaweza kuwa yanatengenezwa baadaye. Sasa hivi tunajenga darasa tunaweka na madawati, lakini nataka niwaambie ukienda shule zote za Chemba 112, upungufu wa madawati ni asilimia 70, wazazi hawana uwezo wa ku-*cover* hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tunaweza kuwa tunatengeneza asilimia 10, lakini ni makakati upi wa Serikali kwa nchi nzima sasa wa kuhakikisha wanaenda kutatua hiyo kero. Tunajenga madarasa ya *aluminum,* yana *tiles*, lakini watoto wataendelea kukaa chini, kwa sababu tumeweka vipaumbele sehemu nyingine, sehemu nyingine tumeacha. Nimwombe Waziri wa Fedha lakini pia nimwombe Mheshimiwa Profesa Kitila, rafiki yangu tunafahamiana sana tangu tukiwa *Pugu Secondary*, anajua na nilikuwa mshabiki wake alikuwa akigombea u-*head prefect,* natafuta kura zake. Nimwombe sana atafute namna ambayo tunaweza kutatua changamoto zilizoko, lakini …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme maneno mawili ya mwisho. Kuna tatizo kubwa sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, malizia muda wako. Kengele ya pili imeshalia.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuwapa pole sana wananchi wangu wa Kijiji cha Handa, ambao wamechomewa nyumba na mahindi kuanzia jana na juzi *operation* ya kuchoma nyumba na watu wa *TFS*, inaendelea. Amesema Mheshimiwa Deus Sangu, hapa tulitamani tuijadili ili tueleze hali halisi, jana watu kadhaa wamechomewa nyumba zao, mahindi yao yamechomwa halafu watu walioenda kuchoma pale ni watu wa *TFS* na magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yawezekana kabisa wananchi wangu wamevunja Sheria. Sasa unawezaje mtu mwenye akili za kawaida unaenda unachoma nyumba ya mtu, labda kweli ipo kwenye msitu wa hifadhi, unachoma nyumba ina magunia 60 unachoma, unaenda nyumba ya pili ina magunia 30 unachoma, ndiyo nini sasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante kwa mchango wako kwenye matayarisho ya mipango.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako, tunashukuru sana Mheshimiwa Mohamed Monni.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Bunge linarejea.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Kiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam, Mwongozo wa Kiti.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 76. Kuna jambo linaendelea nchini Congo ambalo litakuja kuathiri uchumi wa nchi hii, kuna mtu anatangaza katika mitandao ya kijamii na kuzuia magari ya Tanzania yasibebe *copper* na kusema magari hayo yakibeba *copper* yapigwe mawe. Zaidi ya magari 2800 yanayopakia *copper* kutoka Congo kuja Tanzania, tarehe 20, huyu mtu anasema yasipakie na madereva watakaobeba wauawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni kauli ambazo zimetoka, ni tata na hatujaona kauli ya Serikali katika zuio la jambo hili na mtu huyu ni Mtanzania, kwa jina kabisa anaitwa Masanja na ana *passport* kila kitu na anakaa katika *media* za nchi nyingine Congo, Zambia.

Sasa tunatoka katika ushindani wa jambo lingine la bandari, hawa watu wanatafuta njia nyingine tena ili waweze kupata mizigo ya Beira pamoja na Durban.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kauli ya Serikali juu ya jambo hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Hamis Tabasam, kwa mujibu wa Kanuni ya 76 akiomba Mwongozo wa Kiti na kwa mujibu wa Kanuni zetu Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo huo unaombwa kwa jambo ambalo limetokea mapema Bungeni leo. Sasa kwa kuwa umesema jambo hili na Serikali imesikia kwa sababu Kiti hakina taarifa hiyo rasmi na Serikali ipo, basi itachukua na italifanyia kazi, huo ndiyo Mwongozo wa jambo hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru sana Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia katika Mpango kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha huo unaokuja 2024/2025. Tutaendelea na mchango jioni ambako tutaanza na Mheshimiwa Yahya Ali Muhata atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mheshimiwa Leah Jeremiah

Komanya, Mheshimiwa Mohamed Issa na tutaendelea kutaja majina jinsi tutakavyokuwa tunaendelea.

Waheshimiwa, baada ya matangazo hayo machache nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00, jioni.

*(Saa 7.13 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**na**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na michango ya Waheshimiwa Wabunge. Tutaanza na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mheshimiwa Mohamed Issa ataendelea.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambae ameniwezesha mchana wa leo kuwa ndani ya Bunge lako hili Tukufu na kuwa mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuwatumikia nchi hii. Tatu sina budi kuwashukuru Mawaziri wote wawili kwa uwasilishaji wao mzuri Profesa Kitila Mkumbo kwa uwasilishaji wake mzuri wa Mapendekezo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze katika yale maeneo ambayo yana lengo la kuisaidia Serikali kupunguza nakisi ya urari wa biashara ya nje, hivyo nitajielekeza katika maeneo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ule uwasilishaji wa Mwenyekiti wa Bajeti ambae aliwasilisha Makamu Mwenyekiti walieleza kwa kina kwamba kilimo cha umwagiliaji ndicho ambacho kinaweza kikaitoa nchi yetu kutoka sehemu tuliyonayo na kwenda sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika takwimu ambazo amezieleza, wameeleza kwamba nchi yetu ina eneo la hekta 29.8 za kilimo kwa ajili ya umwagiliaji. Hadi Juni, 2023 ni hekta 822 tu ambazo zimetumika kwaajili ya umwagiliaji. Hii inamaanisha kwamba ni asilimia 2.8 tu ya eneo zima limetumika kwa shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hizi takwimu utaona kabisa kwamba tuna kazi kubwa ya kufanya. Hatuwezi kuondoa nakisi hii kama hatutatilia mkazo kwenye kilimo cha umwagiliaji. Tunayo mabonde mengi ndani ya nchi yetu, tunalo Bonde kule Ziwa Viktoria, tunalo Bonde la Ziwa Tanganyika, tunalo Bonde la Ziwa Nyasa na tunalo Bonde katika Mto Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yote haya yanahitaji kuendelezwa ili wananchi wetu, vijana wetu ambao tunawahimiza wajihusishe na shughuli za kilimo waweze kutumia kilimo cha umwagiliaji kama njia ya kujipatia riziki zao. Lakini bila kilimo cha umwagiliaji…

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na msemaji sasa hivi kuhusiana na maeneo ambayo yamekuwa *identified* kwa ajili ya umwagiliaji. Ningeomba wakati Serikali inakuja ku-*wind up* hebu itutajie maeneo kwamba ni maeneo gani kwa sababu ukisema tu ukubwa bila kutaja maeneo yenyewe mwisho wa siku hatujakua kwamba ni wapi kama tumefanikiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaipokea hiyo taarifa ya ziada?

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea ni mchango mzuri. Kwa hiyo, utaona kwamba kuna maeneo mengi ambayo yanahitaji kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji. Mfano katika Bonde la Mto Ruvuma ukianzia Mtwara Vijijini hadi katika maeneo yangu ya Jimbo langu la Nanyumbu eneo lote hili halina eneo kwa ajili ya umwagiliaji jambo hili kwa kweli si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Kitila Mkumbo waliingize katika mipango ya maendeleo ili vijana wetu ambao tunawahimiza waende wakajishughulishe na shughuli za kilimo waweze kufanya shughuli hii mwaka mzima, vinginevyo watakuwa watu wa kusubiri mvua ya Mwenyezi Mungu ambayo kwa kweli haitaweza kumkomboa kijana huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika ukiangalia vijana wetu wanahitaji nyenzo, nyenzo ambazo zitawawezesha wao kufanya kazi kwa bidii. Changamoto ambayo ipo na ukiangalia ile ripoti iliyotolewa na Kamati ya Bajeti wameeleza mgongano wa kimaslahi kati ya taasisi mbili. Kuna taasisi ya umwagiliaji ambayo ipo chini ya Wizara ya Kilimo, pia kuna bodi inayoshughulikia mabonde ya haya maeneo ambayo iko chini ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo wanawajibika katika kuandaa miundombinu lakini maji ni ya watu wa bonde la maji kwa hiyo matokeo yake mgongano huu unasababisha shughuli za kimaendeleo zisiende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Mheshimiwa Waziri na Bodi, hebu tukubaliane ni nani anayewajibika uendelezaji wa mabonde yetu haya kwa ajili ya shghuli za kilimo vinginevyo maji yote ambayo yanapatikana yataishia baharini na wananchi hawanufaiki chochote. Naomba sana jambo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni upatikanaji ya mitaji ya kilimo kwa ajili ya wananchi. Jambo hili siyo jepesi kama linavyoonekana, wananchi wetu kwa kweli wanahitaji mikopo. Ukiangalia takwimu ambazo Kamati yetu ya Bajeti imeeleza mwaka 2022/2023 karibu trilioni 2.6 zilitengwa kwa ajili ya utoaji wa mikopo mbalimbali kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza asilimia Saba ya trilioni 2.6 ilitumika kwa ajili ya mikopo ya uzalishaji na asilimia 93 ilikwenda kwa ajili ya kununua mazao, maana yake asilimia 93 ilitumika kama ulanguzi tu madalali wa ununuzi na asilimia saba peke yake ndiyo ilitumika kwa ajili ya kuwapa watu mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili hatutaweza kutotoa sisi na kuondoa hii nakisi ambayo ipo. Tunahitaji tuzalishe kwa wingi ili tuweza kuingiza fedha nyingi za kigeni. Nitawapa mfano mmoja, mimi natoka ukanda ambao unazalisha sana korosho, mwaka juzi Mkoa wa Mtwara au kwa maana ya korosho yote tulizalisha tani 300,000. Mwaka jana zao la korosho lime-drop kutoka tani 300,000 hadi tani 182,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini maana yake, maana yake kwamba tumepoteza fedha nyingi za kigeni ukilinganisha mwaka juzi na mwaka jana. Jambo hili kama hatutatilia mkazo tutaendelea kupoteza fedha za kigeni kwa sababu wakulima wetu ambao ndiyo tunaowategemea wazalishe korosho ili tupate fedha za kigeni wanashindwa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo mkulima tunazungumza, mkulima anahitaji mkopo, mtu wa pamba kule anahitaji mkopo kwa ajili ya maandalizi ya shamba lake, mtu wa pamba anahitaji mkopo kwa ajili ya kulipa vibarua ili waweze kuanda shamba lake, mtu wa korosho anahitaji mkopo kwa ajili ya kupalilia mikorosho yake, mtu wa mikorosho anahitaji mkopo kwa ajili ya kununua viuatilifu vya kupulizia shamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya jambo kubwa sana la maana inatoa pembejeo kwa wakulima. Jambo hili nizuri kabisa na mimi naonga mkono mia kwa mia lakini, pembejeo pembejeo peke yake haitamsaidia mkulima. Naomba sana wakulima hawa wapewe mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani leo benki zetu za CRDB, NMB, Benki ya Kilimo hawatoi mikopo kwa wakulima wakati wakulima wote wa Kanda ya Kusini wanahifadhi fedha zao katika hizi benki, hili jambo siyo sahihi! Kama kweli tunataka kuhakikisha tunazalisha Korosho za kutosha na itatuingizia fedha nyingi za kigeni tuwapatie mikopo wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza nani mwenye kauli ya kuilazimisha benki hizi zifanye hivyo? Mheshimiwa Hussein Bashe - Waziri wa Kilimo mwaka jana alikaa na hizi benki kwamba toeni mikopo kwa wakulima lakini hakuna benki iliyofanya hivyo! Benki wanakuambia tunashindwa kutoa mikopo kwa sababu wakulima hawalipi, kwa hiyo wale wafanyabiashara walanguzi ndiyo wanapewa hela nyingi lakini wakulima wazalishaji hawapewi mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana jambo hili litiliwe mkazo sana ili wakulima wetu waweze kupata mikopo, waweze kuzalisha kwa wingi.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba kuna shida upande wa mikopo kwa wakulima hasa vijijini kwa sababu hawana *collateral,* hii inahitaji mabadiliko ya Sheria ya Ardhi ili watu wa vijijini nao wawe wanapata hati badala ya kuwepa hati nyingine ya kimila ambayo benki haitambui kama *collateral*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya unaipokea taarifa?

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wazo zuri la Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli kwamba wananchi wanahitaji mikopo na Serikali ipime ardhi lakini nataka niwaambie kwenye korosho mimi natoka katika eneo la korosho na ni mkulima wa korosho, mikorosho yote wananchi wote mikorosho yao inajulikana na wakulima na mabenki yote yanajua kila mkulima ana hekari ngapi, kwa hiyo inatoa mkopo kulingana na idadi ya mikorosho uliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mkulima anayo *account* katika benki husika, kwa hiyo hakuna *room* ambayo itasababisha mkulima ashindwe kulipa huo mkopo. Benki wana sababu ambazo kwa kweli nashindwa kuelewa kwanini hawatoi mikopo kama lengo ni kumuondolea mkulima adha hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu naomba nichangie kipengele cha madini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya malizia muda wako nimekuongezea dakika moja kwa sababu muda umeisha.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Tumeambiwa hapa kwamba jinsi gani madini yanavyoongezea uchumi nchi yetu, lakini naomba nieleze kuna maeneo ambayo yanayo madini lakini wakati huo huo ni hifadhi za nchi yetu. Je, kuna mpango gani wa wananchi wanaoishi katika maeneo yale ili waweze kuchimba madini yale bila kuadhiri uhifadhi katika maeneo yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo tutakuwa tunalinda yale maeneo tukija kutaharuki madini yote yametoka na wananchi wanakuwa hawana chochote cha kujivunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono na nakubaliana sana na wazo la Mawaziri wetu na nina imani katika mabadiliko haya machache ambayo watayafanya nina imani kwamba tutakwenda pamoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya Mhata. Nilimtaja Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mheshimiwa Leah Komanya ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika mpango huu, pia nichukue nafasi hii kupongeza kwa ajili ya mpango huu na nitakuwa na mambo machache ambayo naamini nitachangia na kupata ufafanuzi ili tuweze kwenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachangia mpango na hii ndiyo dira ya utendaji wa kazi katika nchi yetu, katika Wizara zote na Idara zote. Kama ambavyo mpango unasema tunaangalia dira ya maendeleo ya Taifa lakini pia tunaangalia mipango mingine iliyopangwa ya muda mrefu lakini tunaangalia mpango uliopita mwaka jana, tunaangalia na Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo nilitegemea kama ambavyo Kamati wameeleza kwamba kuna mapungufu ya jumla yaliyotokea kwenye Mpango, ni kitu cha muhimu sana ambacho Mheshimiwa Waziri akisimama atuambie. Tunakwenda kupitisha mpango huu lakini mapungufu yake ya jumla ni kwamba tumemaliza mpango ambao umeisha, hatujaambiwa katika Mpango ule ulioisha kuna ajira ngapi zilitengenezwa kutokana na ile miradi ya maendeleo. Sisi 2025 tunakwenda kwa wananchi waliotupa ridhaa ili tuwaambie yale maelekezo ya CCM tutengeneze ajira 8,000,000 mwaka huu tulitengeneza hizi, mwaka huu tulitengeneza hizi lakini mpango haujaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda mpango huu una miradi ya maendeleo baadhi yake haijaelezwa bayana na sisi

tunakwenda kupitisha kwamba uwe ni mpango wetu ambao unabeba miradi yetu ya maendeleo ambayo haijaelezwa bayana. Tunaomba miradi hiyo Mheshimiwa Waziri ukisimama tupate kwa ubayana wake. Pia hatujaelezwa kinagaubaga mafanikio tunayokwenda kuyapata kwenye huu mpango, akisimama atueleze mafanikio tunayokwenda kuyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba nne mpango huu kama ambavyo upo sasa, kwa kuwa tumesema mipango yetu sasa hivi tunayopanga iendane na Sensa tuliyoifanya na kuimaliza mwaka jana. Haijatoka ile ripoti yote ya Sensa lakini anagalau tumepata baadhi ya ripoti. Sasa kama walivyosema mzungumzaji Mheshimiwa Mbunge aliyepita Mheshimiwa Ng'wasi tumetumia zaidi ya bilioni 400 kufanya Sensa, yale matokeo ya Sensa yanatakiwa kutusaidia kupanga mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani kuona tumeambiwa kwenye Sensa *work force* ya nchi yetu ambayo tunaitegemea watu wenye umri kati ya miaka 15 – 64 ni asilimia 53.1. lakini ukiangalia katika hao watu asilimia 34.5 ni watu wenye umri kati ya miaka 15 – 35 ambao ni vijana tunabakiza *work force* ya 18% tu ndiyo wale ambao ni miaka 36 – 64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, mpango huu ni namna gani umezingatia umri huo wa nguvukazi ya Taifa letu, kuwaweka mipango. Tunakwenda kukopa mkopo wa ndani, sijaelewa mkopo wa ndani ni vipi, tutakopa kwenye mabenki yetu au tunakwenda kukopa kwa wazabuni au tunakwenda kukopaje Waziri atatuambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya dola 6,000 hizo sijui milioni elfu sita sijui, hlafu nje tunategemea kukopa hizo 2,200 na ngapi. Sasa katika huu mkopo ni namna gani hii *workforce* ya vijana miaka 15 – 34 tunakwenda kuitumia. Mheshimiwa Waziri umeongea vizuri sana kwenye ripoti yako, kwamba tunatakiwa tuwe na watu wa kutosha na tuwe na watu bora, watu wa kutosha kwa mujibu wa Sensa na ambao ni bora kwa ajili ya *workforce* hii ni hawa asilimia 34.5 wenye umri kati ya 15 mpaka 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoa walioko shule, milioni tano na kidogo, unabaki na watu karibu 16,000 ambao ni vijana. Hao wengi wao ni wale ambao wameajiriwa kwenye Machinga, boda boda, bajaji, kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti inaeleza vizuri sana kwamba Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 62 kupitia *NFRA* na *CPB* kununua mazao ya wakulima. Nilitamani Waziri wa Kilimo angekuwa hapa, naye kama akipata fursa atuambie ni kwa nini fedha wamepewa za kutosha lakini bado kuna malalamiko kwamba wakulima hawajalipwa mazao yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Iringa wameuza mahindi *NFRA* na wameuza *CPB* lakini hawajalipwa fedha zao. Tatizo liko wapi? Kwa sababu hii ndiyo *workforce* ambayo tunaitegemea kwa mujibu wa sensa. Sasa ile mipango ambayo tumesema, kwa mfano, vijana, tuwe na *programme* kabisa ya kuchakachua kuona kwamba tuna *programme* gani? Tuache ile 4:4:2 peke yake, kwa sababu *workforce* kubwa ukiangalia kwenye Taarifa ya *CAG,* wanaopewa ile mikopo wengi ni akina mama, ndio waliopewa zaidi ya asilimia 50 lakini vijana wamepunjwa na watu wenye ulemavu wamepewa kidogo. Kwa hiyo, hii *workforce* bado tunai-*neglect* na kuiacha nje wakati hii ndio nguvu ya Taifa ambayo tunategemea ibadilishe uchumi wetu, tuwe na huo uchumi shindanishi ambao tumeuandika kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii nguvu ya kuchochea tunaiwekea mpango gani? Tuache ile kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ilipewa shilingi bilioni moja ikakosa vijana wa kukopa, wakakopesha tu shilingi milioni 200 tu, shilingi milioni 800 sijui ikaenda wapi; tuwe na mpango madhubuti kabisa. Leo hii tunapoongelea hiyo *workforce*, vijana wengine, nimewatoa wale milioni tano ambao ni wale walioko sekondari, *form one* mpaka *six,* lakini tuna vijana wako vyuo vikuu. Hawa ni *workforce* ambao tunategemea baada ya miaka miwili, mitatu wana-*mature* wanaingia sokoni. Mpaka sasa hivi tunavyoongea, wako foleni wameandikiwa kupewa mikopo lakini hawajapewa na masomo hayajaanza tunaingia Novemba, Desemba, muhula unaisha. Bodi ya Mikopo hawajatoa. Hawa ndio watu tunaowaongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namna gani mpango huu uta-*accommodate* hii *workforce* ya nchi yetu ili kutusaidia ku-*push* uchumi wetu? Hii mikopo tunayosema tunaomba ya ndani zaidi, nataka kujua, kwa sababu kama tutaendelea kuwa-*drain* watu wetu, wazabuni wetu na kuwakopa, ku-*drain* benki zetu, Serikali ikawekeza nguvu kubwa kukopa huko kwenye benki, halafu wakija sekta binafsi ambayo wewe kwenye mpango wako unasema tuna nia ya kuinua sekta binafsi, kuwaboreshea waweze kuwekeza na kuacha zile shughuli nyingine ambazo Serikali inafanya zinazoweza kufanywa na sekta binafsi, sasa Serikali tuki-*drain* kwa kwenda kukopa kule na kutowaachia wawekezaji binafsi hiyo fursa, bado tutakuwa tumechukua fedha mfuko huu, tumehamishia mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungetamani fedha kubwa na ajira nyingi zijengwe na sekta binafsi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ukisimama naomba utuambie, hiyo ndio *workforce* tuliyonayo? Ndiyo mashine yetu, ndiyo kiwanda chetu cha kuzalisha na kuinua uchumi wetu. Hawa vijana tunawawekea mpango gani kabambe? Tukiachana na miundombinu, tunawawekea mpango gani kabambe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna mpango wa kusema, sasa katika hii fedha, sijui ni shilingi trilioni tatu au ngapi tutakayochukua, hatuna mpango wa kusema hizi shilingi bilioni 500, hebu sasa tukakopeshe kwenye *sound organisation* za vijana wetu wanaofanya biashara ndogo ndogo ili watulipe kodi, lakini uchumi utakuwa umefunguka, kama ambavyo tulikuwa tunasema mabilioni ya mama. Tulivyo-*inject* shilingi milioni 1.3, tayari nchi yote ilikuwa inatetemeka kwamba kuna mabilioni ya Mama Samia yameenea nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tutafute fedha ambayo tutakwenda ku-*inject* kwa vijana, Machinga. Tutafute namna ya ku-*inject* kwa bodaboda au bajaji tukaziweke biashara zao kuwa rasmi, wasimame kutoa ajira. Sasa hivi tuna vijana wengi wame-*graduate* wanafanya vizuri kwenye kilimo cha *irrigation*. Hata ukija kwangu Mkalama wamenitengenezea, kila mwezi nauza nyanya hapo kwa zaidi ya shilingi milioni mbili au tatu. Wametengeneza vijana wadogo tu wa kutoka *SUA*. Tukiwawezesha hawa katika

kila wanachokifanya, tukakiboresha kuwe cha kisasa, tukawatafutia masoko na kuwa-*connect* kwenye masoko nje ya nchi, tunaondokana na umaskini kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, naomba ili tuendane na sensa sawasawa, utakaposimama uje utujibu haya, miradi hiyo ni miradi gani? Iwe bayana; ajira ngapi utakwenda kutengeneza? Mwaka jana ngapi tumezitengeneza? Manufaa gani tunakwenda kuyapata kupitia Mpango huu?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jesca. Nilimtaja Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Mohamed Issa, ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa maoni yangu katika hoja zilizopo mbele. Nitoe pongezi kwa mapendekezo mazuri yaliyoletwa na Mawaziri wetu wote wawili. Sina wasiwasi juu ya utendaji wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais wetu, Mama yetu Samia kwa kazi nzuri anazozifanya hususan katika utekelezaji wa miradi mikubwa na mingine ya vielelezo. Kwanza ni utekelezaji wa mradi wa umeme wa Mwalimu Julius Nyerere ambao hadi Juni, 2023 ulikuwa umefikia asilimia 91 na malipo yake hadi Julai yalikuwa asilimia 84.3. Kutekelezwa kwa mradi huu kunatuletea uhakika wa kupata umeme na tukiwa na uhakika wa kupata umeme, mambo mengi yataenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunahitaji uhakika wa umeme? Hata mapendekezo yaliyoletwa na Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji katika kuanzisha viwanda ambavyo vitafanya mchakato wa awali vinahitaji uhakika wa umeme. Tunahitaji uhakika wa umeme ili kupunguza gharama ya uzalishaji katika viwanda vyetu ili zile bidhaa ziweze kushindana na bidhaa

zinazotoka nje ili kuweza kuwavutia wananchi wetu wanunue bidhaa zinazozalishwa nchini zikiwa na gharama ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanalazimika kununua vitu vya nje kwa sababu vitu vile vinazalishwa kwa gharama ndogo, lakini changamoto mojawapo inayosababisha kuwa na gharama kubwa ya uzalishaji ni kutokuwa na uhakika wa umeme. Kwa hiyo, mimi naunga mkono Mpango huu na ninawatakia kila la heri katika utekelezaji au kutuletea mpango ujao ukiwa na uhakika wa upatikanaji wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, katika mapendekezo aliyoyatoa katika kuchochea na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi ya jamii vijijini yaliyopo katika ukurasa wa 21 na moja ya hatua atakazozichukua ni kuweka mazingira maalum katika kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vijijini kwa lengo la kufanya ongezeko la awali la thamani katika sekta za kimkakati kwa lengo la kuongeza ajira na kubakisha thamani vijini. Maeneo ya kimkakati mojawapo ni kilimo, madini, uvuvi pamoja na mifugo. Nilikuwa nataka nitoe mapendekezo yangu au maoni yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani kwa upande wa kilimo, mazao yanayotegemewa kufanyiwa mchakato wa awali, mojawapo ni zao la alizeti. Ni ukweli usiopingika, mwaka huu zao hili bei yake iliporomoka vibaya sana na hivyo kukatisha tamaa wakulima kulilima tena. Natambua thamani ya mafuta ya alizeti, yanahitajika katika nchi za wenzetu. Kwa hiyo, maoni yangu, baada ya kufanya mchakato wa awali, basi tutengeneze mazingira ya kuwepo wengine wengi ambao watafanya *final processing*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwa na wengi, bado kutakuwa na wachache watakaoweza kuhodhi malighafi hii. Mathalani, katika mwaka huu, wananchi wa Wilaya ya Meatu walichukua alizeti na kupeleka kwenye kiwanda ambacho siwezi kukitaja. Walinunua debe kwa shilingi 6,000/= na walipofika kule walikutana na bei ya shilingi 4,000/=, kwa hiyo, elfu mbili ziliwakata wananchi wetu na yule aliyekuwa anapelekewa alizeti ile anai-*process* na kuipeleka moja kwa moja nje, ambapo inatuletea

fedha za kigeni. Sasa naye anaposema kwamba soko la alizeti limeshuka, nakuwa sielewi. Kwa hiyo, Serikali inavyoweka hii mipango, iwahakikishie wananchi wetu masoko ambapo hakutakuwa na ukiritimba wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja zilizoletwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika maelekezo ya maandalizi ya mpango wa bajeti wa 2024/2025 ni kuhusu mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. Naomba kuwepo na mpango kabambe wa kutekeleza matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kuendelea kufanya uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2022 kama tutakumbuka, katika kongamano la nishati safi ya kupikia, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo ya taasisi kuanza kutumia nishati safi. Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, alitoa tamko kwamba matumizi ya kuni mwisho Januari, 2024. Wakati anatoa yale matamko, tayari sisi huku Bungeni tulikuwa tumeshapitisha bajeti, kwa hiyo, ilikuwa ni ngumu kufanya utekelezaji au itakuwa ni vigumu *by* Januari, 2024 kwamba matumizi ya nishati ya kuni yawe mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi naomba Serikali iwe na mpango kabambe. Kama ni kukopa fedha katika mfuko wa hazina ikope, kwa sababu taasisi hizo zinatakiwa zipate hii nishati safi na wakati huo huo bado zitaendelea kufanya matumizi kwa nishati iliyokuwa inatumika awali. Kwa hiyo, tukichukua kwa pamoja zile fedha tukajenga ule mfumo, na zile taasisi zinahitaji kupika kila siku, itakuwa ni ngumu kutekeleza mpango huu. Kwa hiyo, naiomba Serikali ije na mpango kabambe katika mapendekezo kuhusu suala zima la nishati safi ya kupikia katika taasisi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu maoni ya Kamati yaliyopo katika ukurasa wa 50 kuhusu Wizara, Idara, Mamlaka na Taasisi za Umma kutoshirikiana wakati wa kupanga na kutekeleza miradi. Hali hii imesababisha baadhi ya taasisi kutekeleza miradi katika ngazi ya Serikali za Mitaa huku utaratibu na usimamizi wa ufanyikaji ukitoka Serikali Kuu moja kwa moja na hivyo miradi hiyo kukosa uangalizi ama kutekelezwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika, tunapoteza fedha nyingi kutokana na huu mpango wa kutozihusisha Serikali za Mitaa. Kama utakumbuka, jana niliongelea mfano, mojawapo wa utekelezaji wa mradi wa umwagiliaji ambapo watekelezaji walitoka moja kwa moja *DASIP* bila kuishirikisha halmashauri, tukapoteza shilingi bilioni 1.2, wananchi hawana kitu. Ukienda pale kwenye ule mradi utafikiri ni uwanja wa mpira, hakuna kinachoendelea pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji nayo ilitekeleza Bwawa la Mwanjolwa kwa shilingi bilioni 1.8, limebomoka na sasa wananchi wanahangaika na maporomoko ya maji na mradi ule haujawahi kunufaisha hata siku moja. Sasa basi, kama Meatu ni shilingi bilioni tatu, ukiingiza na uhamilishaji wa mifugo 1,000 ambao ulifanywa moja kwa moja kwa Wizara, leo hii ukienda Meatu huwezi kuona ng'ombe mmoja aliye bora aliyetokana na uhamilishaji, lakini fedha nyingi za Serikali zilipotea. Kama Meatu ni shilingi bilioni tatu: Je, nchi nzima itakuwa ni shilingi ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ione namna inavyopoteza fedha kwa kutozishirikisha halmashauri na viongozi waliopo katika *level* ya mkoa pamoja na halmashauri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Leah Komanya. Nilimtaja Mheshimiwa Mohamed Issa, Mheshimiwa Tumaini Magessa ajiandae.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya mpango. Kwa kuanzia, napenda niwapongeze Mawaziri wetu wote wawili kwa kazi nzuri ambayo wameifanya, kazi ambayo inakuja kuleta dira ya nchi yetu kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma vizuri hotuba zote mbili, nimeangalia sehemu za vipaumbele, kwa upande wa Wizara ya Fedha wameandika vipaumbele 12, Wizara ya Mipango wameandika vipaumbele nane, kidogo nilishituka, lakini

nilipofanya uchunguzi wa kina nikaona vile vipaumbele vyote ni sawa. Huku wamechanganua, huku wameunganisha, lakini vyote ni sawa. Hii ni kuonesha kwamba Serikali iko katika *single unit,* yaani ni ya aina moja. Kwa hili, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utaanza sehemu ya biashara. Nimeona hapa wamesema kwamba katika mpango watasimamia *One Stop Center.* Kwanza napongeza. Hili jambo ni zuri ambalo linasababisha kufanya biashara vizuri na nchi ambazo zimetuzunguka. Hiki ni kilio cha Watanzania wengi, wanapofika kwenye mipaka yetu wanakwama sana na wakati mwingine wanatumia gharama kubwa kuweza kuvuka *border* nyingine, kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuja na mpango huu. Napenda sana mpango huu usije ukakwama, tumalize mwaka huu na mwaka unaokuja tusizungumzie kabisa Mpango huu wa *One Stop Center.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hili, nasisitiza Zanzibar nayo inahitaji kuwa na *One Stop Center* kwa sababu nayo ni *border.* Kwa hiyo, katika mpango huu nayo ije; Waziri akiwa ana-*wind up*, atuambie kwamba biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara zimepewa kipaumbele gani? Kwa sababu gani nasema hivyo? Ni kwa sababu biashara inapotoka Zanzibar kuja Tanzania Bara, ama inapotoka Bara kwenda visiwani kunakuwa na *stop* nyingi. Kule kuna *stop* na huku kuna *stop*, kwa hiyo, hii *One Stop Center*, tunataka biashara inapoondoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar ikifika kule iwe ni kulipa *handling charge* siyo jambo lingine, na vile vile ikija huku iwe ni kulipa *handling charge.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kasumba hapa inasemwa kwamba ushuru wa Zanzibar ni mdogo, jambo hili siyo kweli. Maana yake ushuru wa Zanzibar kweli uko chini, lakini ukiangalia gharama za Wazanzibar wanazolipa, ni zaidi ya ushuru unaotozwa Tanzania Bara. Nichukue mfano mmoja, *freight charge* kutoka nchi za nje, mfano kutoka Dubai kuja Zanzibar kontena moja ni dola 8,000 lakini kuja pale Dar es Salaam ni dola 2,600. Kwa hiyo, hii *difference* tu tayari inaleta gharama kubwa. Vile vile kutoa mzigo Zanzibar kuuleta Dar es Salaam kuna *handling charge* pia, kuna *transport.* Kwa hiyo, gharama ni za juu.

Kumtoza mfanyabiashara *differential tax,* siyo halali. Jambo hili liondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumza, tumesema *One Stop Center,* hii ni kwa upande wa *borders*. Tunataka kujua, wakati Mheshimiwa Waziri unakuja ku-*wind up* hapa, Mheshimiwa Waziri wa Biashara, alisema kwamba leseni zote zitakuwa na mfumo wa aina moja. Maana yake, ukiomba leseni hii utakuwa umemaliza shughuli. Kwa hiyo, mara hii kwenye mpango tuje tuambiwe kwamba jambo hili limeanza katika mwaka unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la usafiri kwa upande wa nchi zetu hizi mbili, Zanzibar na Tanzania Bara. Usafiri siyo rafiki. Usafiri uliopo ni wa watu wenye uwezo. Wananchi hawana uwezo wa kulipa nauli ya shilingi 30,000 kwenda Zanzibar ama kurudi. Napenda hasa Serikali ichukue jukumu la kuleta *public transport* ambayo itakuja kuwa na gharama ya chini ili wananchi wetu hawa wasafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja, Serikali haituambii hapa, lakini ndugu zetu wanaotoka Tanga kwenda Pemba ama wanaotoka Tanga kwenda Unguja pale, wengi sana wanakufa ndani ya Mitumbwi. Sasa Serikali hailioni hili? Naomba mpango huu utuelezee kupata *public transport* ili kuokoa maisha ya wananchi wetu. Tusiwe kila siku tunapuuzia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye upatikanaji wa dola. Naipongeza Serikali kwa kutuambia kwamba wana dola za kutosha na benki zetu zinapata dola, lakini cha kushangaza wafanyabiashara wadogo wadogo hawapati hizo dola kule benki. Kwa hiyo, tunataka Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa atueleze upatikanaji wa dola na wananchi watazipata vipi? Kwa sababu inawezekana benki zinafanya ulanguzi, sasa itueleze kwamba itafuatilia vipi? Pia kila mfanyabiashara au anayehitaji dola azipate vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, leo nilikuwa nahitaji dola mia tano kwa kumchangia jamaa yangu alikuwa anakwenda kupata matibabu, nimekosa. Mpaka nimekwenda

kumuomba mtu ambaye anasafiri anipunguzie. Dola mia tano anakosa basi Benki? Basi hili naomba kama Serikali ilisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala la mkataba wa bandari ambao umezungumzwa hapa katika Mpango. Mkataba wa Bandari mimi binafsi naupongeza, ilikuwa ni mkataba mzuri na ninaipongeza *TPA* kwa kuingia huu mkataba wa utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katika Mpango nimeona huu mkataba kutoka *batch zero* mpaka *batch three, batch four* mpaka *batch seven.* Naona kwamba, mkataba huu ni mzuri na unakuja kuleta tija. Mpango haujatueleza. Tuliambiwa hapa kwamba, kwa sasa bandari inakusanya asilimia 10 ya bajeti lakini tukishaingia mkataba huu tutakuja klukusanya asilimia 62. Sasa, Mpango utueleze, je, ni mwaka huu au mwaka unaokuja? Hili napenda kwenye mpango huu mje mtueleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulichangia ni suala la Liganga na Mchuchuma. Suala hili ni suala ambalo tumeona Mheshimiwa Rais, kwanza tunapongeza sana kwa kuweza kulipa fidia kule kwa wenzetu ambako iko miradi hii. Hata hivyo, ningependa kujua sasa huu mpango umetaja jambo hili, tunakweda kwenye *step* gani? Kwa sababu tuliambiwa kuna Mkataba wa wale wenzetu wa kampuni ya kachina. Tunalipa hili ili kuwaokoa watanzania. Je, nataka kujua sasa *status* ya mkataba ule sasa utakuwa umekufa au tunakwenda kwenye mpango kwa kujisukuma ili baadaye tuje tushitakliwe ama tutakuwa kuwalipa *share* hawa wachina? Tunataka kujua katika Mpango huu tuje tuelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nataka nimalizie suala la utawala bora. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* hapa, aje aeleze huo utawala bora tunaoufuata ni wa aina gani? Kwa sababu bila utawala bora hata huo Mpango hautafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana, katika Jimbo langu, juzi watu wameshukiwa wanafanya Magendo ya Karafuu

bila kukamatwa na bidhaa yoyote. Cha kushangaza wamekamatwa, wamepigwa mpaka mimi nikawajibika kwenda kuwaomba polisi kwenda kuwafanyia matibabu. Jambo hili haliwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana Wizara au Serikali itueleze kwa uyakini kwamba utawala bora umekaaje ili kusiwe kuna kunyanyasa wananchi. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mohammed Issa, nilimtaja Mheshimiwa Tumaini Magessa, Mheshimiwa Tabasam Mwagao ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii tena nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii aliyonipatia ya kuchangia katika Bunge hili leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kukubali mpango wa kuirejesha tena Tume ya Mipango. Kwa sababu huko nyuma ilikuwepo, ikaunganishwa na baadaye imerudishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema sana juu ya Tume ya Mipango kwamba, itakwenda ku-*centralize* mipango yetu na sasa itajulikana nani anatakiwa kufanya nini na wakati gani. Nawapongeza sana Mawaziri wote wawili, Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha. Waziri wa Mipango kwa kutuletea Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2024/2025 lakini Waziri wa Fedha kwa kutuletea mwongozo unaotuonesha ni nini kitakwenda kuingia kwenye Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Mkatibu Wakuu, Mtendaji Mkuu wa Tume ya Mipango na uwasilishaji mzuri uliofanyika kwenye Bunge hili. Pamoja na pongezi hizi, yako mambo mengi ambayo yamesemwa katika hotuba hii. Iko mipango mikubwa imeoneshwa kwenye hotuba hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kujikita kwenye Fungu namba 57 ukurasa wa 27 kinachosema kwamba, Mpango

huu utathibitisha Maendeleo ya Kweli yanatokana na Mpango mzuri na nidhamu ya utekelezaji wa mipango hii. Kwa hiyo, kuna hoja ya Mipango na nidhamu ya utekelezaji na hapa ndipo kuna changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki nzima tumekuwa tunaongelea habari ya CAG, ni hoja tu ya nidhamu ya utekelezaji kwamba kuna mahali fulani kwenye nidhamu hatufanyi vizuri sana. Mipango tunayo lakini hatutekelezi vizuri kwa sababu nidhamu yetu iko chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kifungu namba 35 ukurasa wa 26, Waziri wa Mipango alitoa Mfano wa Ndugu yangu Lee, kiongozi wa Singapore. Anasema, uwepo wa Mfumo wa taasisi nzuri ni muhimu na inasaidia lakini muhimu zaidi ni kuwa na watu wazuri katika kuendesha mifumo na taasisi ya Serikali. Sasa, hoja yangu hapa pamoja na kwamba aliitoa kama *quotation*, hawa watu wazuri tunao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa tuliyonayo ni kwamba, tuna mifumo na taasisi nyingi za Serikali lakini na changamoto ya watu wazuri kama inavyoonekana hapa. tumekuwa tunafanya *vetting* kila mwaka kwa viongozi mbalimbali lakini baada ya muda tunajikuta kwenye tatizo kwamba, mtu mmoja anaonekana hajafanya vizuri na CAG anatuambia kwamba huyu hajafanya vizuri ameiba bilioni 18, huyu amesababisha *loss* ya kitu fulani. Kwa hiyo, watu wazuri hatuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu sasa, ni ombi langu kwamba, upande wa elimu watu wa elimu waingize elimu bora ya uraia na uzalendo. Maana inaonekana uzalendo ndani ya nchi hii ni tatizo. Kila anayepewa nafasi anafungua mdomo kwa ajili ya kula badala ya kufungua mikono ili atufanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana hili. Tunapokwenda kwenye mipango yetu, watu wa elimu wahakikishe kwamba, mitaala hii ambayo inakuja hivi karibuni inaweza kutufanya kwenda hatua moja mbele kwenye elimu ya

uraia na uzalendo ili huu wizi na vurugu zinazotokea hadi Wabunge wamefikia mahali fulani wanafikiria kuwaondoa watu kwenye uso wa dunia, maana yake wanyongwe. Kabla hatujakwenda huko tuwape elimu. Pia tukishawapatia elimu tunajua kuwa matokeo mazuri yatakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sana, kiongozi aliyepewa *responsibility matrix* yake, amepewa nini anachotakiwa kufanya, amepewa *KPI* yake, vilevile amepewa *milestone* yake kwamba kama amepotea njia anaweza akajua huku ninakokwenda siko, aende huku. Unashangaa anachokifanya ni kitu ambacho hakuambiwa kwenye ile *responsibility matrix* yake. Tuna kitu cha kufanya maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa yale ambayo yametekelezwa katika mipango iliyopita. Tunaiona *SGR* ikiwa sasa inakwenda *Lot one* iko kwenye hatua nzuri na sasa tunakwenda karibu *Lot Five* huku. Vilevile, tuna habari ya umeme vijijini ambayo inaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, ukiangalia umeme, mchangiaji aliyepita amethibitisha wazi. Nimewahi kufanya kazi viwandani, kama umeme wa kutosha haupo uchumi wetu wa viwanda utadorora kabisa. Hata kama tutaonekana tunapambana kwenye zile hatua nyingine, kama uchumi wa viwanda haujakaa vizuri kwa sababu ya umeme hatuwezi kutoboa. Tutafika mahali fulani tutashindwa tu. Gharama ya kutumia mafuta kuendesha viwanda inaomndoa kabisa ile *net profit* ya kiwanda, kwa hiyo, niwaombe sana kwenye hii habari ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye umeme utagundua kwamba, tuna umeme wa maji *megawatt* 574. Mpaka sasa tuna umeme wa gesi *megawatt* kama 1198 hivi, lakini tuna umeme wa mafuta kama *megawatt* 94.58. Tuna Tungamotaka *megawatt* 10.5, huu ambao uko gridi karibu *megawatt* 38, ukiangalia unaona karibu *megawatt* karibu 1.9 hii *storage capacity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi ukienda kuangalia wanachozalisha watu wa umeme, ni asilimia 50 ya hiyo. Maana yake kwenye Mpango huu tunahitaji kuweka fedha ili hiyo mitambo iliyosimama ikafanye kazi, viwanda vyetu vitembee. Wanasema wameona kabisa *maximum demand,* yaani umeme wa juu unaotumika kwenye nchi hii kwa Mwezi Agosti, ni megawati 1800. Ukienda kwenye ukweli, tukiwasha migodi yote, tukawasha kwa wananchi wote ambao tumewawekea umeme tutahitaji karibu megawati 5000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaponhgeze kwamba Bwawa la Nyerere litaingia hivi karibuni. Lakini pamoja na kuingia kwa Bwawa la Nyerere, sisi tumesema malengo yetu tunahitaji megawati 10000 kwa ajili ya nchi hii kuanza kuyaona maendeleo. Niombe sana mipango yetu ya umeme iendelee kuwepo na hawa wapewe fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ripoti hii utagundua kwamba, mauzo yetu ya nje ya madini mwaka 2022 yalitoka dola bilioni 3.1 mpaka dola bilioni 3.4. Vilevile, ikaonekana kwenye mauzo ya nje, madini wamefanya vizuri kwa asilimia 56 kwenye mauzo yote ya nje. Kwa hiyo, nilitegemea hapa kwenye madini twende kuhakikisha kwamba tunaingiza fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko *vision* ya Mheshimiwa Waziri 2030, inayosema kwamba madini ni utajiri lakini vilevile inaonesha kwamba itatuletea ajira za kutosha. Hii *vision* aliyoisema inahitaji kuingiza utafiti *GST* unaoitwa *High Resolution Airborne Geophysical Survey* ambao haujafanyika kwenye nchi hii. Umefanyika kwa asilimia 16 tu. Kwa hiyo, tunategemea kwenda asilimia 50. Niwaombe sana kwenye hili kwamba, huu utafiti upewe fedha na hii ifanyike ili twende kwenye asilimia 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukajua kwenye asilimia 16 tumepata dola bilioni 3.4. Je, tukifanya asilimia 50? Kama tumekwishaona haya mafanikio, basi haya mafanikio tuyaongezee nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, kule kwangu wanachimba madini. Maeneo yote yanayoleta haya madini, barabara zake ni mbovu. Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri anayeshughulika na barabara (ujenzi wa miundombinu), katika nafasi hii tuliyonayo sasa ya kutoa mapendekezo kwenye hili, zile barabara zijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeisema sana barabara ya kutoka Geita kwenda Kahama, inapita kwenye migodi katika majimbo matatu. Hawa watu wanabeba *Carbon*, hawa watu wanabeba magogo, hawa watu wanabeba *selenide***,** ili waongeze kwenda na kurudi kwa urahisi ni lazima watengenezewe barabara ili wazalishe mara tatu ya hiki ambacho leo tunakiona leo. Kama hatutafanya hivyo maana yake uzalishaji wetu hautapanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara inatoka pale kwangu Katoro kuelekea Jimbo la Bukombe, linapita kwenye migodi zaidi ya sita hadi saba. Niombe sana barabara hii itengenezwe. Haitengenezwi kwa ajili ya kuwafurahisha wale watu. Inatengenezwa ili iweze kuwafanya wale watu wafanye kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kilimo, mwaka 2022 tumetenga zaidi ya bilioni mia tisa tisini na kitu lakini tunaona kabisa sekta ya kilimo cha umwagiliaji imekwenda kutoka hekta 300 mpaka hekta 800. Lengo letu ilikuwa ni hekta milioni 1.2 bado kuna 400 bado hatujaifikia kwa miaka hii mitano. Niwaombe sana kwenye utekelezaji wa bajeti hii, kwenye mapendekezo yangu fedha ipatikane ya kuongeza kwenye eneo hili la umwagiliaji ambalo linaajiri watanzania wengi ili waweze kuchangia pato la Taifa kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ninayotoka mimi kuna Ziwa Victoria lakini maji yake hayajatumika. Yakitumika ninaamini tutazalisha kuliko inavyoonekana leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii katika kilimo hiki hiki ambacho tunakiona kama ni cha mchezo mchezo, inaonekana tulizidi kwa asilimia 124. Kwa hiyo, tulizidi. Maana yake ni kwamba,

tukiwawezesha zaidi tutapata hata asilimia 200. Kwa kuwa kilimo ni biashara sasa itatufanya hawa watu wetu watakula na tutauza mazao yetu nje. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana…

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya uvuvi. Ndugu yangu Jirani hapa Mheshimiwa Mwijage asubuhi alisema kwamba, mpaka sasa uvuvi wa vizimba tuna *metric* tani 18000, wenzetu wa Uganda wana *metric* tani 120000. Egypt wana tani milioni moja kama na laki mbili. Nilikuwa nafanya hesabu ya kawaida tu. Leo tukiweka tukawa na *metric* tani milioni moja, tunauwezo wa kutengeneza trilioni tano kwa mwaka. Trilioni tano hii itakwenda kufanya kazi kubwa, tunaogopa nini kwenye *potential* kubwa ya uvuvi kuingiza fedha. Tunaogopa ni kwenye *potential* kubwa ya mifugo kuingiza fedha? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tumaini Magessa, muda wako ulikuwa umekwisha. Naomba tafadhali umalizie.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tumaini Magesa. Nilimtaja Mheshimiwa Tabasam Mwagao, Mheshimiwa Maimuna Mtanda na Mheshimiwa Jumanne Kishimba, wajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Mpango huu wa Serikali.

Kwanza, nataka niwaeleze wananchi kwamba, Chama Cha Mapinduzi katika Ilani yake ya Uchaguzi wa mwaka 2025, Mheshimiwa Rais kama alivyojua yaani nafikiri kwenye maono yake akaona Mheshimiwa Kitila Mkumbo anafaa kuwepo hapo katika sehemu ya Mpango, ndiyo Mwandaaji. Ndiyo aliyeandaa hii Ilani ya Uchaguzi halafu leo ndiyo amewekwa kwenye mpango, baba ukitufelisha tumekwisha na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, Chama Cha Mapinduzi ni chama cha kijamaa. Vilevile viongozi wake wote ni wajamaa lakini sisi tunafuata Sera za kikomunisti. Kwa hiyo, hauwezi kumtenganisha Mheshimiwa Rais na ukomunisti wa ujamaa. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais ana dini na imani tena kwa mapenzi makubwa kwa wanachi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, sisi ambao tumemtanguliza Mheshimiwa Rais mbele na sisi tuko nyuma yake, sisi pia ni wajamaa lakini pia ni wakomunisti. Sasa, mimi hapa kama Tabasamu hauwezi ukanitenganisha na ukomunisti.

**MHE. DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam kuna taarifa. Mheshimiwa Dkt. Bashiru.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachangia vizuri sana Mheshimiwa Tabasamu. Namuomba radhi ni mara ya pili nampa Taarifa katika maisha ya Bunge hili. Sisi ni wajamaa siyo wakomunisti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasamu, unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiunga mkono mimi mjamaa, sasa nikikataa kwamba siyo mjamaa, itakuwa ni hatari sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba sisi wajamaa tunapekea sana miradi na huduma za wananchi kule kwa wananchi. Ndiyo maana ya Sera ya Chama Cha Mapinduzi. Ni kwenda kuwasaidia wananchi wake kule chini. Sasa, Mheshimiwa Profesa Kitila nakuamini kwa kuandika, wewe ni Profesa. Vilevile wewe ni Mwalimu wangu. Kwa hiyo, sina shaka na wewe. Kwa hiyo, siwezi ku-*doubt* mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu yangu ni kwamba, tuna vijana zaidi ya milioni 20 katika nchi hii, vijana wenye ajira ya kazi, wenye uhakika wa ajira rasmi hawazidi 300000 mpaka 600000. Sasa, huu Mpango wako uje na kuondoa tatizo la hawa vijana kukosa ajira. Lakini vijana wa Kitanzania hawana shida, wakitengenezewa mahala pa kufanya biashara na kufanyia kazi, wako tayari kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Rais mwaka 2022 alielekeza yajengwe masoko ya Machinga kuanzia kule kwenye ngazi za halmashauri mpaka ngazi za kata. Mheshimiwa Waziri, ninaimani wewe ni bingwa kabisa wa kuandika. Hivi ukitengeneza yale magulio yakapata nafasi wale vijana wakaanza kufanya biashara zao kule, mbona tungepunguza sehemu kubwa ya ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Chama Cha Mapinduzi tulisema tuna ajira milioni 10. Ninaimani unaweza ukatengeneza ajira milioni 15. Sasa tunachokuomba, kwa mfano Sengerema inazungukwa na ziwa kwa asilimia karibu 72, asilimia kama 30 hivi ndiyo nchi kavu. Sasa, siyo Sengerema peke yake, Buchosa, ukichukua Geita vijijini, ukichukua Ukerewe, ukichukua Magu, Bunda mpaka Musoma moja kwa moja mpaka Tarime huko. Maeneo haya yote ukija ukachukua hiyo Kagera mpaka Chato, maeneo haya yote tunaweza tukafuga Samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wanaofuga Samaki na kuzalisha Tani za Samaki wanategemea maji yanayotiririka kutoka kwenye Ziwa Victoria kupitia Mto Nile. Sasa, tulikuwa tuna uwezo wa kupeleka vijana Misri au tuwachukue Wamisri waje huku tuwape vizimba wawekeze na tuwape kwa gharama nafuu kabisa ili watu wetu waje kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wamisri wakija, wafanyakazi wao watakuwa ni watanzania. Sasa, andikeni maandiko muwakaribishe wamisri tuje tufuge Samaki ndani ya Ziwa Victoria. Mheshimiwa Mkumbo, hili kwako siyo tatizo.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Cherehani.

**TAARIFA**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumpa taarifa mzungumzaji kuwa, wenzetu Misri pia walitengeneza ziwa la kutengeneza na wanafuga samaki vizuri, pia linasaidia mambo mengi ikiwepo umeme. Kwa hiyo, sisi sasa hivi kipindi hiki cha masika maji ya mvua yanapotea, kwenye madaraja yetu maji yanapotea. Tunauwezo wa kutengeneza benki ya maji ya mvua katika kipindi hiki cha masika.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeikubali hiyo taarifa.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante. Endelea Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ufugaji na uvuvi. Huko kwenye ufugaji tungeunda Mamlaka ya Uvuvi, Mamlaka ya Mifugo. Nasema kama tutafanya kama walivyofanya *TARURA* na *TANROADS* yaani maeneo yote ambayo yameundiwa *authority* yote yanafanya kazi vizuri sana. Tungekuwa tuna Mamlaka ya Mifugo ingesimamia Minada, ingesimamia zahanati kule za mifugo, ingesimamia mambo mengi, uzalishaji wa nyasi mambo yote mazuri yangefanyika kule, lakini kule kwenye Uvuvi pia tungesimamia mambo mengi makubwa tukazalisha. Tunakwama wapi katika Mpango kuweka suala la Mamlaka katika huu Mpango na Mamlaka ya Mifugo na Mamlaka ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la huduma za afya. Hapa kwenye Mpango mimi nimeona kwamba tumeboresha na tunapanga kuboresha huduma za afya, lakini kama hatutatafuta wawekezaji wakaja kuweka madawa kuweka viwanda vya kuzalisha dawa nchini, ni kwamba tu madawa peke yake, tunanunua dawa nje ya nchi asilimia 85, asilimia 15 ndio inayozalishwa nchini. Jamani hata *syringe* tu ya kuchoma sindano miaka sitini ya Uhuru hatuwezi kutengeneza Kiwanda cha *syringe* tu ya kumchoma binadamu, shilingi mia na yenyewe tunaagiza kutoka Korea, tunaagiza kutoka India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawa Wahindi kule kwao wana dawa za gharama nafuu, dawa zao ni za gharama nafuu sana, kwa nini tusiwafuate Wahindi wakaja kuweka viwanda hapa Tanzania, tukakubaliana wasilipe kodi lakini tupunguze nakisi ya kuagiza madawa nje ya nchi. Hili naliomba sana kwenye Mpango Mheshimiwa Profesa Mkumbo aliweke pale ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la mitambo ya maji, mitambo ya maji tumenunua mitambo ya maji mingi sana hii mitambo ya maji kweli kama ilivyokuwa inazungumzwa hapa na Mheshimiwa Monni, Mbunge wa Chemba kule, alizungumza akasema mitambo hii imesimama. Ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Mkumbo hata mimi kwangu Sengerema hii mitambo ipo, nina visima 39 sijui vimechimbwa viwili tu, hii mitambo imesimama, imekosa mafuta. Ukiwauliza wanakuambia hakuna mafuta. Kama tumeweza kununua mitambo ya karibu bilioni 250, Serikali inaweza ikakosa mafuta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno siyo sahihi, tujue tatizo ni nini kwa sababu Serikali haiwezi kukosa Wazabuni wa kufanya kazi hii. Kwa hiyo, tunaomba kwamba aje na majibu mazuri tu. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kutuletea mitambo, Mheshimiwa Rais kununua hii mitambo alikuwa na nia njema sana katika nchi hii. Sasa tunawaomba tu, hii mitambo kwa nini isimame kwa sababu ya kukosa mafuta, ifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho ni suala la Mkataba wa Bandari, Mkataba wa Bandari huu tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake, lakini tuliomba hawa Dubai *World* pia wangepewa Gati la Mafuta kwa sababu kule ndio ingerekebisha ile mifumo ya uzalishaji wa mafuta, wakatujengea *hub* na matenki tumezungungukwa na zaidi ya nchi nane, wanategemea hapa kwetu. Sasa tunaomba sana, kwamba tungerekebisha mifumo ya ushushaji wa mafuta, angalau hata meli zenye *metric tons* 500,000 zishushe mafuta kwa muda mfupi na tupate *storage,* matokeo yake gharama za mafuta katika nchi hii zitapungua. Tunaliomba sana hilo Mheshimiwa Mkumbo aliweke katika mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii tunamwombea sana Mheshimiwa Rais apate maisha marefu sana, mpaka kijijini kwangu sasa hivi kuna watoto wanazaliwa wanaitwa Samia, inaonekana wananchi wamemkubali sana Mheshimiwa Rais katika jambo hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam Mwagao, nilimtaja Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mheshimiwa Jummane Kishimba na Mheshimiwa Emmanuel Shangai, aliandae.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini pia nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa haya ambayo amekuwa akiyatenda. Kwa kweli anatupeleka kuzuri na sisi wote ni mashahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze wote waliotuletea Mpango huu, Mawaziri wote pamoja na Wasaidizi wao, Mpango ni mzuri na nianze kwa kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Mpango kuna mambo mbalimbali na shabaha nyingi zimewekwa, lakini naanza na ile ya elimu, nimeangalia kwenye Mpango wa 2024/2025 ambapo kiashiria kimojawapo kinasema ni viashiria vya maendeleo ya watu, lakini kwenye shabaha inasema kuchochea na kuboresha ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizidi kusoma zaidi kwenye Mpango kumeonesha namna ambavyo kule nyuma tulikotoka kuanzia 2012 hadi 2022 udahili wa wanafunzi ulivyoongezeka kwenye Nyanja zote kuanzia Elimu ya Msingi udahili umeongezeka kutoka asilimia 94.6 hadi asilimia 113.2 mwaka 2022, hiyo ni kuanzia mwaka 2012. Kadhalika na sekondari tunashukuru sana udahili huu umeongezeka kwa sababu ya jitihada mbalimbali ambazo zimefanywa na Serikali inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia uwekezaji katika Sekta ya Elimu ni mkubwa sana, ujenzi wa vyumba vya madarasa umeongeza, maabara zimeboreshwa, ujenzi wa mabweni lakini pia elimu msingi bila malipo bado inaendelea kutolewa hadi leo. Kwa hiyo ni kiasi kikubwa sana cha fedha ambacho kinaenda kwa ajili ya kuimarisha Elimu yetu kuanzia ngazi ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo kwa sababu uwekezaji kwenye Sekta ya Elimu ni mkubwa, tunategemea *outcome* ya wanafunzi hapo mbele na wenyewe waje wanafunzi ambao wameiva ukizingatia kwamba kuna kuchochea na kuboresha ubora wa elimu. ubora wa elimu ni pamoja na kuwa na Walimu wa kutosha ili kuweza kufundisha vizuri na wanafunzi wapate elimu bora mwisho wa siku Taifa liwe na kile ambacho tulikusudia tukawekeza kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwenye Mpango wetu sijaona, nashukuru kwamba zipo ajira ambazo huwa zinatolewatolewa, lakini kwa uwekezaji huu lazima tuwe na mkakati wa dhati wa kuhakikisha Walimu wanapatikana watakaoenda sambamba na idadi ya wanafunzi tulionayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wanahangaika ukienda shule za pembezoni hakuna Walimu, Walimu ni wachache sana kiasi kwamba wanafunzi wengine anaenda anamaliza siku hapati Mwalimu, kesho anarudi tena, anakosa Mwalimu, inasababisha pia hata utoro, Kwa hiyo ili kudhibiti hali hii lazima tuwe na mkakati wa dhati utakaoendana sambamba na uwekezaji ambao Serikali imekuwa ikifanya katika Sekta ya Elimu, lakini pia tuwapunguzie wazazi mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchache wa Walimu, wazazi wengi sasa hivi wamekuwa wakilipia Walimu wao ili wawafundishe watoto wao. Kwa hiyo kulipia kunamwongezea mzazi gharama ya Elimu, kwa hiyo niombe sana Serikali ili tupate *output* nzuri ni lazima tuwekeze na uwekezaji hatuna kwa kukwepea lazima tuajiri, tuweke mikakati ya dhati katika kuajiri Walimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimeliona katika kupitia Mpango wetu ni upande wa kilimo. Naomba ninukuu kwamba; "Kuanzia huko nyuma hadi kufikia mwaka 2000 mauzo ya bidhaa zetu kwenye kilimo, mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi yametawaliwa na usafirishaji wa malighafi bila kuongezea thamani. Hali inayosababisha ukuaji wa uchumi kutoendana na kasi ya kupunguza umaskini na ajira hususani vijijini."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nime-*base* tu kwenye kilimo, hili ni la kweli, lakini niishukuru Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu imeendelea kuboresha Sekta ya Kilimo kwa namna mbalimbali, lakini hili la kuongeza thamani bado tunatakiwa kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao yetu ni kweli kabisa tunasafirisha au tunauza yakiwa ghafi hali ambayo inatupunguzia sana mapato Serikalini lakini kwa Mwananchi mmojammoja na hali ya umasikini sasa imeendelea badala ya kuwa inapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, kwa sababu thamani hii tutaipata kupitia viwanda vidogovidogo vingi, hivyo, Serikali ijikite katika Mpango wa namna ya kufufua viwanda ambavyo vimekufa hususani Viwanda vya Korosho. Ukienda kwenye maeneo mbalimbali yanayozalisha korosho mathalani ukienda Mtwara, Newala na Masasi kuna Viwanda vya Kubangua Korosho vilijengwa huko nyuma. Sasa hivi vile viwanda havifanyi kazi matokeo yake bado tunauza korosho ghafi ambazo hazina afya sana kwa mkulima. Kwa hiyo niombe sana ufufuaji wa viwanda vyetu ufanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali pia upande wa kilimo kwenye zao la korosho wamekuja na mpango wa kujenga Kiwanda kikubwa cha Korosho, *industrial park* kule Nanyamba, lengo la kiwanda kile ni kuhakikisha kwamba korosho zitakazozalishwa zinaenda pale zinabanguliwa, tunasafirisha sasa na kuuza korosho ambazo tayari zimeshaongezeka thamani. Kwa hiyo ni mpango mzuri ambao kama utasimamiwa sawasawa utatutoa sisi hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masikitiko yangu tu kidogo ni kwamba naona kuna changamoto, pamoja na Mpango mzuri wa Serikali kujenga kiwanda hiki, uzalishaji wa zao la korosho unazidi kupungua, kwanza namshukuru Mheshimiwa Rais kwamba ametuletea pembejeo, ambazo wakulima wamezitumia lengo lilikuwa kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametangulia hapa Mheshimiwa Mhata, ametaja mwaka 2021 Tanzania nzima tuliuza tani laki tatu, lakini 2022 tani laki moja na themanini na mbili, mwaka huu hatujui tutauza tani ngapi? Sasa najiuliza tu peke yangu kwamba tumeshaweka mkakati wa kujenga kiwanda kikubwa pale Nanyamba kwa ajili ya korosho, sasa tusipofanya utafiti wa kubaini ni nini kinaangusha au kinaporomosha zao letu la korosho nadhani kiwanda kile hakitaleta tija ile ambayo tulikuwa tunaifikiria. Tukumbuke kwamba ni uwekezaji mkubwa sana ambao umefanyika, kwa hiyo niiombe sana Serikali, kwenye Mpango huu tuweke kipengele cha kufanya utafiti wa anguko la zao la korosho. Iwepo kabisa, ili tukishafanya utafiti tukagundua, basi uwekezaji wetu utaenda vizuri kama vile ambavyo tunatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunaweza tukafanya utafiti, lakini akina nani watashuka kule chini, niombe pia mkakati wa kuajiri Maafisa Ugani ambao wataenda kufika mpaka ngazi ya vijiji kule chini ili kuinua uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo uwekezaji wa viwanda ambao tunao utaleta tija kwa Taifa lakini pia utainua uchumi wa mkulima mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kwenye kipengele cha Sekta ya Usafirishaji hususan reli ya kusini. Usafirishaji ndio ndio uti, tunaweza tukalima, tunaweza tukavuna, tunaweza tukafanya chochote, kama hatuna *means* nzuri ya usafiri, mazao, madini na bidhaa zozote hazitafika kule ambako tunatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba Serikali imewekeza sana kwenye Bandari ya Mtwara, zaidi ya bilioni 168 zimewekezwa Bandarini, lengo Bandari ile ifanye kazi vizuri ili ilete

tija kwa Taifa hili. Nasikitika tu kwamba pamoja na kuweka kule sijaona kwenye Mpango ujenzi wa reli hii ya kusini. Leo hii ukienda Mtwara makaa kutoka Mchuchuma kule Liganga yanasafiri kwa njia ya barabara yanaharibu barabara kiasi kwamba tutakuwa tunatengeneza kila siku. Kwa hiyo niwaombe sana wenzetu wa Wizara kwenye Mpango huu tuwe na mkakati wa dhati wa kujenga reli kutoka Mchuchuma na matawi yake ya Liganga hadi Mtwara ili tuweze kusafirisha bidhaa kwa kupitia reli na kupunguza uharibifu wa barabara ambao unajitokeza siku hadi siku.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi, lakini pia niendelee kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Jumanne Kishimba, Mheshimiwa Emmanuel Shangai na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, ajiandae.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye mjadala wetu huu wa bajeti yetu ya mwaka ujao. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Rais, Waziri wa Fedha na Waziri wetu mpya wa Mipango na *crew* nzima ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikifuatilia mijadala iliyokuwa ikiendelea hapa kati ya Waheshimiwa Mawaziri kwenye mjadala wa *CAG* na Waheshimiwa Wabunge, kitu kimoja kinanipa shida kidogo ni kwenye suala hili la Mikataba. Sitaki kuongelea mkataba wa *DP World* maana yake wenyewe umekwishamalizika, naongelea hii Mikataba mingine ambayo inasemwa kwamba Mikataba hii itakuwa ni siri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kujiuliza, ni kweli ndoa inakuwa siri lakini talaka na ugomvi wa talaka wa ndoa unakuwa wazi. Sasa ni kweli Mkataba unakuwa wa siri, huyu kesi ikianza kesi inafanyika hadharani na kila kitu kinaletwa wazi, sasa maana ya

huu usiri ni nini hasa na nani alileta hii *proposal* ya Mkataba uwe siri? Aliuleta mwekezaji au ni Serikali ndio ilitoa huo muundo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili neno kwa sababu naona nusu ya mgogoro uliokuwepo hapa ni Suala la Mikataba na *penalty* zote na riba zote zinazolipwa ni kwa sababu mikataba yote inaonekana ni siri. Sasa kama mikataba ni siri basi na kesi ziwe siri. Leo tunamwona Profesa Mruma kesi inaendeshwa hadharani, lakini Mikataba ile ilikuwa siri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda Mheshimiwa Waziri wakati wa kufanya majumuisho, ajaribu kutueleza nini hasa kinachosababisha iwe siri. Maana yake ukitaka kwenda kuwekeza kwenye nchi yoyote duniani unapata *data* za kila aina ya uwekezaji ulioko pale, labda kama unataka *special case* ndio unakwenda sasa kuongea na Waziri au Baraza la Mawaziri au Kamati ile, ndio unasema bwana mimi kwa masharti yenu haya naona labda kipengele A, B, C, D naomba kirekebishwe lakini kama hakuna marekebisho mengine yoyote sioni sababu Mikataba yetu kuwa siri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango ni mzuri sana, lakini hofu yangu ni kwamba hauendi kwenye yale maisha kabisa ya kila siku ya wananchi. Wananchi wanachohitaji ni kile ambacho kinawagusa, leo sisi kwenye maeneo yetu ya Kanda ya Ziwa na maeneo ya Tabora kuna maeneo ya hifadhi ambazo hazina hata nyani, wala hazina tumbili, wala hazina kitu chochote lakini kuna dhahabu mle ndani na almasi na ziko labda kilomita saba, kwa nini Wizara ya Maliasili kama yenyewe inapenda miti, iruhusu watu wahamishe ile miti, ihamishiwe sehemu nyingine ili watu wachimbe dhahabu zile. Haiwezekani tukachorewa michoro na Wazungu, tukafa njaa eti pale pana dhahabu si ndio lakini wewe unakatazwa kwamba huwezi kuchimba kwa sababu kuna miti. Kwa nini miti ile isihamishwe?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasamu.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Kishimba kwamba sheria zinazotumika kwanza hizo za hifadhi ni sheria za mwaka 47, Mjerumani, akaja tena Muingereza, halafu na sisi tukapata uhuru. Sasa kwa nini tusitumie sheria zetu za wakati ambapo tumepata uhuru? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jumanne Kishimba unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yeah* ninaipokea. Ndiyo maana nimesema ndugu zetu wasomi tuleteeni pia mawazo kabisa ambayo raia anaweza akakutana nayo mtaani kuliko huu ustaarabu mwingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana sana Mheshimiwa Waziri wa Afya kwenye suala la bima ya afya, lakini tunaiongea bima ya afya kwa maongezi rahisi kwa ajili ya maisha yetu sisi yalivyo ni mazuri. Jana, mtoto wa ndugu yangu kapata ajali kule Mwanza, amefika Sekou-Toure anaambiwa kupimwa kwenye *scan* anahitaji shilingi elfu sitini, mtandao hauendi, mpaka tunalia na Daktari kwamba bwana mpime pesa tutatuma, anakataa na mtu karibu anafariki. Bahati nzuri mtu amekimbia pale amekwenda kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo napigiwa simu toka kijijini, uzuri Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Kitila ni watu wa Singida. Leo humu hata kwenye Mpango hawajasema nyoka au mbwa, je, wakimuuma mtu huwa ni ajali au yenyewe inaitwa nini? Maana yake ukifika umeumwa na nyoka unaambiwa ulipe shilingi elfu 60 na ukiongea na mtu anakwambia huyu alienda kuwachokoza nyoka kule shambani. Huyu mtu kazaliwa Dar es Salaam. Nafikiri wangeangalia kabisa suala la kwamba, je hawa watu tunaohudumia ni Watanzania wa aina ipi? Msisemee tu habari ya mbolea sijui habari ya nini, hapana, wasemee maisha yao kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukiwa una wezi, hata kama wamekuja wezi wa kuku, ukipiga simu au yowe zinakuja *defender*

nne au tano za Polisi, lakini polisi wale watamkata huyu mtu au hakupatikana wataondoka, gharama ni karibu shilingi laki mbili. Leo mtu anaumwa amekwenda hospitali hana pesa, haya mtu wa msamaha amemsamehe kweli hakuna shida, lakini hakuna dawa pale hospitali, lakini pale *pharmacy* dawa zipo, anafanyaje kati ya hospitali na *pharmacy*. Huyu mtu atakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha aeleze kwamba mtu kama hana pesa na wale hospitali hawana dawa, huyu mtu aende polisi aje na polisi mpaka *pharmacy* anywee dawa hapo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo wananchi wanayohitaji, hizi blaa blaa zote, hakuna mwananchi anayehitaji. Tuweke kitu ambacho kiko *practical* wazi, kwamba mimi kama naumwa sina pesa, nafanya nini hasa? Kweli msamaha nimepata, lakini wale pale hospitali walionipa msamaha hawana dawa, kwa nini huyu mtu wa msamaha tusiondoke naye mpaka Polisi, Polisi wanidhamini ile dawa wapige picha *WhatsApp* waitume Wizarani, si wana mafungu ya maafa. Sasa hayo mafungu ya maafa huwa yanatumika namna gani au maafa maana yake nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake hiyo mifumo kama tumeirithi toka kwa wakoloni, matokeo yake inatutesa, inatutesa. Leo hii wanakusanya pesa kwenye njia ya *M-Pesa*, kwani kwenye *M-Pesa* pesa haramu huwa inarudishwa? Mtu akituma pesa ya uwizi au rushwa kwenye *M-Pesa* ina *legality*? Ameuza gongo si akutuma kwenye *M-Pesa* inapokelewa na ushuru wanakata. Sasa wanakataaje kumtibu mtu? Kama ni watakatishaji, basi mtakatishaji wa kwanza atakuwa Serikali. Maana si ndio Mheshimiwa Mwigulu, yeye ndiye anapokea pesa zote kwenye miamala, miamala imewahi kurudisha pesa, kwamba pesa hizi hatuzitaki kwa sababu ni haramu? Inapokea pesa zote na inachukua na ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najaribu kulieleza neno ambalo linawagusa wananchi. Sisi tunaowakilisha hayo yote wanayoongea wala hawana habari, wanachotaka ni kwamba huu uhuru tulioutafuta, nikiwa leo naumwa naweza kusimimamiwa

na Mwenyekiti wa Kijiji nikatibiwa na Serikali ikatambua hilo? Ndicho wanachotaka na dhamana ikawa ni mimi mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kumalizia tu, sisi leo tuna matatizo sana kule kijijini, leo ukipata kesi unatakiwa udhaminiwe na mtu ambaye ni mwajiriwa wa Serikali, lakini unakataaje mtu wa ng'ombe, ana ng'ombe kunidhamini mimi. Je, mimi nina ng'ombe 200 unakataa kweli mimi nisimdhamini mtu kwenye kesi? Ng'ombe, sisi ndiyo tunatumia kuoa mke. Huwezi kwenda kuoa kwa kutumia friji wala *TV,* huyu mtumishi wa Serikali anamiliki *TV* na friji, unamkataliaje mwananchi mwenye ng'ombe kudhamini mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo, hivi vitu vyote tumerithi ni vya mkoloni, waendelee kuwafanyia urahisi wananchi ili wananchi waanze kuona kwamba kweli sasa tuko na Mama. Mama Samia anataka vitu kama hivi ili wananchi wa-*feel* kweli kwamba wako huru hata. Kama hana maji ya kunywa na wanawakopesha wanakataaje kumkopesha mtu dawa? Kwa nini unakataa? Umeme unanikopesha, maji unanikopesha nitalipa mwisho wa mwezi, wewe unakataa kunikopesha dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mchango huo naendelea kumshukuru tu Mheshimiwa Rais hasa kwa suala hili la bima ya afya. Baada ya hapo nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumanne Kishimba. Nilimtaja Mheshimiwa Emmanuel Shangai, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na Mheshimiwa Mariam Nyoka wajiandae.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Mapendekezo wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2024/2025.

Naomba niwapongeze Mawaziri wote wawili kwa kazi nzuri ya uwasilishaji wa hotuba zao ambazo zimesheheni mambo mazuri kwa Watanzania. Napenda kusema kwamba Nchi yetu

kwa miaka yote haijawahi kuwa na shida ya mipango. Tatizo letu kubwa ni namna tunavyotekeleza mipango tunayojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapanga vizuri sana tunaandika kwenye makaratasi vizuri sana. Leo mwananchi akisikiliza huko nje anadhani kesho kutakuwa kuna mto unatoa maziwa, lakini kwa jinsi tunavyotekeleza inakuwa ni tatizo. Leo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Profesa Kitila ukurasa wa 13 amesema kwamba; "Ili kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakuwa na athari chanya katika kuinua kiwango cha maisha ya watu wetu na kupunguza umaskini, mipango ya muda mrefu na mfupi ijayo itajikita katika kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi wetu unakuwa jumuishi, unapunguza umaskini, unazalisha ajira nyingi, unatengeneza utajiri na unachochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa dhamana nje ya nchi…" Katika aya ya mwisho amesema: "…kazo wa kipekee utakuwa katika kuchochea maendeleo kijamii na kiuchumi *or rural social – economic development*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite katika maeneo mawili, kwanza suala la elimu. Nataka baadaye Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo anapokuja atuambie ni namna gani tunaweza kuwajumuisha wananchi wa vijijini ili waweze kushindana na watoto wa mjini. Leo mtoto anayesoma Shule ya Msingi ya Samunge, Kata ya Samunge, Wilaya ya Ngorongoro anawezaje kushindana na mtoto aliyeko Dar es Salaam. Yule mtoto aliyeko Samunge yeye anategemea jua ili asome, lakini aliyeko Dar es Salaam yeye anategemea jua na wakati huo huo anategemea umeme. Nadhani ni vizuri tujikite kuangalia katika suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni namna gani tunaweza ku-*balance* au kuweka sawia Walimu; Waziri atuambie kwenye mpango wake ni namna gani tunaweza ku-*balance* uwepo wa Walimu katika shule zetu za vijijini kwa sababu, leo tukiangalia kuna kipindi fulani Mheshimiwa Jenista alisema, ukiangalia kwenye shule za mjini unaangalia somo moja lina Walimu zaidi ya saba, somo moja mjini, lakini kule kijijini Mwalimu mmoja anafundisha zaidi ya masomo 12. Kwenye mpango wa

Waziri aje atuambie kwa sisi tuliopo kule vijijini, ni kwa namna gani tunaweza kupata watumishi ambao watawafundisha watoto wetu kule chini. Sambamba katika sekta zote kwenye afya pamoja na elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la mifugo. Sisi wafugaji tunategemea ardhi kwa kila kitu, lakini kumetokea tatizo kubwa sana hapa, *coordination* ya Wizara zetu. Kwa mfano, leo tunaweza tukawa na Wizara ya Maji, Wizara ya Maji anapeleka maji labda kwenye kata fulani, lakini pia mtu wa mifugo anataka ajenge josho, lakini wakati huo huo anaenda kujenga josho eneo ambalo hakuna maji na Waziri wa Maji ataenda kuweka mradi wa maji katika eneo fulani ambalo mifugo hawaogeshwi kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mpango wetu useme ni namna gani hizi Wizara ziongee, kwa sababu Wizara zikiongea itasaidia kutatua matatizo makubwa katika nchi yetu. Leo mtu wa Maji ni lazima aongee na mtu wa Mifugo, kwa sababu unaenda kutatua tatizo la maji ili kuogesha mifugo, tunahitaji maji, lakini mtu wa mifugo anaenda kujenga josho eneo ambalo hakuna maji, hiyo nayo ni *misplacement* ya *resources,* ni lazima tuzungumze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine Mheshimiwa Profesa natamani atuambie Mpango huu ni namna gani unaenda kutatua migogoro ya ardhi katika nchi yetu. Suala la migogoro ya ardhi limekuwa ni tatizo kubwa kwa miaka mingi. Mpango wa Waziri utuambie ni namna gani wanaenda kutatua migogoro ya ardhi. Leo ukienda kwenye wilaya nyingi za wafugaji kuna migogoro ya ardhi. Ukienda Longido kuna migogoro ya ardhi, Simanjiro, Kiteto na maeneo yote yanayozunguka hifadhi zetu kuna migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tukiangalia kwenye Wilaya yangu ya Ngorongoro, toka mwaka jana Serikali imetenga eneo la kilometa 1,500 wananchi wangu wameendelea kuumia kwa sababu hawana ardhi. Nataka Profesa akija hapa atuambie, mpango huu utaenda kuwasaidia hawa wananchi waweze kupata ardhi ya malisho kwa sababu hawana ardhi ya malisho mpaka sasa hivi. Kwa mfano kila siku hata leo kuna mifugo

imekamatwa zaidi ya 834, wapo na wananchi wanaenda kutozwa fedha, lakini mpaka sasa zaidi ya mifugo 2,082 wametaifishwa, ni kwa sababu wananchi hawana ardhi kwa ajili ya kulisha mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wafugaji wa kule kijijini tunategemea mifugo kwa ajili ya chakula, kwa ajili ya kusomesha watoto wetu, kwa ajili ya afya. Ni lazima sasa mpango huu uje utuambie hawa wananchi ambao hawana ardhi, kuanzia Ngorongoro ukienda *Lake Natron* ukienda maeneo ya Mara, wananchi hawa wanalia kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kwamba Mheshimiwa Rais wetu ana moyo wa dhati wa kuwasaidia wananchi na kuwaletea maendeleo, lakini tuangalie kwenye mipango yetu pamoja na Mawaziri wote, tuone namna ya kumsaidia kutatua changamoto zilizopo. Leo wananchi wa Ngorongoro wanasema angalau hata hao mifugo wakale tu kwa sababu hatuna namna, ni bora tufe polepole kuliko kufa kwa wakati mmoja, kwa sababu kama mwananchi unategemea mifugo kwa ajili ya chakula huna pa kulisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliambiwa hapa kwamba watu watachimbiwa maji, mpaka leo ni visima viwili na havitoi maji ambayo mifugo inatumia na ile mifugo ilikuwa inategemea maji kutoka eneo lile la kilometa 1,500 kwa ajili ya kupata maji. Walisema wataweka malisho hakuna, hakuna malisho ya aina yoyote sasa wale wananchi wataishije, mpango huu uje utuambie ni namna gani wanaweza kwenda kutatua changamoto za wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, kuna suala hapa wanazungumza, naomba mpango huu utuambie, je mpango huu unawahusu wananchi 100,000 wa Tarafa ya Ngorongoro ambao Serikali imewawekea vikwazo vya maendeleo kwa zaidi ya miaka miwili sasa. Hawapati maji, hawapati chochote. Mpango huu uje utuambie, Serikali ina mpango gani kwa ajili ya hawa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, …

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangai Kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge Shangai wa Ngorongoro juu ya hali ya tarafa yake ya Ngorongoro aliyoieleza, kwamba kutokana na urasimu ulioko katika Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro, hivi sasa kuna baadhi ya shule ambazo vioo vyake vimevunjika, vimepasuka na hawaruhusiwi wala hawapewi kibali cha kujenga. Kwa miaka hii miwili wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro kwa miradi ya maendeleo waliyokuwa wamepangiwa, miradi hiyo yote fedha zake zimesimama. Mpango huu utuambie ni Mpango wa Tanzania nzima isipokuwa Tarafa ya Ngorongoro ili tujue wananchi wa Ngorongoro watapangiwa mpango wao lini na kuletwa katika Bunge hili Tukufu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangai unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa ya Kaka yangu, Mheshimiwa Ole-Sendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema maendeleo jumuishi, maana yake tunalenga zaidi wale ambao wako nyuma kimaendeleo ambao ni watu wa vijijini ambao wanategemea kilimo. Kwa hiyo, niiombe Serikali kuhusiana na suala hili la Tarafa ya Ngorongoro pamoja na suala la Tarafa ya Loliondo na Sale, ni muhimu sana Serikali iangalie namna wale wananchi wanaangamia. Waziri aje na mpango mzuri wa kuwajali na wao kwa sababu ni Watanzania wanahitaji maendeleo. Tunaposema uchumi mzuri, ni lazima tunawaongelea na wao, lakini sasa tutakuwaje na maendeleo jumuishi kama kuna watu bado tunawauzia mifugo, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la *infrastructure; coordination* yetu katika Wizara zetu, Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Rais alitangaza *Royal Tour,* lakini sasa hivi ukienda kwenye hifadhi zetu, nitolee mfano, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro pale getini. Wazungu hawataki silaha getini, kule ni *hospitality industry,* ni watu ambao wanaenda kwa starehe, lakini wanapoenda getini wanakutana na watu wenye silaha wanashangaa. Tutengeneze mifumo ya utalii ambayo itasaidia nchi yetu kupata mapato makubwa na Wazungu wanaokuja waende na kurudi tena. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili hiyo.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya pili?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na mchangia niliyemtaja kuna taarifa ya wageni waliopo Bungeni, ambao ni wageni sita wa Mheshimiwa Nicodemas Maganga ambao hao ni Madiwani wa Viti Maalum kutoka Mbogwe, Mkoa wa Geita; kuna Ndugu Salome Lukas, Ndugu Rahma Salum, Ndugu Pili Meshack, Ndugu Ndabacha Simon, Ndugu Lucy Samwel na Ndugu Ester Mihayo. Karibuni sana wageni wetu ambao ni Madiwani kutoka huko Mbogwe, Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Tunaendelea na mchangiaji anayefuata ambaye ni Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, baadaye Mheshimiwa Engineer Samwel Hhayuma, ajiandae na Mheshimiwa Joseph Kamonga.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye hii

taarifa au Mwongozo wa Mpango kwa maana ya maandalizi lakini na kwa Taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Naungana na wenzangu kumpongeza sana Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu kwa kazi nzuri anazoendelea kufanya katika kulitumika Taifa hili. Sasa nimesikia kwa namna ambavyo Profesa ameweza kuwasilisha mpango, kusema kweli ni Mpango mzuri isipokuwa kuna eneo ambalo nadhani ni la muhimu sana ambalo Profesa alihitaji kulitia mkazo kuli-*bold*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote ile mojawapo ya kazi yake kubwa inayopaswa kufanya ni kuhakikisha kwamba watu wake wanapata ajira. Sasa kwa Tanzania kusema kweli hilo sasa ni tatizo. Kwa hiyo, ndio maana nilidhani kwamba mpango huu ungeonyesha moja kwa moja kwamba ni kwa kiasi gani Serikali imejipanga kuongeza ajira kwa watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee tu mfano pale Jimboni kwangu Musoma, yaani Musoma Mjini kwenye mambo ya *social service* hatuna matatizo, habari ya afya, habari ya maji, yaani habari ya elimu hatuna shida, lakini shida kubwa iliyopo ni kwamba vijana wetu hawana ajira na hili ni tatizo kubwa sana. Kulikuwa na Viwanda kama *MUTEX* vya nguo vimekufa, kulikuwa na Kiwanda kikubwa cha Maziwa kimekuwa, kulikuwa na Viwanda vya Samaki vimekufa. Kwa hiyo, leo usishangae kuona unatembea hata saa saba za usiku unawakuta vijana wanacheza *pool,* ni kwa sababu hawana ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilidhani huu mpango ulikuwa ni lazima uoneshe kwamba ni kwa kiasi gani utaweza kuwasaidia vijana wetu waweze kupata ajira. Kusema kweli nimeona hata katika maeneo mengine hata kule kwa wenzetu kule Tarime, niliona kwa sababu ya watu kutafuta ajira mpaka wakaingia kilimo kibaya cha bangi lakini Serikali ilichofanya ni kwenda kufyeka halafu somo likaishia hapo. Kwa hiyo, lazima tuone kwamba ni kwa kiasi gani tunaweza kujipanga kuhakikisha kwamba tunawasaidia vijana wetu ili wapate ajira kwa sababu hilo ndiyo jukumu kubwa la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Waziri wa Mipango umeweza kuzungumza hapo ukagusa kidogo kwamba

katika vipaumbele vyako, Serikali ijielekeze zaidi katika kilimo. Ni kweli kwamba kilimo kitasaidia kwa sababu kinachukua, kinaweza kuajiri watu wengi zaidi, nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Waziri wa Kilimo kwa kazi kubwa na nzuri anayoendelea kuifanya. Pamoja na hii kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya bado tunasafari ndefu, kwa maana kwamba watu wanaoingia kwenye ajira kila siku ni wengi ukilinganisha na kiasi cha ajira kinachotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye taarifa hapo tumeona kwamba hata lile deni la Serikali sasa unajua tunaelekea kugota kwenye 100 ambapo sasa *up to 25* tutakuwa kwenye kukopesheka itakuwa ni kazi kubwa. Hata ile miradi mizuri ambayo tumeianzisha *return* yake bado itachukua muda kuanza kupata *return,* kwa hiyo, bado tunayo kazi kidogo. Ushauri wangu sasa pamoja na hizi juhudi kubwa ambazo zinachukuliwa ni vizuri sasa tukaweza kuangalia na ile miradi ya *quick win* inayoweza kuleta matokeo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu lengo letu saa hizi tunaandaa mpango, tunatengeneza mapendekezo ya mpango, mimi nilitaka nilete mapendekezo ya mpango na uwe *specific* kwa Mkoa wa Mara, endapo huo mpango utakubalika basi tuone namna ya kuuelekeza katika mikoa mingine yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ule mpango wa *quick win* ambao nadhani unaweza ukaleta matokeo mazuri umejikita tu katika maeneo mawili, eneo la kilimo na eneo la ufugaji wa samaki, maana kwenye samaki hapa kwanza nilishasema katika bajeti iliyopita, nikasema hii kama hatuwezi kuunda Mamlaka wale samaki lile Ziwa litakuwa tu ni maji ya kunywa na kuogelea lakini tukiunda Mamlaka maana yake samaki watahifadhiwa watu wetu wataweza kuendelea kuvua samaki kwa utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba jiandae kututengea shilingi bilioni 10 kwa Mkoa wa Mara katika bajeti ijayo na katika hizo shilingi bilioni kumi sisi tutazielekeza kwenye kilimo na kwenye ufugaji wa

samaki. Tukizielekeza upande huo nina uhakika kwamba kwa mpango ambao mimi nimeshaufanyia utafiti, kila mwaka tutaweza kupata ajira za moja kwa moja zisizopungua 4,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ombi langu kwako ni moja tu kwamba Mheshimiwa Waziri utakaposimama hapa utuambie kwamba hii *investment* ya shilingi bilioni 10 kwenye *direct* ajira ya 4,000 mpaka 5,000 *is that project viable or not?* Kama ni *viable,* mimi nitakachokiomba ni kitu kimoja tu kwamba sasa nitakapotoka hapa ule mpango ambao nilishauandaa nitamshirikisha *RC* wangu pamoja na ma-*DC*. Tukishamaliza, Mheshimiwa Waziri wa Mipango uje Musoma uje pale Mara sisi tukuoneshe kwamba ni kwa kiasi gani tumeweza kujipanga kupokea hizo fedha ambazo zitaweza kuajiri vijana wetu wasiopungua 4,000 kila mwaka na kwa kufanya hivyo tunadhani kwamba tatizo la ajira tutakuwa tumelipunguza kwa Mkoa wa Mara lakini tuone ni namna gani tunaweza kulipunguza katika nchi nzima ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema kwamba kati ya wadau ambao nategemea kuwashirikisha nimesema Mkuu wa Mkoa nikasema na ma-*DC* nikasema lakini pamoja na ndugu zetu wa Magereza pamoja na JKT. Tukifanya hivyo basi tunadhani kwamba tunaweza tukaajiri vijana wengi zaidi na hili tatizo litapungua. Kwa sababu leo unapozungumza habari ya kilimo, uko ule mpango wa muda mrefu kama huo wa kuchimba mabwawa, uko huo wa visima lakini kwa Mara sisi Ziwa Victoria lile, yaani ni kwamba tuna mbuga za kutosha. Ukienda pale Mto Mara tunamabonde ya kutosha, yaani pale kinachohitajika leo ukizungumza habari ya *irrigation* pale inahitaji *power* pamoja na ule mtambo unalima tayari maisha yanaendelea au ukizungumza habari ya *hose irrigator* yaani ni vitu ambavyo havihitaji habari ya mitaro, ni vitu ambavyo havihitaji hata hayo mambo ya *feasibility study* kwamba maji yatateremkaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndiyo maana mimi nasema nimalize tu kwa kusema kwamba utakaposimama mimi nataka tu jambo moja. Moja kwamba *investment* ya shilingi bilioni 10 kwa vijana 4,000 uniambie kama *the project is not viable or it is viable,* kama hiyo *project* inalipa ukubali kuja kupokea mpango

na kama ukishakubali kupokea mpango, tukishajiridhisha na wewe ukaukubali basi tuuweke kwenye utaratibu na Waziri wa Fedha awe tayari kutulipa ili tuweze kupunguza tatizo la ajira kwa watu wetu. Kwa hiyo tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo itakuwa imetusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye hili suala nilililoomba la kuwa na Mamlaka ya Uvuvi. Leo wote ni mashahidi ukienda katika mbuga zetu zote za wanyama pamoja na changamoto zote zilizopo lakini ni kwamba hifadhi zetu zinao wanyama wa kutosha na ni kwamba zinakidhi vigezo vyote vya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiliangalia lile Ziwa Victoria ni Ziwa kubwa sana lakini ni kwamba kutokana na lile Ziwa kushindwa kuwa na usimamizi madhubuti ndiyo maana habari ya samaki imeisha. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Manyinyi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na masuala ya ajira kwa vijana naomba pia apate taarifa na atambue mchango wa Serikali kwamba Serikali hii imeamua kujenga Vyuo vya *VETA* kwa ajili ya kuwasaidia vijana katika Wilaya zote lakini pia katika miradi mikubwa yote ya maendeleo ni kipaumbele kwa vijana ambao ni *unskilled, semi-skilled* na *skilled* wanapata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo Mheshimiwa Rais pia ametoa fedha kwa ajili ya *program* mbalimbali za uanagenzi pia *apprenticeship* lakini pia za kukuza ujuzi na *recognition of prior*

*learning* ambazo hizi zote zinawa-*involve* vijana ambao walikuwa na changamoto ya kutambulika labda pengine kwa sababu ya sifa za kielimu. Pia ipo mikopo ambayo imeendelea kutolewa kwenye Halmashauri mbalimbali ya asilimia10. Asilimia Nne kwa ajili ya vijana pia asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu, yote hii imeendelea na tunairatibu sasa ili ianze kutolewa katika utaratibu wa kibenki kwa wale ambao hawana ajira waweze kupata na kuendeleza biashara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwa taarifa ni kwamba tunayo taarifa ya Mheshimiwa Rais kupitia TAMISEMI, hivi karibuni anaenda kutoa ajira 11,000 kwa ajili ya vijana kwenye Sekta ya Afya, ajira 11,000 kwa ajili ya Sekta ya Elimu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Mbunge anaendelea vizuri kuchagiza kwenye eneo la kuongeza kasi kwenye ajira atambue pia mchango wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana Mheshimiwa Naibu Waziri, mdogo wangu ametumia dakika tano nzima kwa ajili ya hoja yangu lakini tuzungumze tu ule ukweli. Mimi nakubaliana kwamba Serikali imeweka mikakati mingi ambayo inayoza ku-*create* ajira lakini tuende kwenye hali halisi. Tukienda kwenye uhalisia ukilinganisha namba za watoto vijana ambao wanaingia kwenye ajira mfano kwa Musoma Mjini kila mwaka siyo chini ya vijana 2,000 wako tayari kuingia kwenye ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni wangapi hao ambao wanaopata ajira? Kwa sababu ukizungumza yaani pamoja na kwamba wako vijana ambao wanaingia kwenye ajira kulingana na juhudi za Serikali lakini ukija kwenye *percentagewise* Mheshimiwa Waziri haivuki hata asilimia tano. Kwa hiyo, ndiyo

maana na sisi tunazungumza mipango ya ku-*compliment* kwenye hizo ajira zinazopatikana ili vijana wengi zaidi waweze kuajiriwa na maisha yao yaweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lile la samaki kama nilivyosema kwamba ile Mamlaka ya Uvuvi itawezesha kuhakikisha kwamba inaweka utaratibu madhubuti wa kuangalia wale samaki namna ya kufanya waendelee kukua, waendelee kuwa *sustainable*. Pale Mjini zaidi ya viwanda vitano vimekufa kwa sababu hakuna Samaki, kwa hiyo, tusipoweka mpango wa Mamlaka inayoweza kusimamia maana yake ni kwamba ajira itaendelea kuwa tatizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedastus Manyinyi. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma, Mheshimiwa Joseph Kamonga na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani wajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Mpango wetu. Kwenye Mpango wakati Mheshimiwa Waziri wa Mipango anawasilisha hotuba yake, kwenye ukurasa wa 20 aliongea kwamba, "Tutaongeza uzalishaji na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi kupitia kilimo, mifugo, uvuvi na madini."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni wazo zuri sana, hii mimi likanisukuma niangalie je, kwenye mpango huu suala la ardhi limeangaliwa kiasi gani? nilivyomsikiliza Waziri wakati anawasilisha sikusikia neo ardhi lakini nikaenda kwenye Mpango nimebahatika kupitia ukurasa wa 100 yote yanayoripotiwa ni ambayo yamekwisha kufanyika kwa sehemu kubwa. Ukiangalia zimetumika shilingi bilioni 17.2 kwa ajili ya upimaji wa vijiji lakini katika kurasimisha na viwanja 118,045 kwa mwaka 2020/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea tena kwenye kuimarisha mipaka ya kimataifa. Mpaka kati ya Kenya na Tanzania umetumia kwa mwaka 2020/2023 shilingi bilioni 1.75 na ukiangalia mambo yote yaliyogusa ardhi ni yale ambayo yamekwisha kufanyika. Ukisikiliza Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wamechangia inaonyesha tunatatizo kubwa sana kwenye eneo la ardhi. Ardhi ya kilimo, ardhi ya mifugo kuna changamoto kubwa, ardhi ambayo tunaihifadhi kwa ajili ya misitu changamoto ni kubwa. Eneo hili ninaamini kwamba kwenye mpango ilipaswa kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea wananchi wangu wa Kijiji cha Diloda, Kata ya Gidafira wote wamechomewa nyumba zao wakisema kwamba eneo lile ni hifadhi. Sasa tuna Kitongoji tumefanya uchaguzi 2019, tumeweka Mwenyekiti wa Kitongoji na viongozi wote wa Serikali wanaohusika. Kwenye ramani ya vijiji Kitongoji hicho ni sehemu ya Kijiji, unaenda leo Maliasili na Utalii unasema hili ni eneo la msitu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi imani yangu ni kwamba tukitibu tatizo la ardhi, maendeleo mengine yanaweza yakawa ni rahisi. Tunaweza kuwa na maeneo ya uhakika ya kilimo, tunaweza kuwa na maeneo ya uhakika ya wafugaji lakini pia hata uvuvi kwa sasa kwa sababu tunataka kuchimba mabwawa, tunaweza kuwa na uhakika na maeneo ya kuchimba madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme Mpango lazima uangalie vizuri eneo la ardhi, lakini kuhusu eneo hili ambalo Wananchi wamechomewa nyumba zao. Ninaomba Serikali i-*act* haraka kwa sababu wananchi hawa kwa sasa hawana makazi, wananchi hawa nyumba zao zimechomwa na mazao ndani na ambayo ilikuwa ni chakula. Mbegu zao zimechomwa ndani lakini pia mavazi yao kwa sababu walifukuzwa na nyumba zikachomwa watu hao hawana mavazi. Hayo yote ni mambo muhimu katika maisha ya binadamu, watu hawa wamekoseshwa haki zao tena kipindi kigumu kipindi ambacho mvua inanyesha, watoto wadogo wanalala nje, mama wajawazito. Naomba Serikali kwenye eneo hili iliangalie kwa kina na watu hawa waweze kusaidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli ni hifadhi, ukiuliza upande wa Hanang' upande wa Manyara wao wanasubiri kuweka *beacon* ya mipaka kwa sababu kuna utata wa mpaka kati ya Singida na Manyara hakuna alama zinazoeleweka, Manyara au Hanang' hatujawahi kukaa vikao vyovyote kutenga eneo la Hifadhi ya Msitu! Ninaomba eneo hili liweze kushughuliwa haraka ili watu hawa waweze kusaidiwa na wasiendelee kukaa kwenye mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kuchangia kwenye mpango wetu, pamoja na malalamiko haya ya wananchi wangu, nitambue kazi nzuri ambayo imefanyika kwenye eneo la kilimo. Kilimo inaajiri watu zaidi ya asilimia 65 lakini ninafarijika sana ninavyoona kwamba yenyewe ndiyo inayoongoza kwenye Pato la Taifa. Tuendelee kuwekeza, tuendelee kuboresha eneo la kilimo lakini pia tuendelee kuboresha utafutaji wa masoko ya mazao ya kilimo, ili tuboreshe eneo hili kwa sasa ni wakati wa mvua, utaratibu wa upatikanaji wa mbolea lakini mbegu za ruzuku, ili tuweze kupata mbegu bora wakulima wetu waweze kulima ili waweze kuzalisha mazao na waweze kuzalisha kwa tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto baada ya kuvuna. Tumejifunza wakati wa *corona* umuhimu wa nchi kujitegemea. Kipindi kile cha *lock down* ukitaka bidhaa za afya kwa sababu nyingi tulikuwa tunaziagiza toka nje, changamoto hata mafuta nazo tulianza kupata changamoto kwa vitu vyote tunavyoingiza nchini. Kuna umuhimu sana wa nchi kuanza kujitegemea. Maana yake ni nini? Bidhaa zile tunazozizalisha ndani ya nchi tuhakikishe kwamba zinakuwa na soko la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sasa hivi tuna changamoto kubwa ya nakisi ya uzalishaji wa ngano lakini wakulima wakizalisha ngano upatikanaji wa soko ni changamoto kubwa kwa sababu tumeagiza ngano nyingi kutoka nje na kwa hali ya uzalishaji wa nchi yetu bei ya ngano ya nje ni nafuu kuliko ya ngano ya ndani. Changamoto hiyo tunayo kwenye alizeti, tunayo kwenye mazao mengine. Ninachotaka kusema, vile ambavyo vinawezekana kuzalishwa hapa nchini tutoe kipaumbele kwanza, tuwe tumevitumia ili nakisi inayobaki ndiyo tuagize kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mjadala mrefu kwenye suala la zao la ngano. Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe anakumbuka vizuri kwamba wale wanaotumia ngano wanunue ngano yote ya ndani ndiyo wapewe kibali cha kuingiza ngano kutoka nje ya nchi. Ninaomba hilo lifanyike kwenye mazao yote ili kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanakuwa na uhakika wa soko wa kile wanachokizalisha mashambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda hata kwenye upande wa nishati. Wabunge wengi wameongelea, tunayo gesi. Gesi hii husikii sana matumizi yake yakitangazwa. Ukiongea namna ya vituo hivi vinavyopatikana vibali yawezekana ni changamoto au vinachukua muda mrefu. Ninachoomba kile ambacho kinaweza kupatikana hapa nchini tuwekeze na tuweke msukumo mkubwa. Tufanye *marketing* ili gesi iweze kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tuendelee kuagiza mafuta kwa kiasi kikubwa wakati tungeweza kuhamasisha matumizi ya gesi kwenye magari yetu. Tukianza kuna Wabunge wameshasema kwamba magari ya Serikali yawe ya kwanza kwenye suala la gesi. Upatikanaji wa vibali vya kujenga vituo kwa ajili ya gesi urahisishwe na ikiwezekana uwe *fast tracked* ili gesi hiyo iweze kutumika kwa ufanisi na tuache kuagiza mafuta ili hatimae fedha zile ambazo tungezitumia kwa ajili ya kuagiza nishati nje ya nchi izunguke hapa hapa ndani ili tujitosheleze hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mitambo ya kuzalisha umeme, tuhakikishe mitambo yote ambayo inatumia *either diesel* tuibadilishe ianze kutumia gesi ili gesi hiyo iweze kutumika na iweze kutusaidia. Ni muhimu sana kuweka huo msukumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamakaa ya mawe, ni karibuni tumeanza kutumia lakini dunia nzima inafanya harakati ya kuondokana na makaa ya mawe, gesi yenyewe harakati zinafanyika mpaka 2040, 2050 iwe imeondoka sokoni na sisi bado hatujanufaika vya kutosha, lazima tuweke nguvu kubwa kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umeisha?

**MWENYEKITI:** Malizia dakika moja.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naomba nihitimishe kwa kusema hivi, suala la ardhi ni suala muhimu, tuweke mkakati mzuri wa matumizi ya ardhi na yale ambayo yanaathiri watu wetu tuchukue hatua sasa. Tuone namna ya kuwashirikisha Wenyeviti wa Vijiji ambao wanakaa karibu na wananchi ili elimu iweze kwenda sawa sawa. Hawa Wenyeviti wa Vijiji wakati mwingine ndiyo wanaosababisha *confusion* hata kwenye maeneo yetu kwa sababu hawana mishahara kwenye kazi wanayoifanya, tutengeneze mfumo rasmi wa kuwatumia na kuwalipa, hiyo itatusaidia ili kutumia ardhi yetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Samweli Hhayuma. Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Kamonga na Mheshimiwa Emmamuel Peter Cherehani ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kulipongeza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu mwaka huu limepitisha sheria ambayo imerejesha Tume ya Mipango. Halikadhalika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuidhinisha sheria ile na kuitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaye Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo amekaa hapo na ametuandalia taarifa nzuri sana. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Profesa ns Waziri wa Fedha, taarifa zenu nimeanza kuzisikiliza, kwani mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, tumezichambua na ushauri wetu ni kama ambavyo umewasilishwa na Mwenyekiti wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nianze kwa kuangalia eneo la umuhimu wa utafiti katika kuandaa mipango ya maendeleo ya nchi kwa sababu kuna mjumbe mmoja Mheshimiwa Zaytun Swai nilimsikiliza, alitoa tafsiri ya Mpango. Alisema; "kupanga ni kuchagua." Maana yake unakuwa na vitu vingi, unachagua lipi lianze na lipi lifuatie kutegemeana na umuhimu wake na vipaumbele vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naona kwamba eneo la utafiti ni nyenzo muhimu sana katika kupata mipango mizuri. Sasa tukiangalia kwenye Mfuko wa Utafiti wa Maendeleo *(COSTECH)* naona kwa mwaka 2024/2025 kwenye hii taarifa ya Mpango inaonesha kwamba mwaka 2022/2023 fedha ambazo zilitengwa kwa ajili ya utafiti ni shilingi bilioni 4.9 ambayo ni sawa na 0.003% ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kinyume kabisa na lengo la nchi yetu ambapo tumejiwekea malengo ya kila mwaka kwenye pato la Taifa angalau 1% iende kwenye eneo la utafiti. Hii 1% hatujaweza kuifikia. Kwa hiyo, naishauri Serikali vipindi vinavyokuja iongeze bajeti kwenye eneo la utafiti. Katika lile pato la Taifa angalau tuweze kutimiza hii 1% ya pato la Taifa. Kwa sababu tafiti na ripoti mbalimbali zinaonesha kwamba nchi nyingi ambazo zimepata maendeleo, utafiti umesaidia sana katika kuweka mipango ambayo ni madhubuti na endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa utafiti unasaidia sana watunga sera katika kufanya maamuzi ambayo ni sahihi. Kwa mfano, tukiangalia Benki ya Dunia, taarifa yake ya mwaka 2023 inaonesha kwamba Taifa la China limefanikiwa kupata maendeleo makubwa sana kwenye nyanja za afya, elimu, teknolojia na ubunifu kutokana na kuwekeza kwa kiwango kikubwa kwenye eneo la utafiti. Halikadhalika, hata nchi kama vile Rwanda na Korea Kusini zinaonesha kwamba wameweza kuzisaidia nchi zao katika kujenga, kuimarisha na kuendeleza uwezo wake wa ndani. Kwa hiyo, naishauri Serikali yangu iweze kutimiza angalau hili lengo la 1% ya pato la Taifa kwenye eneo la utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyo vyuo mbalimbali hapa nchini; tuna Chuo Kikuu cha Sokoine *SUA,* vinaweza vikatumika katika kufanya tafiti kwenye maeneo mbalimbali. Kwenye eneo la kilimo nampongeza sana Waziri wa Kilimo amekuja na mikakati na mipango mizuri kwenye eneo la kukuza kilimo nchini. Ameungwa mkono na Serikali kwa kuongeza bajeti kwenye eneo la kilimo, lakini kwa kiwango gani tunavitumia vyuo vikuu vyetu kwenye eneo la utafiti ili viweze kuboresha mipango na mikakati ile? *(Makofi0*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, eneo la tafiti naona ni eneo ambalo ni nyeti sana. Litatusaidia katika kuendeleza eneo la kilimo na masoko ya bidhaa mbalimbali hapa nchini. Kwa mfano, eneo la kilimo, tuna hawa watu wa *NFRA,* ukiwaangalia wao jukumu lao la msingi kisheria ni kuhifandhi tu chakula ili kukitokea tatizo waweze kusaidia maeneo yale yenye upungufu wa chakula. Tuna chombo gani ambacho kinasaidia haya mazao ya chakula kutafuta masoko kwa mfano mahindi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri asubuhi amejibu vizuri swali la wakulima kucheleweshewa malipo yao ya mahindi. Alitoa ufafanuzi mzuri na nina imani kwamba Serikali itawalipa, kwa sababu sasa hivi mvua zimeshaanza, wanaanza kilimo, wanazitegemea kwa ajili ya shughuli. Kwa hiyo, tumewaambia watulie, wasubiri maelekezo aliyoyatoa asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tafiti katika maeneo haya ya masoko, kuongeza thamani ya mazao na vitu vingine yatasaidia sana kupata mipango madhubuti ambayo itachangia kwa kiwango kikubwa kuleta maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee eneo la ardhi, mipango miji na maendeleo ya makazi. Tukiangalia eneo hili tunaona linakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinasababisha washindwe kufikia malengo. Tukiangalia kwa mfano eneo la makusanyo ya kodi za ardhi, kuanzia Julai, 2022 mpaka Mei, 2023 malengo yalikuwa ni shilingi bilioni 250.1 lakini ilifanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi milioni 132 ambayo ni 53.2% ya malengo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia changamoto ambazo zinaisababishia Wizara ya Ardhi ishindwe kufikia malengo: moja; uhaba mkubwa wa watumishi. Tuna vyuo vikuu vinatoa wahitimu kila mwaka, lakini ajira zake hazijatoka muda mrefu. Kwa hiyo, Wizara hii ingeweza kuongezewa wapima ardhi, maafisa mipango miji kwa sababu kuna ripoti ambayo inaonesha kwamba kasi ya ukuaji wa makazi holela ni 67%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, makazi holela yanakua kwa kasi na kasi ya upimaji wa ardhi haiendani na kasi ya ongezeko la idadi ya watu. Vilevile, tunatambua kwamba ardhi ikipimwa, kodi itaongezeka kwenye Serikali lakini wananchi watakuwa na usalama wa milki zao, vilevile watakuwa na dhamana ambayo itawawezesha kupata mikopo kwenye taasisi za fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili eneo nadhani tungeliangalia kwa kuongezea vifaa, lakini hata kupitia vile viwango ambavyo tunatoza kodi kulingana na eneo husika na matumizi ya ardhi. Je, ni rafiki? Zinalipika? Ule mfumo ambao tunautumia kudai kodi tungeutumia kama wa watu wa maji, muda ukifika unatumiwa *message* kwenye simu yako na *control number* kwamba unadaiwa kiasi hiki. Huo mfumo ukiwa rafiki, tutaweza kuongeza mapato eneo hili la kodi ya pango la ardhi. Kwa hiyo, napenda kusisitiza kwamba viwango vile viangaliwe lakini mifumo iboreshwe iwe rafiki inamvutia mlipaji kuweza kulipa kodi ya pango la ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile watumishi waliopo natambua kwamba ni chini ya 15% ya mahitaji yote yaliyopo nchini. Bajeti wanayopewa wangeweza kuongezewa ili wapime kwa kasi kubwa sana. Katika hili nampongeza sana Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Jerry Silaa, watu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, wamefanya kazi nzuri sana Makete na Ludewa. Kwa hiyo, naomba waendelee kuongezewa fedha ili wafanye kazi nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile eneo ambalo napenda kuliangazia ni eneo la matumizi ya makaa ya mawe. Tunatambua kwamba kuna makubaliano huko ya Kimataifa ambayo

yanakwenda kuondoa kabisa matumi ya makaa ya mawe ifikapo 2030. Sisi tuna zaidi ya tani bilioni tano ambazo hatujazichimba. Walau Kiwira na Ngaka kidogo tumeanza ambapo Ngaka wanatoa tani 250,000 na Kiwira tani 150,000. Lini tutazifikia hizi tani bilioni tano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiangalia *logistics,* namna ya kutoa mkaa kule unakopatikana mpaka kupeleka kwenye bandari miundombinu nayo bado ni changamoto. Kulikuwa na mpango ule wa kujenga reli inayoanzia Mtwara mpaka *Mbamba Bay,* Tawi, Mchuchuma na Liganga. Sasa mradi huu wabia ambao wanatarajiwa, wanaanza kuangalia sasa Serikali inafanya nini kwenye kuanza kwa mradi wa Liganga na Mchuchuma? Kwa sababu bila kupata uhakika wa mzigo wa kusafirisha tunaweza tukachelewa sana kupata mbia wa kujenga ile reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali yangu iharakishe majadiliano na mwekezaji ili kuwe na uhakika wa mzigo wa kutosha wa chuma na makaa ya mawe kwenda Bandari ya Mtwara. Vilevile, naishauri Serikali yangu iangalie uwezekano wa kupitia hizi sheria hii Reli ya Tazara ambayo inahusisha pia nchi ya Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inawezekama kufanya majadiliano, kungekuwa na tawi pale, litoke Makambako liende pale Liganga ili nayo iweze kusaidia kusafirisha mzigo, kwa sababu siyo mzigo wote utasafiri kupitia Bandari ya Mtwara. Mzigo mwingine unaweza kuhitaji bandari nyingine. Kama itawezekana, itakua njema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, majadiliano yale yafikie kikomo na tuangalie *multiply effects* kwa sababu kuna ajira nyingi pale zimelala na sasa hivi kuna uhaba wa dola, lakini madini yale yamechanganyika na madini ya *Titanium* na *Vanadium* ambayo ni madini yenye thamani zaidi ya mara tano ya chuma chenyewe. Kwa hiyo, ule uhaba wa dola, mradi ule ukianza kwa kiasi kikubwa itakuwa ni mwarobaini. Tunaweza tukapata fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia miradi hii itaongeza pato kubwa sana kwenye Taifa letu na hasa uhaba wa dola kama nilivyoeleza. Kwa hiyo, nashauri kwenye Mpango huu, yale majadiliano yafikie mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda umenitupa mkono. Baada ya kusema hayo machache, nitamke kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kamonga. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo atakuwa Mheshimiwa Emmanue Peter Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunipa nafasi ya pekee leo kunipa uhai wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suuhu Hassan kwa fedha nyingi ambazo anazidi kutuletea majimboni. Nampongeza ndugu yangu Daktari wa Uchumi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa Mpango wake mzuri ambao ametuwekea hapa Mezani kama Wabunge tuweze kuujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, tumepitia mipango yenu yote, ni mizuri; tumepitia mipango na maandiko haya yote yamekaa vizuri kwa manufaa ya wananchi wetu. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa wananchi wa Ushetu, kilio chao cha barabara ambazo zilikuwa hazipitiki kwa msimu mzima kupitia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, mipango yako uliyoileta toka mwaka 2022, wananchi wa Ushetu barabara zao zote sasa zinafunguka, zinapitika, madaraja yanajengwa, hospitali ya wilaya imekamilika, jengo la utawala linaendelea vizuri na shughuli za kilimo, kwa sababu wananchi wa Jimbo wa Ushetu ni wakulima, wanafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nampongeza sana rafiki yangu na ndugu yangu Waziri wa Kilimo, kwa kazi nzuri aliyoifanya

kwa wakulima wa tumbaku hapa nchini. Uzalishaji kwa miaka hii miwili ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imepanda kutoka uzalishaji wa kilo 60,000 lakini leo mwaka 2023 tumeweza kuzalisha kilo milioni 122 zenye thamani ya dola za Kimarekeni zaidi ya milioni 341. Ni uchumi mkubwa ambapo fedha nyingi zimesambaa kwa wakulima. Msimu huu wa 2023/2024 wanunuzi wetu wameweza kuongeza uzalishaji tani 214,000 ambazo tunatarajia kuja kupata zaidi shilingi bilioni 900. Ni fedha nyingi sana. Hongereni sana na tumpongeze sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kuchangia. Nijikite kushauri kwenye upande wa maliasili na upande wa mifugo. Maeneo haya mawili yanatakiwa yaunganishwe yakae pamoja, mifumo yao isomane kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi. Kwenye upande wa maliasili na upande wa mifugo tuna fedha pale tumeziacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijaribu kufafanua kidogo; ukiangalia leo tunahifadhi zetu ambazo zina vivutio na zina Wanyama, na pia tuna hifandhi ambazo hazina vivutio kabisa, hakuna Wanyama, lakini tumeweka gharama ya askari wetu kulinda yale maeneo lakini Serikali haipati chochote. Madhara yake ni kuendelea kugombana na wananchi, kufukuzana na wananchi, kutengeneza matabaka mawili kati ya askari wa wanyamapori na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naendelea kushauri…

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, pale kuna fedha.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maganga.

**TAARIFA**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa ndugu yangu Mheshimiwa Cherehani ni mzuri sana. Kwa kweli tunapoishauri Serikali tufikirie tunaishaurije ili kusudi kukusanya makusanyo mazuri ili kufikia shilingi trilioni 47. Kwa mfano amewatolea mfano askari wa wanyamapori, kweli utakuta Polisi anakusanya na anatoza faini kwa wafugaji, hana *POS*. Anapokata faini kwa wafugaji, pesa anaweka mfukoni. Tunaiomba Serikali itengeneze mpango, ikiwezekana kila askari awe na *POS* ili faini hizo ziwe zinaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Maganga, nami nilikuwa naelekea huko. Nataka nishauri, tuna hekta nyingi ambazo hakuna wanyama, misitu inaendelea kuchoka, fedha zinakusasnywa zinaingia mifukoni mwa wachache. Kwa nini maeneo haya tusiyatengeneze yawe maeneo ya malisho ya wananchi wetu ambao ni Wafugaji ili kupunguza migogoro ya wafugaji na wakulima? Leo kila ukiingia kwenye mitandao utakuta habari kuhusu migogoro ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, mama yangu jana hapa aliongea, migogoro inazidi kuongezeka. Inazidi kuongezeka kwa sababu wafugaji hawana mahali pa kwenda kuchungia mifugo yao. Hakuna. Wafugaji hawana maji, mabwawa hakuna, Wizara ya mifugo mnaiwekea bajeti ndogo ya fedha kwa ajili ya mabwawa. Ongezeni fedha. Fedha zile hatumwombi hata Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba zile fedha, tutengewe tu sasa kwenda kutoza kwenye maliasili ambazo hazina wanyama na vivutio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwa sensa ya mwaka juzi 2021, tuna ng'ombe wasiopungua milioni 36 hapa nchini. Tukisema tu kila mwaka kila kichwa cha ng'ombe tuchangie shilingi 2,000 twende kuchunga kwenye mapori yetu huko

ambayo hayana wanayama wala vivutio, tunaenda kukusanya zaidi ya shilingi bilioni saba kwenye upande wa ng'ombe. Pia tuna mbuzi zaidi ya milioni 24, nao tuweke shilingi 200. Tayari pale tuna shilingi bilioni 4.800. Tuna kondoo wasiopungua milioni 10 na kwenyewe tukasema tuweke shilingi 200, tayari tutakusanya shilingi bilioni mbili; tuna punda wasiopungua milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile ni fedha, lakini wale askari wetu tumeamua kuwapa bunduki wakagombane na wananchi; hakuna watalii, hakuna Wanyama, hakuna vivutio. Kwa nini tusiwape kazi ya kuwalinda wananchi wetu wachunge vizuri, badala ya kukaa na bunduki mle porini, tuwape *POS* tu. Wakae na *POS* mle wawaelimishe wakulima wetu, miti itapandwa vizuri, wafugaji watapata maeneo mazuri. Fedha hizi ambazo ukizikusanya kwa mwaka ni zaidi ya shilingi bilioni 80, zinaenda kuchimba mabwawa upande wa mifugo na uvuvi, zinaenda kuwachimbia wafugaji wetu mabwawa ya kunywesha ng'ombe na zinaenda kuwatengenezea *clinic* ya mifugo. *Clinic* ya mifugo hakuna. Ng'ombe wetu wanapata wapi *clinic?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ranchi ambazo ziko zaidi ya hekta 14 ambazo ni zaidi ya hekari 500,000. Zile ranchi ambazo tunazo ambazo zinalindwa kwa gharama kubwa na fedha nyingi ambazo zinaenda kule, Serikalini tunapata nini? Tunaomba tuzitengeneze Wizara zetu badala ya kumtegemea Waziri wa Fedha atupe fedha. Wizara zipeleke fedha Wizara ya Fedha kwa ajili ya manufaa ya wananchi na Taifa letu kwa ujumla. Tumsaidie Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukiangalia leo hii migogoro imeongezeka, ni kwa sababu wafugaji wengi wamekimbia maeneo yao, wanaenda kutafuta maji na malisho. Wakati tungewachimbia maji kwenye maeneo yao, tukapeleka kule usukumani wakachimba mabwawa makubwa ya maji kwa fedha hizi, wala hatuendi kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu. Kuna haja gani ya kuendelea kugombana na wananchi? Kuna haja gani ya kuwa na kelele nyingi, kila Mbunge analalamika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kila Mbunge anayesimama Bungeni ni kilio cha wakufugaji na wakulima. Leo…

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Iddi.

**TAARIFA**

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba kwenye kata inayopatikana kwenye Jimbo la Ushetu, Mheshimiwa Diwani miaka miwili imepita alikamatiwa ng'ombe wake zaidi ya 1,500 na baada ya ng'ombe zile kukamatwa ziliuzwa na baada ya kuuzwa Mheshimiwa Diwani alienda kufungua kesi na kesi ile akashinda, lakini mpaka leo bado hawajamlipa fedha zake, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa kwa sababu ripoti ile tayari tulishaipeleka kwa Waziri Mkuu na aliipokea akasema ataifanyia kazi, lakini mpaka leo hatujapata majibu yoyote, ni kuongeza migogoro mikubwa kwa wananchi. Migogoro hii tunatakiwa tuiondoe kwa mapori ambayo hayana wanyama na vivutio, tuyatenge kuwa malisho, tukusanywe fedha, Serikali ipate fedha nyingi, na migogoro hii ya wakulima na wafugaji itaondoka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie upande wa Wizara yetu ya Muungano na Mazingira. Wizara ile itafutiwe fedha, hawana hela. Bajeti yao ni ndogo, haitoshi kabisa kwenda kutengeneza pesa. Kwa sababu badala ya kwenda kuzibua, kwa sababu niliona wengi tunasema kwamba wakazibue mito kwa ajili ya kuhakikisha uchafu unaondoka, lakini tugeuze uchafu kuwa pesa. Tuwafanye wananchi wetu wanapoona uchafu, wakimbilie tutengeneze viwanda ili uchafu ukatengeneze fedha. *Plastics* hizi sasa hivi ni hela kwenye nchi za wenzetu. Karatasi zinatua barabarani, kwenye nchi za wenzetu zinakusanywa zinakuwa pesa. Hata uchafu kwenye vyoo vyetu na majiji yetu wanaenda kutupa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile zote ni pesa kwenye nchi za wenzetu. Sasa tunafanyaje? Wizara ya mazingira hawana fedha bajeti yao ni ndogo tutengenezeni, tuwape fedha za kutosha. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu tumekubaliana kwamba fedha ziko maeneo haya. Tuna vijana wenzetu wanaochoma mkaa, kila siku tunawakamata miaka yote, miaka nenda rudi, tangu uhuru na uhuru. Magari tunatumia gharama kubwa. Tuwafanye wale wanaosimama kwenye mageti, wakae na *POS* ya kukusanya fedha badala ya kukaa na bunduki kukimbizana na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana, Wizara yetu ya Mazingingira hawana fedha. Tuwape fedha wakatafute fedha ili uchafu wote unaotupwa barabarani, wananchi wakimbizane kwamba unauzwa kwenye viwanda vyetu vya hapa nchini ili tuweze kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahangaika mbolea, leo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anaagiza mbolea kutoka nje kila mwaka. Kwa nini kupitia ng'ombe zetu, uchafu unaopatikana katika nchi yetu, mazingira haya yote tusafishe wenyewe kwa sababu tukitengeneza viwanda vyetu itasaidia sana. Nawapongeza sana ndugu zangu, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, nawaongezea hili, tumechoka kukimbiza na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechoka kufukuzana na wananchi kwa sababu ya ng'ombe kwamba wameenda kulisha kwa wafugaji wetu. Hili limekuwa donda ndugu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nami naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKINGI – KATIBU MEZANI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tumekamilisha shughuli zetu kwa leo. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameweza kutoa michango yao na kuishauri Serikali kwa ajili ya Mpango wa Taifa pamoja na Bajeti kama kanuni zetu zinavyotutaka Kanuni ya 113. Naamini Mawaziri wote wawili wamesikia na watayafanyia kazi ili tuweze kupata mpango bora na bajeti bora mwaka 2024/2025.

Baada ya kusema hayo, kuna tangazo moja limetoka kwa Katibu wa Umoja Wabunge Wanawake Tanzania ambaye anaomba kuwatangazia Wabunge wote na Watumishi wa Bunge kuwa Tarehe 8 Novemba, 2023 mara baada ya kuahirisha kikao cha Bunge cha jioni, kutakuwa na hafla fupi ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson, Mbunge na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Hafla hiyo itafanyika katika viwanja vya Bunge. Nyote mnakaribishwa.

Baada ya kusema hayo, nawatakia jioni njema. Naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.23 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 8 Novemba, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*